SUPA JACKPOT
TZS.1,048,875,802
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

UKURASA 3



**SAMIA** akutanisha marais wanane Misri kujadili hoja nyeti


Tutawakumbuka sana Sokoine, Mrema na Rais Dk. Magufuli

Ukurasa 17

BUFE
IJUMAA NOVEMBA 11, 2022 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

WIKI YA MWANA - KATAVI ...Mkoa wawekeza kwenye Royal Tour, waanza kushuhudia matokeo chanya

Ukurasa 15

JICHO LA MKUTANONI COP 27

Hoja yaibuliwa kupinga miradi gesi inayoendelea Bara Afrika

Na Mwandishi Wetu

VIONGOZI wanapokutana kujadili jinsi ya kupunguza uzalishaji wa gesi chafu, vizazi vya wakazi wa kwanza wa Kusini mwa Afrika wanaibua wasiwasi kuhusu mradi wa utafiti wa mafuta na gesi.

Viongozi wa kidini pia wanauita kwamba 'ni dhambi; na kutoa wito kwa wajumbe wa COP27 kudhibiti shughuli za kampuni za mafuta.

Katika nchi za Kusini mwa Afrika, Botswana ni mojawapo ya delta kubwa zaidi za bara duniani, mandhari ambayo Umoja wa Mataifa umeitaja 'wa kipekee'' na 'nadra' kwa uzuri wake.

Okavango Delta ni chemichem inayopatikana katikati ya Jangwa la Kalahari. Eneo hilo ni makazi ya baadhi ya wanyama walio hatarini ...

anahudhuria COP27 nchini Misri kama mwanaharakati wa haki za watu wa kiasili.

"Tunajali mazingira na ulinzi wa maliasili zetu, kwa sababu mara [uchimbaji visima unapoanza] kutakuwa na mabadiliko mengi.

Wanyama watahama na tunahofia kupoteza mimea yetu ya kiasili." Serikali ya Botswana ilikataa maombi kadhaa ya mahojiano, lakini Waziri wa Rasilimali Madini, Lefoko Moagi, amewahi kusema kwamba "masharti ya leseni yanahitaji ReconAfrica kuhifadhi mazingira asilia kadiri inavyowezekana na kupunguza ... uharibifu wa asili na rasilimali za kibaiolojia."

Serikali pia inasisitiza kwamba hakuna uchimbaji unaopangwa kwa sasa nchini Botswana - uchunguzi utafanywa kwa njia zisizo za uvamizi.

Lakini Anita anahofia kwamba iwapo uwepo wa mafuta au gesi utathibitishwa, hatimaye uchimbaji wa visima utaongezeka sana.

Askofu Pato ana wasiwasi kuhusu nini kinaweza kutokea. Yeye ni kutoka kwa watu wa Mto San ...

UKURASA 13

# Nipashe

Ijumaa Novemba 11, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581126
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Hatua zaidi kukabili uhaba wa maji Dar

UKURASA 2 NA 10



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja (kushoto), alipokagua visima vya dharura vinavyosafishwa, kufufuliwa na kuunganishwa kwenye mfumo wa huduma ya maji kwa wananchi, eneo la Mwananyamala Komakoma, Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**




Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula (wa pili kushoto) na Meneja Masoko wa GSM, Rukia Yazid, wakizindua rasmi nembo ya siku ya TPSF 2022 jijini Dar es Salaam jana, inayotarajiwa kufanyika Desemba mwaka huu kusherehekea mafanikio ya sekta binafsi nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 3

## CHADEMA YASUSIA VIKAO MAREKEBISHO YA SHERIA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema hakitashiriki katika vikao vya marekebisho ya sheria vinavyoanza leo na kudai kinachopaswa kutangulia ni katiba mpya...

UKURASA WA 5

## WANANCHI 115 WAATHIRIWA KUPASUKA BWAWA LA MGODI

WANANCHI 115 ambao wanaishi katika vijiji vya Nyenze na Ng'wangholo, Kata ya Mwadui Lubumbo wilayani Kishapu, wameathiriwa na tope la Bwawa...

RIPOTI MAALUM

# Wananchi wanapofikia hatua kuweka ulinzi kwenye ugali

UKURASA 4

# Vibali ujenzi vituo mafuta vyasitishwa

UKURASA 2

MICHEZO NABI: TULIWAKAMATA HAPA CLUB AFRICAIN UK. 32
KATUNI UK. 6



Balozi wa Indonesia nchini, Triyogo Jatmiko, akisalimiana na mtoto anayetumia mguu bandia aliyekuwa katika karakana ya kutengeneza viungo bandia na vifaa saidizi katika Hospitali ya CCBRT, wakati mabalozi wa Vietnam, Indonesia na Palestina nchini walipotembelea hospitali hiyo, Dar es Salaam jana. Wengine ni Balozi wa Palestina nchini, Hamdi Mansour AbuAli (mwenye tai nyekundu), Mkurugenzi Idara ya Mashariki ya Kati, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Hemed Mgaza (wa pili kulia) na Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hatua zaidi kukabili uhaba wa maji Dar

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametangaza mpango kabambe wa kutatua tatizo la maji katika mkoa wa Dar es Salaam ambao kwa sasa una upungufu wa lita milioni 120.

Katika mpango huo, amesema mkoa leo unatarajiwa kukabidhiwa magari 25 ya uchimbaji wa visima ambavyo vitasaidia kupunguza tatizo hilo ambalo limesababisha uhaba wa maji na kutolewa kwa mgawo.

Pia amesema Novemba 15, mwaka huu, mikoa saba iliyoko kandokando ya Mto Ruaha, watu wa bonde hilo na wizara sita watakutana chini ya Mlima Kitonga kujadili hatima ya mto huo na uhitaji wa maji kwa wananchi.

Majaliwa aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa visima vilivyofufuliwa kama vinatoa maji kwa ajili ya kutatua tatizo hilo. Aliagiza upatikanaji wa maji zaidi ya lita milioni 540 ili ziada hiyo isaidie kutumika inapotokea mto umekauka.

Waziri Mkuu alisema ametembelea visima hivyo kwa lengo la kuona maeneo ambayo yanaongeza maji katika mfumo wao na kwamba kwa mujibu wa wataalamu wao, Dar es Salaam inahitaji maji lita milioni 540 na uzalishaji uliopo kwa sasa ni lita milioni 520.

"Maana yake tuko chini ya kiwango cha mahitaji lakini kutokana na hali ya hewa na athari za Mto Ruvu na mitambo yetu ya Mto Ruvu kutokupata maji vizuri, kiwango cha maji kimeshuka sana mpaka lita milioni 300. Utaona upungufu wa lita milioni 220," alisema.

Majaliwa alisema baada ya kuona hali hiyo, wataalamu awali walishafanya utafiti wa maeneo mbalimbali wakapata visima 197 vya maji vyenye uwezo wa kutoa maji zaidi ya lita milioni nne.

"Tulivyoona hili tatizo na ile kampeni yetu ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtoa ndoa mama kichwani yenye maana ya kutoa huduma za maji yenye uhakika, akatupatia Sh. bilioni 25 ambazo wataalamu wetu wa DAWASA (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira) walikwenda kuchimba visima vikubwa kule Kigamboni," alisema Majaliwa.

Alisema kwa Kigamboni, mahitaji ya maji ni lita milioni 25, hivyo zilizobaki iliagizwa DAWASA kuzipeleka maeneo mengine kwa sababu Kinondoni, Mwananyamala, Sinza, Ubungo na Kariakoo hali ilikuwa mbaya.

Pia alisema waliagiza visima 197 vifufuliwe na wataalamu wao wamemweleza wiki moja wamehangaika na visima 160 ambavyo vimeongeza lita milioni 29 ambazo zimeingia katika mfumo.

"Nimepita kujiridhisha na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kama hiyo kazi imefanywa na maji yanapatikana tunaendelea kukabiliana na upungufu huo. Kwa sasa uzalishaji wa maji unafikia lita milioni 399 bado hazitoshi kwa sababu tuna upungufu wa lita milioni 120," alisema.

Kwa mujibu wa Majaliwa, Rais Samia alitoa fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya kuchimba maji tayari magari yamenunuliwa na leo yatakabidhiwa na mkoa wa Dar es Salaam utapata magari yasiyopungua 25.

Alisema magari hayo yataongeza kasi ya uchimbaji wa visima katika maeneo ambayo yana maji mengi ambayo yanafaa kwa matumizi ya binadamu na kuingizwa katika mfumo ili mgawo wa maji hayo yaende katika maeneo yote.

Majaliwa alisema wananchi wa Kariakoo, Ilala na Tabata watapata maji kutokana na visima hivyo kuanza kutoa maji. Alisema malengo yao ni kuzalisha lita zaidi ya milioni 540 na tayari kazi hiyo imeanza ya kuhakikisha wanapata wingi wa maji.

"Wananchi tujitahidi kutunza haya maji. Lazima tuwe makini na hawa watabiri, Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) bado hawajatuhakikishia vizuri kwamba tutaanza kupata mvua lini," alisisitiza.

Waziri Aweso alisema wamepita katika kipindi kigumu na ameahidi yeye na watumishi wake kufanya kazi usiku na mchana katika kuhakikisha wananchi wanapata maji.

Alisema msaada ambao wamepatiwa na Rais Samia unawatosha kukimbizana ili mambo yaende vizuri na kipindi hicho cha mapito wamejifunza mambo mengi.

Kwa mujibu wa Aweso, maji yaliyopo ni lita milioni 400 ambayo hayatoshelezi walichokipata watakigawa bila kuwepo na upendeleo katika maeneo ya jijini. Alisema Rais Samia baada ya kuona tatizo hilo alitoa Sh. bilioni 23 ambazo zimetumika kuchimba kisima Kigamboni ambacho kimekamilika na kinaingiza lita milioni 70 katika mfumo.

# Vibali vya ujenzi vituo vya mafuta vyasitishwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeagiza kusitishwa mara moja kwa utoaji wa vibali vipya vya ujenzi wa vituo vya mafuta kwa muda wa miezi mitatu ili wizara zinazohusika zifanye tathmini.

Hatua hiyo ni moja ya maelekezo saba ya serikali baada ya kubaini kushamiri kwa ujenzi holela wa vituo vya mafuta, ukiukwaji wa mipango kabambe ya miji na ugawaji holela wa viwanja vilivyopangwa na kupimwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema kuna ujenzi holela wa vituo hivyo visivyozingatia matakwa ya sheria ya mipango miji na kanuni zake katika mikoa mbalimbali ikiiwamo Dar es Salaam na Pwani.

"Ongezeko hili limeleta malalamiko mengi kutoka kwa wadau mbalimbali na kutishia ustawi sawia wa uendelezaji wa miji na matumizi ya huduma za vituo vya mafuta.

"Kanuni za viwango vya ukubwa wa maeneo kupitia kanuni namba 93 ya mwaka 2018, Kanuni ya 5(i)-(iv) imetoa maelekezo kuwa umbali wa kituo kimoja hadi kingine ni mita 200 kwa maeneo yaliyopangwa na mita 500 kwa maeneo yasiyopangwa," alisema.

Kuhusu ujenzi unaokiuka mipango kabambe, Waziri Mabula alisema wamiliki wamekuwa wakiomba vibali vya kukarabati majengo chakavu mijini na baadaye kufanya uendelezaji kwenye maeneo hayo kinyume cha sheria.

Alisema suala hilo liko katika majiji ya Dodoma, Mwanza, Dar es Salaam, Manispaa ya Morogoro, Iringa na maeneo mengine.

Pia alisema kumekuwa na ugawaji holela wa viwanja vilivyopangwa na kupimwa kinyume cha utaratibu jambo linaloathiri huduma na taswira ya miji nchini huku akibainisha kuwa tatizo hilo limeshamiri Dar es Salaam na Arusha.

"Naelekeza kusitishwa kwa vibali vipya vya ujenzi vinavyokiuka mipango na kusitisha ugawaji viwanja holela unaopelekea taswira ya miji yetu kuharibika. Mfano eneo lililopangwa kuendeleza ujenzi wa maghorofa vibali vifuate mpango," alisema.

Waziri huyo aliagiza mamlaka za upangaji kuhakikisha uendelezaji mpya maeneo ya ndani ya miji na mgawanyo wa maeneo unafuata mipango kabambe iliyoko na mipango kina iliyoandaliwa.

"Naelekeza wataalamu katika ofisi za ardhi kote nchini zisimamie utekelezaji wa mipango kabambe na kuwe na ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha mapendekezo ya mipango kabambe yanatekelezwa," alisema.

Sambamba na hilo, alisema kuna tabia imeibuka hivi karibuni ya watu wenye viwanja vikubwa kufanya taratibu za kuweka michoro ya viwanja vidogo vidogo kinyume cha utaratibu na kuharibu mandhari.

HABARI KITAIFA

# Samia akutanisha wanane Misri kujadili hoja nyeti

Na Jenifer Gilla



NGUVU ya ushawishi na uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan (pichani) imewezesha Tanzania kuwa na mkutano wake wa pembeni wa juu na viongozi wengine kwa nchi za Afrika katika Mkutano wa 27 wa Nchi za Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP27) Jiji la Sherm El Sheikh, Misri.

Marais sita wa nchi na wawili wa mashirika ya kimataifa, walihudhuria kikao hicho kilichojadili kwa kina uwezeshwaji wa nishati jadidifu kwenye mifumo ya pamoja ya nchi za Kusini mwa Afrika (SAPP) uliofanyika Novemba 8, mwaka huu.

Akifungua mkutano huo, Rais Samia alisema miaka 27 iliyopita, nchi hizo zilianzisha kituo cha kuunganisha umeme utakaounganisha gridi na kufanya biashara ya nishati hiyo miongoni mwao lakini ahadi hiyo bado haijatekelezwa kikamilifu ingawa ndoto bado haijafa.

Rais Samia alisema wakati watu wa nchi hizo wanahitaji zaidi umeme, upatikanaji kwa baadhi ya nchi ni angalau asilimia 19 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 48 kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na asilimia 90.5 duniani, hivyo juhudi zinahitajika ili kuziba pengo hilo.

Alisema SAPP ina upungufu wa nishati takribani megawati 6,000 pamoja na kilomita 6,085 za njia za usambazaji na viunganishi, hivyo jitihada za pamoja zinahitajika.

"Kwa hiyo tunakutana hapa ili kufufua mtandao huu na kuupa uhai mpya ili kuzalisha umeme mwingi zaidi, kukamilisha miunganisho na kuimarisha gridi zetu za ndani. Ahadi hii inahitaji rasilimali nyingi za kifedha ambazo lazima tutafute ushirikiano wa kimataifa ili kuhamasisha ndiyo maana tuko hapa," alisema Rais Samia.

Alisema kuunganisha kituo cha umeme wa nishati jadidifu katika nchi hizo kutaendeleza uchumi na kuondoa hewa ya kaboni kwa kuwa asilimia 62 ya umeme wa Kusini mwa Afrika, huzalishwa kutokana na makaa ya mawe.

Rais alisema iwapo nchi za kusini mwa jangwa la Sahara zitaendelea kuchochea matumizi ya nishati jadidifu, kuna uwezekano wa kupungua uzalishaji wa hewa ukaa kwa asilimia 27 na kuwa si kiasi kidogo, ikizingatiwa idadi ya watu na ukuaji wa uchumi vitasababisha viwango vya utoaji wa hewa chafu kuwa visivyo na maana tena.

Katika mkutano huo, wakuu hao walikubaliana hoja tano, ikiwamo kuongeza uzalishwaji wa umeme katika ukanda huo ili kukuza uchumi, wawekezaji na washirika wa kimataifa kuangalia na kutathmini kituo cha umeme cha kikanda na kukuza soko la umeme la SAPP kama njia ya ufadhili wa bei nafuu kwa miradi ya umeme.

Akizungumzia mkutano huo, Waziri wa Nishati, Januari Makamba, alisema Rais Samia aliwaalika marais wenzake wa SAPP kujadili nishati hiyo ili kuongeza uzalishaji wa umeme wa nishati jadidifu na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme huo katika ukanda huo.

Alisema mkutano huo ulitoa kipaumbele kwa umeme wa jua na upepo kwa sababu ndizo rasilimali zilizoko kwa wingi katika maeneo yao na kuna rasilimali za kuzalisha kwa ukubwa umeme huo.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Rais wa Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), ambazo hutoa mikopo ya bei nafuu katika miradi mbalimbali pamoja na wawekezaji taasisi zingine za fedha duniani ambazo rais alipata nafasi ya kushawishi kuhusu fursa zilizoko katika nishati.

# CHADEMA yasusia vikao marekebisho sheria

Na Maulid Mmbaga

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema hakitashiriki katika vikao vya marekebisho ya sheria vinavyoanza leo na kudai kinachopaswa kutangulia ni katiba mpya. Tume ya Marekebisho ya Sheria inatarajiwa kuanza leo mchakato wa kukusanya maoni ya marekebisho ya sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema ni muhimu mchakato huo ukasimamishwa ili kuhakikisha unakwenda kuwa na msaada kwa Watanzania.

"Wasitishe wasisitishe, lakini sisi CHADEMA vikao hivyo vinavyoanza kuanzia kesho 'leo' tumeshatoa maelekezo ngazi ya kanda, ili kushusha kwa mikoa na majimbo kutoshiriki vikao hivyo," alisema na kuongeza:

"Tumefikia uamuzi huo kwa kuzingatia matatizo yetu ya kiuchaguzi msingi wake ni upungufu ulioko kwenye katiba ya sasa," alisema Mnyika.

Pia, alibainisha upungufu wanaotaka ufanyiwe marekebisho, akidai kuwa katiba ya sasa haijaunda tume huru ya uchaguzi, mfumo mzima wa watumishi wa tume kuanzia mkurugenzi na wasimamizi, na kwamba kikatiba wanapaswa kuwekewa mfumo ambao tume ndiyo itawezesha upatikanaji wao.

"Matokeo ya Rais yamezuiliwa kwa katiba kupingwa mahakamani, huwezi kutunga sheria yenye kuruhusu matokeo ya urais kupingwa mahakamani bila kwanza kufanya mabadiliko kwenye katiba, imekataza wagombea binafsi, pia haijaweka utaratibu ambapo chaguzi za chini za serikali za mitaa kusimamiwa moja kwa moja na tume ya uchaguzi," alisema Mnyika.

Aliongeza kuwa katiba haijaweka utaratibu ambao kura yake ya maoni kuweza kusimamiwa na tume huru ya uchaguzi, na kwamba haijaweka pia utaratibu wa maamuzi ya tume kupingwa au kuhojiwa mahakamani katika hatua mbalimbali.

Aidha, alisisitiza kwamba endapo watataka kutibu tatizo la kukosekana kwa uchaguzi huru na haki, wanapaswa kuanzia kwenye katiba, huku akidai kuwa kinachofanyika sasa ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi. Kwa mujibu wa Mnyika, matatizo yao yanayohusiana na uendeshaji wa vyama vya siasa nayo ni ya kikatiba, huku akitoa wito kwa tume kujitokeza na kujiunga kwenye sauti ya kutaka kuondolewa kwa zuwio la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa, jambo ambalo alilitaja kuwa liko kinyume na katiba pamoja na sheria.

"Pia tunakemea utaratibu uliotumiwa na tume ya marekebisho ya sheria, kuruka ngazi za kitaifa za vyama na kwenda kufanya vikao na viongozi wa chini katika mambo ambayo walipaswa kuwasiliana na vyama ngazi ya taifa," alisema na kuongeza:

"Sisi hapa ofisini hatuna barua yoyote kutoka kwa tume ya merekebisho ya sheria ikituomba CHADEMA ngazi ya taifa, maoni au mapendekezo yoyote kuhusu haya mambo ambayo yameruka kinyemela na kushuka ngazi za chini kukusanya maoni ya vyama kuhusiana na mabadiliko ya vyama vya siasa na sheria, utaratibu huu haukubaliki." alisema Mnyika.


## ABBOTT FUND TANZANIA

**(Certificate of Registration Number 00483)**

**PUBLIC NOTICE MADE PURSUANT TO REGULATION 13 (A) OF THE NON-GOVERNMENTAL ORGANISATION ACT (AMENDMENTS) REGULATIONS 2018 MADE UNDER GOVERNMENT NOTICE NO. 609 OF 19TH OCTOBER 2018**

**WHEREAS** Regulation 13 (a) of the abovementioned regulations require that all non-governmental organisations in Tanzania publish biannually funds received and their expenditure in a widely circulated newspaper which are accessible by the targeted beneficiaries as part of financial transparency and accountability compliance requirements.

**IN VIEW OF THE ABOVE**, we wish to make the following public disclosure of the funds approved for 2022 activities and their proposed expenditure, which publication covers the reporting period from 1st July 2022 to 31st December 2022:

| Project Area Expenditure | Amount in (USD) |
|---|---|
| **Muhimbili National Hospital Sustainability Strategy Support:** Includes support to LeadershipCapacity-Building | 200,000 |
| **Emergency Medicine Regional and District Amplification:** Includes support to MNH EmergencyMedicine; Infrastructure project at Chalinze District Hospital | 630,000 |
| **Village Emergency Care Model** | 225,000 |
| **Building Livelihoods**: Includes National Children's Centre Infrastructure Project (Dodoma) | 285,000 |
| **Administration:** Includes travel, office costs and program implementation staff | 1,763,000 |
| **Total Funds received from Abbott Fund, Chicago IL, USA for the year 2021** | **3,103,000** |

**ISSUED BY**
**EXECUTIVE DIRECTOR**
**ABBOTT FUND TANZANIA**

2171142302



Tanzania Human Rights Defenders Coalition
[THRDC]
P. O. Box 105926 Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 769 642 208 E-mail; info@thrdc.or.tz
Website: www.thrdc.or.tz

**KUMB: THRDC/AGM/Vol.1/2022**

**NOTISI YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA MOJA WA WANACHAMA (THRDC)**

Kwa wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Wanachama wa Mtandao 2022.

**Ndugu Mwanachama,**

**HII NI TAARIFA RASMI KWAMBA;** Mkutano Mkuu wa Kumi na Moja (11) wa Wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) utafanyika wa siku ya **Jumamosi tarehe 10 mwezi wa 12** kuanzia saa nane Alasiri mpaka saa kumi na moja jioni katika ukumbi wa Kisenga – LAPF Tower Kijitonyama jijini Dar es Salaam na kwa njia ya Mtandao.

**Ajenda zifuatazo zitajadiliwa:**

1.1 Kuhakiki Akidi ya Mkutano Mkuu waliohudhuria
1.2 Kufungua Mkutano
1.3 Kuthibitisha na Kupitisha Ajenda
1.4 Kuidhinisha Kumbukumbu za Mkutano Uliopita wa mwaka 2021
1.5 Yatokanyo na Mkutano uliopita wa mwaka 2021
1.6 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya 2021
1.7 Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa ya mwaka 2021
1.8 Taarifa ya mpango kazi mwaka 2023
1.9 Taarifa ya mpango mkakati wa tatu wa Mtandao; 2023 – 2027
1.10 Mchakato wa Ununuzi na Ujenzi wa Ofisi ya Mtandao
1.11 Hali ya Uanachama
i. Kupitisha wanachama wapya
ii. Kufuta wanachama wanaodaiwa Zaidi ya miaka miwili kwa mujibu wa Katiba ya Mtandao
iii. Kuaga waratibu wa kanda waliomaliza muda wao
iv. Kutambulishwa kwa waratibu wapya wa kanda za Mtandao kwa miaka 2023 – 2026
1.12 Kufunga Mkutano.

**NOTISI HII IMETOLEWA RASMI LEO HII TAREHE 10/11/2022.** Tunategemea kupata maoni yenu kuhusu ajenda zilizopendekezwa kabla ya tarehe 25/11/2022.

Sajili ushiriki wako kupitia barua pepe **membersaffairs@thrdc.or.tz** au namba **0743 390452 kabla ya tarehe 29/11/2022**

**Ikumbukwe kwamba, Wanachama waliokamilisha vigezo vya uanachama kama inavyoeleza Katiba ndio watakaokuwa na haki ya kuhudhuria mkutano huu. Inasisitizwa kwamba, gharama za ushiriki wa mkutano huu zitagharamiwa na mwanachama mwenyewe kwa mujibu wa katiba ya Mtandao.**

**Onesmo Olengurumwa**

**THRDC - Mratibu Kitaifa**

2171142302

Board of Directors:
Hon.Rtd Judge Joaquine De-Mello, Silas Nyumba, Dr. Rose Rueben, Maxence Melo, Jamila M. Juma, Hassan Kh. Juma, Edwin Soko, Edward Porokwa, Angela Benedicto.

*Defending Human Rights is not a Crime!*

# Wananchi wanapofikia hatua kulinda ugali

## ■Wenyeji na hofu ya athari kuhamia darasani

**Na Mary Mosha,** ROMBO



Pulceria Marandu (70), mama wa watoto wanane katika Kitongoji cha Kwasuva, Kijiji cha Msaranga wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro, akionyesha choo cha kaya yake na kulalamikia tatizo la kukosekana kwa maji kunakochangia eneo hilo kuwa na harufu kali alipotembelewa na Nipashe wiki iliyopita. **PICHA: MARY MOSHA**

UKWELI ni kwamba hali hairidhishi kijijini Msaranga wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro kutokana na upungufu wa chakula.

Anayelalamika hali iliyotawala, Pulceria Marandu, mkazi wa Kitongoji cha Kwasuva kijijini Msaranga, anatumia kauli: "Ukipika ugali, ukienda chooni au kutafuta sahani chumbani au kuhemea maji, ukirudi wezi wameiba sufuria yenye ugali. Chakula chenyewe tunakwenda kuhemea huko ukanda wa juu kwa kufanya vibarua.

Shida ni nini na kipi kilichotawala? Ni swali kuu ambalo Nipashe inalazimika kutembea nalo kupata ufafanuzi kijijini huko.

Pulceria, mjane na mama wa watato wanane, analalamika maisha yao yamezidi kuwa magumu kutokana na wezi hao ambao kwa sasa wameachana na wizi wa kuku na mbuzi, wamegeukia kwenye wizi wa chakula kilichopikwa.

Mama huyo anasema tatizo hilo jipya kijijini huko limechangiwa na uhaba wa chakula unaowakabili wakazi wa vijiji vingi vilivyoko wilayani humo, hasa kwa ukanda wa chini kutokana na kutokuvuna chakula.

Pulceria anasema kwa sasa hali imekuwa ngumu kwa kuwa hakuna chakula wala biashara wanazoweza kufanya katika kijiji hicho.

"Wengi wetu hujishughulisha na vibarua vya mashambani pamoja na ukataji wa majani kwa ajili ya kuuza lakini kwa sasa hakuna kazi, hatupati vitu kama hivyo, hivyo inatuwia vigumu kupata riziki ya kila siku.

"Kwa sasa mimi siwezi kufanya kazi kutokana na kuumwa, watoto wangu huwa wanakwenda kuhangaika huku na huko, wakipata tunakula, wakikosa tunalala, hatuna uhakika wa maisha. Vibarua wanavyotafuta ni vya kuchimba mashimo na shughuli zozote, hakuna mwenye kazi ya uhakika," anasema.

Anasema tangu mumewe afariki dunia miaka 16 iliyopita, amepambana kuwalea watoto wake, akiwasomesha na kumaliza elimu ya msingi na mmoja kuendelea na masomo ya sekondari, sasa akiwa kidato cha pili, kukiwa na ugumu katika kufanikisha mahitaji ya shuleni.

Suzan Grigori, mjane na mama wa watoto saba kijijini Msaranga, anaungana na mtangulizi wake, Pulceria, kupaza sauti dhidi ya uhaba wa chakula unaowakabili, akibainisha wanakula mlo mmoja kwa siku, huku akiutaja ukame kuwa mzizi wa madhila hayo.

Anasema kuwa wakati mwingine hulazimika kutembea Km 20 hadi 25 kwenda ukanda wa juu kutafuta chakula kutokana, akikiri watoto wake watatu kati ya saba wamelazima kuondoka nyumbani na kwenda kujitafutia vibarua ili wasaidie upatikanaji wa chakula kwa familia yake.

"Licha ya kukipata chakula kwa shida, kuna tatizo la wizi wa chakula, ukipika chakula ni lazima uhakikishe unakilinda na unakula hadi kiishe bila kunyanyuka, hapa hatuna umeme katika kitongoji chetu na wezi wa vyakula ni wengi.

"Kwa kweli hadi sasa hatuwezi kujua ni nani anaiba chakula maana tupo mpakani mwa Kenya na Tanzania na vijana wa kifugaji hutembea tembea huku kwa lengo la kutafuta malisho. Tunashindwa kuelezea nani anayefanya kitendo hicho," anawasilisha kilio chao.

Lucia Corineli (55), mama wa watoto wanne na mkazi wa eneo hilo, anaendelea mazungumzo ya Suzan na Nipashe katika kudadisi kinachojiri kijijini huko, akitamka:

"Ninamshangaa Mungu ninavyoamka salama, maana kulala njaa kwa siku mbili tatu kwangu ni kawaida, na nimelazimika kuwatoa mabinti zangu waliomaliza kidato cha nne wameenda huko kwa ndugu zangu wakawasaidie ili wapate chakula, sitaki niwaone wanavyokufa kwa njaa hapa.

"Kama hali itaendelea kuwa hivi, mimi siwezi kufika mwaka 2023, hakuna maji, hakuna umeme, hakuna chakula. Akipatikana mfadhili, ninaomba anisomeshee watoto wangu ili wakue na wamudu kujitegemea kimaisha.

"Mimi nipo karibuni kufa japo sijakata tamaa, ninalima na kupanda labda mvua itanyesha na nitapata chakula. Tunaomba serikali kuchukua hatua za haraka, kwa sasa kuna wizi mkubwa wa chakula hasa kilichopikwa."

Anasema hatambui watoto wake wako katika mazingira gani ila anachokijua wako katika maeneo mbalimbali wanapata chakula ili asiwashuhudie wakipata tabu nyumbani kwake, hata kupoteza maisha kwa njaa.

Bathalameo Kilau, mkazi wa Kijiji cha Msaranga, anasema kwa sasa njaa haiepukiki, akiomba serikali kupeleka haraka chakula cha msaada ili kusaidia wanafunzi, watu wenye ulemavu, wajane na wananchi wote ambao hawana uwezo wa kumudu gharama za chakula.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kwasuva, Fransic Shirima anasema tatizo uhaba wa chakula linaathiri kwa kiwango kikubwa wanafunzi, akibainisha baadhi yao sasa wanalazimika kukacha vipindi vya masomo na hawana uwezo wa kushiriki masomo ya ziada na michezo kutokana na kutopata chakula.

"Tunaomba msaada wa chakula hasa kwa wanafunzi ili wasome kwa bidii na kufanya mabadiliko katika mitihani yao ya kitaifa.

Pia kuna wizi wa vyakula ingawa tayari tumeshatoa taarifa katika vijiji na tumeahidiwa kuundwa sungusungu kwa ajili ya kutokomeza hilo," anasema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Msaranga, Fratern Arsen anakiri eneo lake la kazi kukabiliana na shida katika upatikanaji wa huduma ya maji, pia kuibuka wizi wa chakula nyumbani.

"Kuna baadhi ya shule zilizoko katika kijiji changu watoto hawali ugali, bali uji, tena kwa siku moja moja. Walimu wanalalamika watoto wanapofundishwa hasa nyakati za mchana wanalala sana na walimu wanapowahoji, hulalamika njaa, unakuta nyumbani alilala bila kula na anakuja huku shuleni nako hakuna chakula, hali ni mbaya, hatujui matokeo ya mitihani hasa ya taifa itakuwaje.

"Kuna utaratibu wa sungusungu unakuwapo, lakini hali kiuchumi ni mbaya, mifugo inakufa. Kwa kweli wananchi wanahangaika," anasema Arsen.

Mathias Assenga, Diwani wa Kisale Msaranga, anabainisha kata hiyo ina kaya 2,201. Kati yake, kaya 1,137 ziko katika hali mbaya kutokana na kukabiliana na uhaba wa chakula, akiwa na mrejesho kwa Nipashe kwamba tayari wameshatoa taarifa kwa mamlaka husika ili kuzisaidia kaya hizo.

"Hali ya wananchi wetu ni mbaya na tayari timu ya wataalamu imefanya tathmini na kubaini hali halisi. Kwa sasa tunangoja mamlaka zichukue hatua ili kuwasaidia wananchi kujinusuru. Watoto wetu hawawezi kusoma vyema, serikali itunusuru kwa njaa hii," Diwani Assenga anasema.

Kuhusu wizi wa chakula, kiongozi huyo wa kisiasa anasema tayari wameshapatiwa askari polisi katika utaratibu mpya wa Jeshi la Polisi kupeleka huduma hadi ngazi ya kata. Anasema askari huyo ameanza kuunda sungusungu katika vitongoji 20 vya kata yao vitakavyosaidia kutokomeza uhalifu, ukiwamo wizi wa chakula.

Mararie Lyimo, Diwani wa Mwengwe wilayani Rombo anasema kinachoshuhudiwa Kata ya Kisale Msaranga, kinavikabili pia vijiji vitatu ndani ya kata yake, kimoja kikiwa katika hali mbaya zaidi na hatua walizochukuliwa ni kuliwasilisha suala hilo kwa uongozi wa halmashauri.

"Tuna vitongoji 12 katika kata yangu, ila hali ya njaa ni kubwa sana katika Kijiji cha Mfuriashi, tulishaongea na mkurugenzi wa halmashauri ili kuandika andiko la kuona namna ya kupata chakula cha bei nafuu kwa ajili ya wananchi," anasema.

Godwin Chacha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, anasema timu ya wataalamu imeshafanya tathmini ya hali halisi, ikibaini baadhi ya kaya zinakabiliwa na upungufu wa chakula kutokana na ukame uliolikumba eneo hilo katika misimu minne mfululizo iliyopita.

"Halmashauri imechukua hatua za kutuma wataalamu kama tulivyoelekezwa na mkoa na tayari tumeshapeleka maombi katika ghala la taifa ili tupewe chakula kwa bei nafuu," anasema Chacha.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, akiwa katika kikao na wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri ofisini kwake mwanzoni mwa mwezi Agosti mwaka huu, aliwataka kufanya tathmini ya kina na kuona kama kuna uhaba wa chakula ili kuomba chakula cha bei nafuu serikalini.

Kiongozi huyo pia alitoa angalizo kwa viongozi hao, akiwataka kusimamia utolewaji wa chakula hicho ili kisinunuliwe na wafanyabiashara na baadaye kuuzwa kwa wananchi kwa bei ya juu.

"Tunatambua kulikuwapo uhaba wa mvua kwa misimu zaidi ya mnne mkoani kwetu. Kwa vyovyote kutakuwa na uhaba wa chakula kama watu hawakuhifadhi vyema chakula.

"Wakurugenzi kwa kushirikiana na wataalamu hakikisheni mnafanya tathmini ya kina katika kila halmashauri, ili kuona namna ya kuandika dokezo la kuomba chakula cha bei nafuu. Hatutawavumilia wafanyabiashara watakaonunua vyakula hivyo na kuja kuuza kwa dei ya juu.

"Na ninyi wananchi, wakati serikali yenu inaangalia suala la chakula cha bei nafuu, msiuze vyakula kwa sasa na acheni tabia ya kuwakaribisha wageni nyumbani kwenu ili kunusuru hali ya chakula," Babu aliagiza.

# Wananchi 115 waathiriwa kupasuka bwawa la mgodi

**Na Marco Maduhu, KISHAPU**

WANANCHI 115 ambao wanaishi katika vijiji vya Nyenze na Ng'wangholo, Kata ya Mwadui Lubumbo wilayani Kishapu, wameathiriwa na tope la Bwawa la Mgodi wa Almasi Mwadui baada ya kingo za bwawa hilo kubomoka.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema alitoa taarifa ya athari za usambaaji wa tope hilo jana wakati wa ziara ya Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko mkoani hapa, akitembelea waathirika wa bwawa hilo.

Alisema tathmini ambayo imefanyika tangu juzi, imebaini jumla ya watu 115 wameathiriwa na tope la bwawa la mgodi huo pamoja na mashamba yenye ukubwa wa ekari 16 kwa kufunikwa na tope na sasa wanaishi ndani ya mgodi.

Sophia alibainisha kuwa nyumba za wananchi hao zimezingirwa na tope, mashamba na visima vya maji vimefunikwa, lakini hakuna mwananchi aliyepoteza maisha.

Akizungumza katika ziara yake, Waziri wa Madini, Dk. Biteko, alisema kubomoka kwa kingo za bwawa hilo la mgodi ni uzembe kwa kuwa tangu mwezi Septemba mwaka huu kulikuwa na dalili za hatari ya kubomoka.

Waziri huyo alisema kwa sasa wanasubiri majibu ya uchunguzi kupitia kamati ambayo imeundwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga ndipo serikali itoe uamuzi wake ili tatizo hilo lisijitokeze tena.

Meneja wa Baraza la Taifa la Udhibiti na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Ziwa, Kayombo Jarome, alisema kuna uharibifu mkubwa wa mazingira ambao umetokea kutokana na kupasuka kwa kingo za bwawa hilo.

Alisema wanaendelea kusubiri majibu kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kujua kama tope hilo lina kemikali ambazo zina madhara kwa wananchi.

Mhandisi Mkuu wa Mgodi huo, Shagembe Mipawa, alikiri bwawa hilo la mgodi kuwa na hitilafu tangu mwezi Septemba mwaka huu na walitolea taarifa kwa uongozi, wakaziba sehemu ambazo zilikuwa zinavuja na wakajiridhisha kuwa lipo salama.

Meneja Mkuu wa Mgodi wa Mwadui, Ayob Mwenda, alisema kitu cha kwanza walichokifanya baada ya kupasuka kwa bwawa hilo, ni kuwahi usalama wa wananchi na kuweka matuta ya kuzuia tope hilo lisiendelee kwenda zaidi kwenye makazi ya watu.

Alisema mgodi huo unaendelea kufanya tathmini ili kujua ni kwa kiwango gani wananchi wameathirika ikiwamo kupoteza nyumba pamoja na mashamba na kuangalia namna ya kuwapatia fidia huku wakiendelea kuwapatia huduma ya chakula, maji na matibabu.

Kuhusu usalama wa tope hilo, Meneja Mwenda alisema kemikali wanazozitumia kwenye mgodi huo hazina madhara kwa binadamu kutokana na uzalishaji wa almasi kuwa tofauti na ule wa dhahabu, hivyo kuwatoa wasiwasi wananchi kuhusu ya afya zao.

# TPSF yaanika mafanikio 10 ndani ya miaka miwili

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) imetaja mafanikio 10 inayojivunia ndani ya miaka miwili, ikiwamo ukusanyaji wa kodi bila kutumia nguvu, kushusha riba sekta kilimo na ongezeko la mizigo kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Vilevile, sekta hiyo imekiri kufanya mazungumzo na serikali yaliyosaidia viwanda vikubwa kupewa kipaumbele cha umeme unaotumia gesi.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSD22) yanayotarajiwa kufanyika wiki ya kwanza ya mwezi ujao.

Alisema yapo mafanikio ambayo wanajivunia ndani ya miaka miwili tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani.

Alisema katika sekta ya utalii licha ya kuwapo wa janga la UVIKO-19, Rais Samia aliitangaza nchi kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour ambayo nchi imechangia ongezeko la watalii ambalo ni mafanikio kwa sekta binafsi.

"Katika sekta ya kilimo, riba zimepungua, zipo benki zimeshusha hadi digiti moja na mikopo inapatikana kwa urahisi, watu wamefungua mashamba kilimo, sekta inatabirika, kwa sasa mkulima ana uhakika wa soko la ndani na nje ya nchi, sekta imepata ruzuku kubwa ya mbolea na imevunja rekodi kwa kuwa na bajeti kubwa mara tatu zaidi ya miaka mingine," alisema.

Kwa upande wa masoko, Ngalula alisema ndani ya miaka hiyo, mipaka imefunguka na biashara kubwa zinafanyika kuliko ilivyokuwa awali.

"Mpaka mwakani tutaweza kusafirisha tani 15,000 za parachichi kulinganisha na tani 8,000 mwaka 2018, tumeongeza soko kubwa la mbuzi kwenda Oman, Kuwait na Falme za Kiarabu ambapo wafanyabiashara mwaka huu, wameweza kuuza zaidi ya Sh. bilioni nane sawa na ongezeko la asilimia 25," alisema.

Katika eneo la viwanda, alisema miaka ya nyuma baadhi walikuwa wakisumbuka suala la marejesho ya kodi ambayo yalisababisha wengine kushindwa kuendesha viwanda vyao, lakini mafanikio wanayojivunia ni wengi wamelipwa na mazingira yameimarika huku sera na mipango ya serikali ikitabirika.

"Mwekezaji anataka akiweka fedha benki iwe salama, ilikuwa mfanyabiashara akiweka fedha yake zinachukuliwa au anafungiwa akaunti, kwa sasa sioni," alisema.

Eneo lingine alilitaja ni la wadhibiti na watoza kodi, ambazo katika miaka hiyo miwili, taasisi hizo zimekuwa siyo wadhibiti bali wawezeshi, wakijikita kutoa elimu na upo urahisi wa ulipaji wa kodi.

Alisema katika sekta ya usafirishaji, walikuwa na kitendawili kupitia Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) ambao ulichukua biashara zote lakini kwa sasa wakala unafanya shughuli zake na sekta binafsi inafanya zake.

Ngalula alisema mafanikio katika Bandari ya Dar es Salaam yanatokana na mabadiliko hayo yaliyofanywa na serikali.

Kwa upande wa sekta ya ujenzi, Ngalula alisema kuondolewa kwa utaratibu wa serikali kufanya kazi za ujenzi wa miradi yake bila kutumia makandarasi (force account) kumesaidia sekta binafsi kupata zabuni.

Mafanikio mengine aliyoyataja ni upatikanaji wa vibali vya uwekezaji ambavyo kwa sasa vinapatikana ndani ya muda mfupi na ndiyo maana wafanyabiashara wengi wanakuja kuwekeza.

Pia alisema serikali imetoa ruzuku kwenye mafuta na kuifanya biashara kuwa himilivu na nchi imeridhia mkataba wa kujiunga na Eneo Huru la Biashara la Afrika (EfCFTA).

Alisema ili kujua sekta binafsi kama imeathiriwa na kukatika umeme, inahitaji utafiti wa kitaalamu utakaoleta majibu kuhusu hilo.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONYESHA NIA: KUBUNI NA KUTEKELEZA PROGRAMU YA KUREJESHA MBINU ZA KUPATA MAHITAJI YA MAISHA KUPITIA UVUVI NA BAHARI KWA AJILI YA JAMII ZA WAVUVI ZA MKOA WA TANGA.**
**REJEA: 00000027**

EACOP Ltd (Kampuni) Tanzania, kampuni ya mafuta na Gesi, inaalika taasisi zenye uzoefu na sifa kuonyesha nia ya kutoa huduma ya kuandaa, kusimamia na kutekeleza ''**Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha Kupitia Kuvua na Uvuvi wa Baharini**'' ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na kusafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**
Kituo cha baharini cha Mradi wa EACOP kilichopo katika Rasi ya Chongoleani, kinajumuisha hifadhi ya baharini ya kituo cha mwisho (Marine Storage Facility), gati yenye kilomita 2 na kituo cha kushushia mizigo. Shughuli za uvuvi za jamii za eneo hilo zitaathiriwa na ujenzi na uendeshaji wa gati ambayo inawezekana ikajumuisha eneo hilo kufanywa kuwa ukanda uliotengwa, ambao vyombo vya uvuvi havipaswi kuwepo

Mpango Kazi wa Uhamishaji watu na Makazi (Resettlement Action Plans) wa nyongeza na Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha vimebuniwa na ukusanyaji wa taarifa za ziada unaendelea ili kuifafanua programu zaidi. Mtaa mmoja utaathiriwa zaidi, mtaa wa pili utaathiriwa kiasi na mitaa mingine miwili itaathiriwa.

Kampuni/watoa huduma ya ushauri/taasisi ya wataalamu, inahitajika kufanya ubunifu wa kina na kutekeleza programu ya uvuvi/Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha Kupitia bahari ikijumuisha ketengo kinacholenga kaya zilizoguswa na mradi na kitengo kinacholenga jamii nzima

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**
Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

1. Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana na utekelezaji wa programu za uendelezaji uvuvi, programu za uvuvi za kijamii na mbinu za kupata mahitaji ya maisha kupitia baharí (mfano kukusanya mazao ya baharí, kuvua, nakadhalika) ndani ya Tanzania

2. Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

3. Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kutekeleza programu za uendelezaji uvuvi, programu za uvuvi za kijamii na mbinu za kupata mahitaji ya maisha kupitia baharí (mfano kukusanya mazao ya baharí, kuvua, nakadhalika) na uzoefu wa kufanya kazi na jamii zinazotegemea mbinu za kupata mahitaji ya maisha kupitia baharí.

4. Mifano ya kazi zinazoonyesha uzoefu wa kufanya kazi zinazofanania na hizo zilizofanywa kipindi cha karibuni, ndani miaka mitano iliyopita toka siku ya tangazo hili
5. Wafanyakazi wataopendekezwa kufanya kazi kwenye mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.

6. Uthibitisho wa kusajiliwa ndani ya kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi au udhibitisho kuwa wa maombi ya kusajiliwa katika kanzi data yameidhinishwa wakati wa kuwasilisha ombi la kuonyesha nia.

7. Mwombaji azingatie Kanuni ya Sekta ya Petroli ya Ushirikishwaji wa Wazawa/Ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe **20 Mb**) saa au kabla ya **saa tisa mchana saa za Afrika Mashariki** (EAT) tarehe **23 Nov. 2022.** Kichwa cha barua pepe kiwe ni **00000027.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

2171424O2

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usitishaji vibali ujenzi wa vituo vya mafuta mwafaka

**KATIKA** maeneo mbalimbali nchini hasa kwenye miji mikubwa na ile inayoendelea kukua, kumekuwa na tatizo la ujenzi holela wa makazi pamoja na miundombinu mingine ya huduma, hali ambayo husababisha sheria, kanuni na taratibu za mipango miji kutokuzingatiwa.

Kutokana na hali hiyo kumekuwa na msongamano wa nyumba ambazo hazijapangiliwa hivyo maeneo mengi kuonekana kutokuwa na mpangilio maalum. Hali hiyo imejitokeza katika miji mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Iringa na Morogoro.

Licha ya kuwapo kwa mpangiilio mbovu wa makazi unaosababisha baadhi ya huduma kama barabara na maji kushindwa kupita kwa urahisi, pia kumejitokeza utitiri wa vituo vya mafuta kandokando ya barabara kubwa na zile za kawaida pamoja na maeneo ya makazi ya watu.

Hatua hiyo imesababisha serikali kuagiza kusitishwa kwa utoaji wa vibali vipya vya ujenzi wa vituo vya mafuta kwa muda wa miezi mitatu ili tathmini ifanyike kwa kuhusisha wizara zinazohusika.

Akitangaza hatua hiyo jana, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema suala hilo ni moja ya maelekezo saba ya serikali baada ya kubaini kushamiri kwa ujenzi holela wa vituo vya mafuta, ukiukwaji wa mipango kabambe ya miji na ugawaji holela wa viwanja vilivyopangwa na kupimwa.

Bila kuuma maneno, Waziri Mabula alisema kuna ujenzi holela wa vituo uliokithiri katika maeneo mbalimbali ambao hauzingatii matakwa ya sheria ya mipango miji na kanuni zake huku akiweka bayana kuwa tatizo hilo kwa kiasi kikubwa, liko katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Ni dhahiri kwamba utitiri wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani umekuwa ukiongezeka kila uchao jambo ambalo linasababisha kuwapo kwa maswali mengi yasiyo na majibu. Kwa watu wenye uelewa na wasio na uelewa wanapokuta vituo vya mafuta vikijengwa kwa kufuatana, wanaweza kujiuliza maswali mengi yasio na majibu.


Katika barabara kuu ya Dar es Salaam - Morogoro, kwa mfano, kuna baadhi ya vituo ambavyo kutoka kimoja kwenda kingine umbali wake hauzidi hata mita 500 hali inayosababisha jamii kujiuliza kama sheria, kanuni na taratibu za ujenzi huo zinazingatiwa. Mbali na vituo katika barabara kuu, hivi sasa kumekuwa na vituo vingi vya mafuta karibu na makazi ya watu. Hali hiyo pia inaibua maswali kama wizara zenye dhamana na mamlaka katika usimamizi wa ardhi na mipango miji, mazingira na nishati zinafuata miongozo iliyowekwa katika utoaji wa vibali kwa ajili ya ujenzi huo.

Kwa mantiki hiyo, swali la kujiuliza ni je, sheria ya ardhi na mipango miji inazingatiwa? Tathmini ya mazingira inafanyika na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) yenye dhamana ya kutoa vibali kwa ajili ya ujenzi wa vituo inazingatia sheria?

Wahenga wanasema kutenda kosa si kosa bali kurudia. Kwa mantiki hiyo, hatua ya serikali ya kutangaza kusitishwa kwa utoaji vibali inaungwa mkono ili kuepusha majanga yanayoweza kujitokeza kutokana na ujenzi huo ambao umeibuka kwa kasi katika kipindi kifupi kilichopita.

Ni vyema wizara husika zikakutana na kuweka mambo sawa ili kuwapo na mwongozo sahihi ili kuepusha maafa yanayoweza kujitokeza hasa katika ujenzi wa vituo katika makazi ya watu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Majaliwa wapo wengi mtaani, hawaja ajiriwa tu kuonekana

**ANGA** la Tanzania liligubikwa na simanzi Jumapili iliyopita, baada ya ndege ya Shirika la Ndege, kampuni ya Precision Air, kuanguka na kuzama kwenye Ziwa Victoria, ikiwa na abiria 19 na wengine 26 kuokolewa. Kati ya hao waliookolewa, 24 walikuwa kwenye ndege na wawili ni majeruhi wa harakati za kuokoa.

Wakati ikitangazwa idadi ya waliookolewa, ndipo likaja jina la kijana Majaliwa Jackson. Kwa sasa, amekuwa kijana maarufu zaidi nchini Tanzania kutokana na kutangazwa na Mkuu wa mkoa huo, Albert Chalamila na baadaye Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Walimtangaza kuwa ndiye aliyeokoa kiasi cha abiria 24 waliotoka hai ndani ya ndege hiyo.

Yeye mwenyewe alisimulia jinsi alivyofanya kila aina ya njia kuhakikisha anawaokoa watu waliokuwa ndani ya ndege hiyo wakihangaika kufungua mlango wa ndege bila ya mafanikio.

Kifupi tu ni kwamba, kijana huyo ni shujaa. Hakuangalia usalama wake yeye mwenyewe, kwani kuikimbilia ndege ambayo imeanguka nayo inahitaji moyo na ujasiri wa hali juu, kwa sababu inaweza kulipuka.

Alibebwa na ubinadamu zaidi na wala yote yanayotokea yeye hakutegemea wala kudhania kuwa yatamtokea.

Kijana wa kawaida tu, kutoka maisha ya kawaida mvuvi mdogo, anayetumia mitumbwi hafifu, bila kujali matatizo yote ya nyumbani na ya kimaisha, akabebwa na roho ya huruma kwa binadamu wenzake bila kujali usalama wake, akaokoa roho za binadamu wenzake.

Wala hakutegemea malipo, lakini tayari viongozi wa watu kadhaa wamekuwa wakiahidi kumpa fedha ambazo ukizisikia ni kama ndogo hivi, lakini kwa Majaliwa ni pesa nyingi sana, kwani inawezekana kabisa hakufikiria wala kuota kuzishika kwenye maisha yake.

Kama vile haitoshi, Rais Samia Suluhu Hassan akaagiza kuwa kijana huyo apelekwe kwenye Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Kijana ambaye ndoto zake za kusoma zilikatishwa na umasikini, leo anakwenda kupata mafunzo, lakini bado akiwa na ujuzi wake wa kuvua samaki na kuogelea.

Tutaongea mengi ya kitendo cha kishujaa alichofanya Majaliwa, lakini ninachoweza kusema ni kwamba, kama ajali ya ndege isingetokea hakuna mtu yeyote ambaye angejua kipaji cha kijana huyo.

Kipaji cha kuogelea kwenye maji kwa ufundi wa hali ya juu na kuweza kukaa majini kwa muda mrefu. Hapa Tanzania si Majaliwa tu, kuna vijana wengi sana hasa mitaani wana vipaji vikubwa na vya ajabu, lakini hawajafikiwa au kutokea tukio linaloweza kuwafanya wafahamike au 'wa-trendi' kwa lugha ya kisasa.

Achilia suala la maji kuogelea, wapo vijana wenye uwezo mkubwa wa kuruka sarakasi, ufundi redio, televisheni, ujenzi, michezo na vingine vingi vinavyofanana na hivyo, lakini bado wamekuwa wakiishia mitaani tu.

Nikisema ufundi redio, siyo kwamba anatengeneza redio iliyoharibika, la hasha! Ila anaweza kuchukua nta na mbao, waya na vifaa vingine akatengeneza redio ikavuta mawimbi na kuongea.

Unashangaa kijana kama huyu akichukuliwa na kuendelezwa kwa mafunzo, anaweza kuwa mtu wa aina gani? Kuna fundi gereji, ambaye akisikia mngurumo tu wa gari anajua lina tatizo gani na haichukui muda mrefu analitengeneza.

Serikali nyingi hasa zilizoendelea zimeshagudua hilo na kufanya utaratibu na kila idara kukusanya vijana wa aina hiyo, wanapowasomesha wanawaletea mafanikio makubwa sana kwenye nchi zao.

Usione nchi zinatengeneza ndege, vipuri, treni, ndege za kivita, silaha za kulinda nchi, majengo makubwa ya kisasa yenye nakshi, wana- michezo mahiri wote wanatokana na mchango wa serikali kutafuta vipaji vilivyojificha na kuvichukua.

Rais ameonyesha mfano kwa kutotaka kipaji hicho kipotee, hivyo wenye majukumu hayo kwenye taasisi mbalimbali za serikali sasa, wana dhima ya kuanza kutafuta mazingira ya kusaka vipaji mbalimbali ili visaidie taifa. Ili nchi ikue na ipate maendeleo kwa karne ya sasa inahitaji wenye elimu na vipaji pia.

HABARI KITAIFA

## Ataka kauli ya serikali nafasi Tanzania kiuchumi

**Na Richard Makore,** DODOMA

MBUNGE wa Ubungo (CCM), Profesa Kitila Mkumbo, ameiomba serikali kutoa taarifa rasmi bungeni ilipo Tanzania kiuchumi.

Alisema taarifa hiyo ni muhimu kwa kuwa kuna taarifa kuwa Tanzania imeshuka na kutaka serikali iweke wazi suala hilo.

Profesa Mkumbo alitoa ombi hilo wakati akichangia hoja kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2023/2024.

Alisema taarifa za Benki ya Dunia (WB), zinaonyesha Pato la Taifa (GDP) kwa sasa ni Dola za Marekani bilioni 67.78, jambo analoamini Tanzania haijashuka kutoka uchumi wa kati.

Aidha, alisema taarifa za WB, matatizo ya ugonjwa wa UVIKO -19 watu 140,000 walipoteza ajira, milioni mbili walipoteza kipato na 600,000 wapo hatarini kukumbwa na umaskini.

Aliomba serikali ipeleke mkakati maalum wa kupunguza umaskini kwa kuwa hali sio nzuri, huku akitaka uanzishwe mpango wa uzazi wa mpango, ili kudhibiti ongezeko la watu.

Alisema takwimu za sensa na makazi ya watu, idadi ya Watanzania imezidi kuongezeka kwa kasi katika kipindi cha miaka 10 iliyopita na kwamba lazima kuwe na udhibiti wa makusudi.

Akichangia mjadala huo bungeni, Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, aliomba kuundwa kamati teule ya Bunge kuchunguza ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere, kwa kuwa kuna mkanganyiko wa taarifa ujenzi wake unavyoendelea.

Alisema kuna taarifa zinasema mradi huo utakamilika 2023 na wengine wanasema mwaka 2024 na kuomba Bunge lichunguze kupata taarifa za uhakika.

Mpina aliomba serikali kumdai mkandarasi anayejenga mradi huo, Sh. trilioni 1.56 ambazo zimetokana kuchelewesha mradi huo, fedha zilizotakiwa kurudishwa kwa jamii (CSR).

Aidha, Mpina aliomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kukagua ili kujua kwanini deni la taifa limeongezeka kwa kasi.



Mtuhumiwa Pinisto Nzali akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, katika Mahakama ya Hakimu Kisutu, jijini Dar es Salaam jana kabla ya kusomewa mashtaka yanayomkabili ya kuchapisha taarifa yenye kuharibu hadhi ya Rais Samia Suluhu Hassan katika mtandao wa Tiktok. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kortini tuhuma za kumdhihaki Rais Samia mtandao wa Tiktok

**Na Grace Gurisha**

MKULIMA Pinisto Nzali (20), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akituhumiwa kuchapisha taarifa yenye kuharibu hadhi ya Rais Samia Suluhu Hassan katika mtandao wa Tiktok ikimwonesha akiimba jambo ambalo halikuwa la kweli.

Nzali, mkazi wa Mkoa wa Morogoro, alifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Ruboroga kwa mashtaka matatu likiwamo la kushindwa kusajili laini ya simu iliyokuwa ikimilikiwa na mtu mwingine.

Akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Sylvia Mitanto, alidai Oktoba 8, 2022 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Nzali alichapisha taarifa yenye kuharibu heshima au hadhi ya Rais ya Samia Suluhu Hassan.

Alidaiwa tarehe hiyo kupitia mtandao wa Tiktok mshtakiwa alichapisha video inayomwonesha Rais akiimba jambo ambalo halikuwa la kweli.

Ilidaiwa pia, Oktoba 10, 2022 mshtakiwa alichapisha taarifa inayofanana na hiyo ikimuonesha Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete akiimba jambo ambalo halikuwa la kweli.

Wakili Mitanto alidai, Nzali katika tarehe tofauti kati ya Oktoba Mosi, 2022 na Oktoba 20, 2022 alitumia laini ya simu ambayo awali ilikuwa inamilikiwa na Benjamani Chaji bila kutoa taarifa ya mabadiliko ya umiliki kwa mtoa huduma.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana tuhuma hizo na Hakimu Ruboroga aliahirisha kesi hiyo hadi leo kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi uliopofikia.

KABWELA — Fadhili Mohamed



# Msajili wahandisi akiri rushwa kikwazo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSAJILI wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), Bernard Kavishe, amesema rushwa bado ni kikwazo kikubwa katika ujenzi na sekta mbalimbali hali inayosababisha watu wasio na uwezo kupatiwa kazi katika maeneo mbalimbali.

Kavishe alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya bodi hiyo na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka 2022/23.

Alisema rushwa bado ni tatizo katika sekta mbalimbali nchini hali ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa baadhi ya miradi kujengwa chini ya kiwango kutokana na kupatiwa watu wasio na uwezo.

"Rushwa bado ni kansa ya taifa katika maeneo mbalimbali. Bado wako watu ambao wanajihusisha na vitendo vya rushwa lakini sisi tunapowabaini tunawafikisha katika vyombo vyenye mamlaka na suala hilo kama vile TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa)," alisema.

Pia alisema mikakati ambayo wamejiwekea hivi sasa ni pamoja na kupunguza maambukizi ya virusi vya ukimwi katika sekta hiyo.

"Sisi tunao mkakati wa kupinga rushwa katika sekta yetu hali ambayo imetulazimu kuwa na sera ya 'Zeo Corruption' katika sekta hii lakini tuna mkakati wa kupambana na maambukizi ya virusi vya ukimwi kwani afya ndiyo kila kitu kwetu," alisema.

Kadhalika, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa vyombo vinavyo husika kila wanapoona kuna viashiria vya rushwa wakati wanapohitaji huduma za kihandisi.

Mhandisi Kavishe pia alisema kikwazo kingine wanachokabiliana nacho ni vishoka walioko katika fani ya uhandisi hivi sasa na kusisitiza kuwa mtu kujifanya mhandisi ni kosa la jinai kama ilivyo kwa mtu kujifanya daktari huku akijua kuwa hana taaluma hiyo.

"Vishoka ni 'crime' (uhalifu) kama ambavyo ilivyo katika tasnia nyingine mtu kujifanya daktari wakati si taaluma yake. Anastahili kushtakiwa na kufungwa kama mhalifu mwingine," alisema.

Kuhusu soko la wahandisi wazawa nje ya nchi, alisema ni zuri kwa kuwa ziko baadhi ya nchi ambazo zimekuwa zikiwatumia katika miradi mbalimbali.

"Jumuiya ya Afrika Mashariki tunayo klabu yetu ya wahandisi na hivi karibuni tutakuwa na kikao ambacho tunakwenda kukubaliana na mhandisi ambaye yuko kwenye nchi mwanachama kufanya kazi nchi yeyote bila kusajiliwa upya," alisema Kavishe.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, aliipongeza bodi hiyo kwa namna ambavyo imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia wahandisi wakati huu ambao taifa likiwa linatekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.




Ofisa Mkuu wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Peter Shewiyo (wa pili kushoto), akizungumza na Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Emmanuel Mjema, wakati wa kongamano la wanataaluma chuoni hapo, jijini Dar es Salaam jana, kuelekea mahafali ya 57 ya chuo hicho kesho. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# CBE yapongezwa kuanzisha klabu ya kodi

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imekipongeza Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa kuanzisha klabu ya kodi kwa wanafunzi ambayo itaelimisha umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi.

Pongezi hizo zilitolewa jana chuoni hapo na Ofisa Mkuu wa Kodi wa Mamlaka hiyo, Peter Shewiyo, wakati wa kongamano la 57 kuelekea mahafali ya chuo hicho yatakayofanyika kesho.

Alisema klabu za kodi ni muhimu kwa ajili ya kuelimisha Watanzania kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ambayo hutumika kwa ajili ya maendeleo kama ujenzi wa vituo vya huduma za afya, barabara na shule.

"Naipongeza CBE kwa kweli mmefanya jambo jema na kubwa sana kuamua kuanzisha klabu ya kodi kwa sababu wafanyakazi wa TRA peke yao hawawezi kuwafikia Watanzania wote lakini kwa klabu hii ya CBE yenye vijana 100, nina uhakika Watanzania milioni moja watapata elimu ya kodi," alisema.

Aliahidi kuwa TRA itashirikiana na klabu hiyo kwenye masuala mbalimbali ya kuelimisha umma kuhusu mambo ya kodi na itakuwa inawachukua kushiriki kwenye maonyesho mbalimbali nchini.

Naye Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Emmanuel Mjema, aliwataka wahitimu wanaotarajiwa kuhitimu kesho wasione kwamba wamemaliza masomo badala yake waone ni mwanzo wa kupiga hatua nyingine zaidi kielimu.

Aliwataka watumie elimu hiyo kuonyesha mabadiliko kwenye jamii kwa kuanzisha biashara na kujiajiri na kuajiri wenzao na kuachana na kasumba ya kutembea na vyeti mitaani kutafuta ajira.

Naibu Mkuu wa chuo, Taaluma, Utafiti na Ushauri, Prof. Tandi Lwoga, alisema lengo la kufanya kongamano hilo ni kuwakutanisha wanafunzi waliopo na waliosoma zamani kujadili mada mbalimbali za kitaaluma.

Alisema kongamano hilo ni muhimu kwani huwawezesha wanataaluma hao kujadili mada zinazoigusa jamii na kiuchumi ili kuchangia na kufikia lengo kuu la nchi la kuwa taifa la viwanda kufikia mwaka 2025.

Kwa mujibu wa Prof. Lwoga, kwenye mahafali ya kesho, wahitimu 1,605 watatunukiwa ngazi mbalimbali za kielimu na aliwataka kuwa wabunifu kwa kuanzisha biashara na kampuni zao kwa kuwa wahitimu ni wengi na soko la ajira ni dogo.

"Wanaotaka kuendelea na masomo warudi hapa kwa sababu tunatoa hadi shahada za uzamili katika usimamizi wa biashara, ununuzi na ugavi, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Jumla ziko programu 13 tunazotoa shahada za uzamivu," alisema Prof. Lwoga.

# Kortini madai kumbaka mwanafunzi mwenzao

**Na Hadija Kitwana,** KILOMBERO

WANAFUNZI sita wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Matundu Hill wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kilombero kwa madai ya kumbaka mwanafunzi mwenzao wanayesoma naye darasa moja.

Wanafunzi hao waliofikishwa mahakamani, ambao wanatarajia kufanya mtihani wa taifa wiki ijayo ni Nice Mayoka (19), Vitalis Kifyoga (17), Mohamedi Manduta (17), Gerald Kivimba (19), Issa Lukulu (19), Paschal Mwakatage (18) wote wakazi wa Idete.

Mwendesha Mashtaka Mkaguzi wa Polisi, Thomas Kamsini, alidai juzi mbele ya Hakimu Bestina Saning'o kuwa Novemba 5, mwaka huu, katika Shule ya Sekondari Matundu Hill, Kata ya Idete, Kilombero mkoani Morogoro, washtakiwa hao walimbaka mwanafunzi mwenzao (jina linahifadhiwa).

Baada ya kusomewa shtaka hilo, walikana kutenda kosa hilo na upande wa mashtaka ulidai hauna pingamizi la dhamana kwa washtakiwa hao.

Hakimu Saning'o aliwataka kila mshtakiwa awe na mdhamini mmoja na atakayetia saini bondi ya Sh. milioni moja na awe anamiliki mali isiyohamishika kwa thamani hiyo.

Washtakiwa hao walikidhi masharti ya dhamana na Hakimu Saning'o aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 8, mwaka huu, kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali.

# EOTF yasaka dawa tatizo la ajira nchini

**Na Pilly Kigome**

MFUKO wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF) unakuja na mkakati wa kuboresha huduma zake ili kuongeza tija na kuwafikia watu wote wenye mahitaji maalum na kuongeza ajira nchini.

Maeneo yatakayoboreshwa ni pamoja na sekta ya afya na elimu kuanzia ngazi ya chekechea, wakijikita kuboresha mafunzo ya ujasiriamali kwa kinamama kwa kupanua kanda katika kutoa elimu hiyo nchini.

Mkurugenzi wa mfuko huo, Stephen Emanuel, alibainisha hayo juzi alipozungumza na Nipashe ofisini kwake wilayani Temeke mkoani Dar es Salaam.

Emmanuel alisema taasisi hiyo kwa sasa inajikita katika kuboresha huduma zake kwa kuwa kumekuwa na uhitaji mkubwa kwa walengwa nchini.

Alisema EOTF inaboresha sekta ya afya kwa kuwa tayari wameshabaini kinamama wengi vijijini wana maradhi yanayotokana na ukaa wa moshi, shida kuu ikiwa ni matumizi ya kuni na vinyesi vya wanyama katika kupikia.

Alisema wanakuja na suluhisho la awali la kutokomeza ama kupunguza matumizi ya mkaa wa moshi ili kupunguza maradhi kwa kinamama hao.

Alisema utafiti uliofanywa na taasisi hiyo umebaini kinamama wengi, hasa vijijini na mijini wanapata maradhi ikiwamo saratani kutokana na matumizi hayo ya kuni na vinyesi wakati wa kupikia kutokana na uwezo mdogo kiuchumi na kukosa njia mbadala salama kwa matumizi ya jikoni.

Alisema wako katika mkakati wa kutengeneza majiko ya kisasa zaidi ya 100,000 ambayo yana uwezo wa kutumia kuni moja au mbili yatakayotengenezwa kitaalamu na watayagawa kwa kinamama kwa hatua ya awali.

Alifafafua katika upande wa elimu, wamekuja na mpango mkakati wa kuboresha elimu kwa kuendelea na ujenzi wa majengo ya shule kuanzia ngazi ya chekechea na tayari majengo manne yameshakamilika katika Kituo cha Kibaha. "Pia tumepanga kuboresha huduma ya watoto yatima kwa kuwekeza miradi mbalimbali sanifu ikiwamo ya ufugaji samaki, kuku na nguruwe pamoja na kilimo cha mahindi, mtama, mihogo na mboga za majani ili kuinua uchumi wao," alisema.

Alisema katika elimu ya ujasiriamali, awali walikuwa wakitoa elimu kwa kuwakutanisha kinamama na kuwapa elimu kwa pamoja.

Alibainisha kuwa kazi hiyo itafanywa kwenye kanda zao, akitoleo mfano Kanda ya Magharibi itakayokutanisha kinamama kutoka mikoa ya Tabora, Kigoma, Mara na Kagera.

# Daktari abainisha hatari ya ndoa za utotoni kiafya

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

DAKTARI wa idara ya kinamama katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Njombe, Shomari Masenga, amebainisha madhara ya ndoa za utotoni, akifafanua kuwa msichana akibeba ujauzito unamweka kwenye hatari ya kupoteza maisha.

Dk. Masenga alibainisha hayo jana alipozungumza na Nipashe akiwa na ufafanuzi kwamba hali hiyo huchangiwa na umri wa mzazi kuwa mdogo, hivyo viungo vya uzazi kutokuwa tayari kubeba ujauzito.

"Binti akiwa ameolewa na kuzaa katika umri mdogo anakuwa katika hatari ya kuzaa kabla ya wakati kwa sababu katika makuzi anaweza akapata matatizo mengi kama vile kuwa na uwezekano wa kupoteza maisha.

"Mtoto huyu pia anakuwa hajakua vizuri, viungo vyake havijakomaa, unakuta ana shida ya macho kwa sababu misuli yake haijakomaa kuona, shida ya kusikia na matatizo mbalimbali za makuzi," anabainisha.

Alisema kuwa kwa sababu ya umri mdogo na kutopevuka kiakili na kimwili, mama atashindwa kumlea mtoto kwa sababu ya hali ya kiuchumi na kushindwa kumpa mtoto haki za kijamii ikiwamo elimu na afya.

"Huyu mzazi ambaye bado na yeye ni mtoto, anaweza akashindwa kumlea huyu mtoto kwa sababu mara nyingi anakuwa hayuko vizuri kiuchumi. Hivyo, atashindwa kumpa haki zake kama elimu na afya," alisema.

Daktari huyo aliyataja madhara mengine kuwa msichana huyo anaweza kupata presha ya uzazi ambayo inasababisha kifafa cha mimba na mara nyingi hulazimika kujifungua kwa njia ya upasuaji kwa sababu nyonga zinakuwa hazijakomaa.

"Tunaposema anaweza kuzaa kwa upasuaji maana yake ni kwamba nyonga zao ni ndogo, ndiyo maana wakati mwingine wanaishia kufanyiwa upasuaji lakini kama atachelewa kwenda kufanyiwa upasuaji, maana yake watapata uzazi pingamizi na uwezekano wa kupata fistula ni mkubwa," anaonya daktari huyo.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akifurahia pamoja na washiriki mbalimbali wa semina ya fursa za uchumi iliyoandaliwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), kwa ajili ya wabunge wanawake jijini Dodoma jana. (Katikati) ni Mkuu wa Uendeshaji wa Benki hiyo, Allelio Lowassa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Spika apongeza mikakati NBC kuinua wanawake

**Na Mwandishi Wetu,**

DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson amepongeza jitihada zinazofanywa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kupitia Chama cha Wanawake Wafanyakazi wa benki hiyo katika kuendesha mafunzo mbalimbali yanayolenga kuwakomboa wanawake dhidi ya vikwazo vya kiuchumi.

Kwa mujibu wa Spika Tulia, jitihada mbalimbali zinazofanywa ili kuwakomboa wanawake kijamii huenda zisifanikiwe vyema iwapo kipaumbele hakitawekwa katika kuwapatia mafunzo yanayolenga kuwajenga kiuchumi.

Spika Tulia alitoa rai hiyo jijini hapo jana wakati akifungua semina ya fursa za uchumi iliyoandaliwa na NBC kwa ajili ya wabunge wanawake.

Kwa mujibu wa Dk. Tulia, kupitia mafunzo hayo, wanawake watabadili fikra zao kuhusu vipaumbele vyao pindi wanapofanya uamuzi mbalimbali wa kiuchumi kwa kuwa licha ya jitihada mbalimbali za wanawake nchini katika kujiongezea kipato, bado kuna tatizo limebaki kwenye namna ambavyo wanatumia kipato chao.

"Nitolee mfano mdogo tu kwenye VICOBA, ni kweli wanawake tunafanikiwa kujiongezea kipato lakini sehemu kubwa ya kipato hiki mara nyingi imekuwa ikielekezwa kwenye matumizi yasiyo ya kipaumbele ikiwamo ununuzi wa mavazi mengi, zikiwamo sare nyingi tunazoshona au kununua kwa ajili ya kila tukio tunalolifanya kinamama.

"Ndiyo maana ninawapongeza Benki ya NBC kwa sababu kupitia wabunge hawa, elimu hii itawafikia wanawake kote nchini," Dk. Tulia alisema.

Spika alisema mbali na kuwasaidia wabunge wanawake ambao pia baadhi yao wamekuwa na udhaifu kwenye nidhamu ya matumizi ya fedha zao, semina hiyo pia itasaidia kuwajengea uelewa kuhusu masuala ya kiuchumi wabunge hao hususani pale wanaposhiriki kwenye mijadala ya kibunge inayolenga kuishauri serikali kuhusu masuala mbalimbali ya kiuchumi yanayowahusu wanawake na nidhamu katika matumizi ya fedha za umma.

"Hivyo, ninatarajia kuona matunda ya semina hii kwenye mijadala mbalimbali inayoendelea hususani kwenye vikao vya Bunge vinavyoendelea. Ninashukuru sana NBC mmefanya kitu sahihi wakati sahihi," alisema.

Awali, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, Mkuu wa Uendeshaji wa Benki ya NBC, Allelio Lowassa, alisema semina hiyo iliwalenga wabunge hao kwa kuwa ni wawakilishi wa wananchi na wenye ushawishi mkubwa kwa jamii, hususan makundi ya wanawake, ili nao wafikishe ujumbe kwa walengwa.

Akizungumiza kuhusu Chama cha Wanawake Wafanyakazi wa NBC (Women Network Forum) ambacho ndicho kilichoratibu semina hiyo, Allelio alisema kinalenga kuwaunganisha na kukuza elimu ya kifedha miongoni mwa wanachama wake ili wakawe mabalozi kwa wanawake wengine.

"Chama hiki pia kimeenda mbali kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa makundi ya wanawake katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kupitia chama hiki, benki pia imeweka utaratibu maalum wa kuwapa nafasi wafanyakazi wanawake ili kushika nafasi za uongozi," alisema huku akibainisha kuwa kwa sasa benki hiyo ina wafanyakazi zaidi ya 900 na kati yao, asilimia 47 ni wanawake.

Katika semina hiyo, kulishuhudiwa maofisa mbalimbali wanawake kutoka Benki ya NBC wakitoa elimu kwa wabunge hao kuhusu mada mbalimbali za kiuchumi ikiwa ni pamoja na usimamizi wa fedha, bima za biashara na maisha na pamoja na hati fungani ya NBC.

# Spika ashtuka athari mabadiliko tabianchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ameitaka serikali kuangalia uwezekano wa kutumia vyanzo vya maji vya uhakika ikiwamo maziwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Tulia aliagiza hayo jana bungeni baada ya Wizara ya Maji kujibu maswali mbalimbali ya wabunge kuhusu masuala ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo yao.

"Kwa ukame unaoendelea nchini, ni muhimu ninafikiri wabunge wameshauri mara kadhaa serikali kutumia vyanzo vya maji vya uhakika, kama maziwa tuliyonayo ni vyanzo vya uhakika, yale maji huwa hayapungui wala kwenda popote.

"Ni miradi mikubwa, inahitaji fedha nyingi, huko mbele lazima tutazame haya mabadiliko ya tabianchi yanahitaji uwekezaji huo mkubwa. Tuanze kidogo kutumia maziwa kuyaweka kama ilivyo kwenye umeme, tuna Gridi ya Taifa na kwenye maji tufanye hivyo kuwe na Gridi ya Maji, ili kwenye maeneo yenye shida ya maji, yapelekwe kutoka vyanzo vingine," aliagiza.

Katika swali la nyongeza la Mbunge wa Mpanda Mjini (CCM), Sebastian Kapufi, alihoji mkakati wa serikali kukitumia chanzo cha Ikorongo kutokana na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kukabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa maji.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, akijibu swali hilo, alisema maeneo mbalimbali nchini yanapitia shida ya maji kutokana na kina cha maji kupungua kwenye vyanzo.

Alisema kuwa kutokana na janga la ukame lililoko, vyanzo vya maji ambavyo vina maji mengi, vitatumika ili kupunguza tatizo la maji kwenye jamii.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Suma Fyandomo alihoji lini serikali itatoa fedha kwa ajili ya Mradi wa Maji wa Kiwira ili uanze kutekelezwa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mahundi alisema serikali imekamilisha mapitio ya usanifu kwa ajili ya mradi utakaotumia chanzo cha Mto Kiwira kupeleka maji katika Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi.

"Hatua inayoendelea sasa ni ununuzi wa mkandarasi na katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetenga Sh. bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa chanzo na utekelezaji wa mradi utafanyika kwa awamu," alisema.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, akijibu maswali yaliyoulizwa na wabunge kwenye kikao cha tisa cha mkutano wa tisa wa Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge ataka utafiti wa dawa za ganzi zinazoua




MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christina Mnzava, ameitaka serikali kufanya utafiti ili kubaini dawa za ganzi au nusu kaputi zinazosababisha vifo kwa wanaojifungua kwa upasuaji.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alisema Wizara ya Afya inapaswa kufanya utafiti huo ili kujua sababu ya vifo hivyo pindi wanapojifungua kwa upasuaji.

Akijibu swali hilo jana bungeni, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema utafiti mbalimbali uliofanyika unaonyesha sababu zimegawanyika katika makundi matatu.

Alitaja sababu hizo ni za nasaba (DNA) zinazohusiana na ganzi lakini sio za moja kwa moja na zenye uhusiano wa moja kwa moja na ganzi.

Hata hivyo, alisema vifo vya namna hiyo hutokea mara chache na ndiyo maana wakati wote wanawashauri wajawazito kuhudhuria kliniki ili kutoa muda wa kutosha kufuatiliwa na pale itakapohitajika kufanyiwa upasuaji usiwe wa dharura.

Dk. Mollel pia alisema jamii inapaswa kuhamasishwa kutoa lishe bora kwa wajawazito.

# 'Mpango maalum unahitajika kukarabati makazi ya polisi'

SPIKA wa Bunge ameitaka serikali kuwa na mpango maalum wa kukarabati makazi ya askari wa Jeshi la Polisi kutokana na baadhi ya makazi hayo kuwa na hali mbaya.

Dk. Tulia Ackson aliagiza hayo jana bungeni baada ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutoa ufafanuzi wa maswali mbalimbali ya wabunge.

Dk. Tulia alisema makazi ya polisi nchi nzima yanahitajika kukarabatiwa licha ya mikakati ya serikali ya kujenga vituo vya polisi.

"Haya makazi hayahitaji ardhi nyingine, makazi yao yana hali mbaya maeneo mengi, hivyo ni muhimu sana kuwa na mpango maalum wa kuyarekebisha makazi ya askari wa Jeshi la Polisi," aliagiza.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu alihoji lini serikali itapeleka Sh. bilioni 1.1 zilizoidhinishwa kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi Ikungi ili ujenzi huo uanze mara moja.

"Tulipitisha hapa bungeni bajeti ya Sh. bilioni 1.1 kwa ajili ya kujenga kituo cha polisi pale Ikungi. Ninavyozungumza leo ni mwezi wa 11 fedha hazijatolewa. Je, ni lini serikali italeta fedha kwa ajili ya kujenga kituo hicho?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alikiri kuidhinishwa kwa fungu hilo kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

"Kinachofanyika ni kwamba Jeshi la Polisi limewasilisha mpango kazi wa ujenzi ambao utakapopitishwa na wizara utawasilishwa Hazina kwa ajili ya kuidhinisha fedha.

"Ni imani yetu fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki kwa vile zinatoka kwenye mfuko ambao tuliuzungumzia kikamilifu wiki iliyopita, zitatoka kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa kituo hicho kuanza," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Naghenjwa Kaboyoka, alihoji lini serikali itaanzisha vituo vya polisi katika Tarafa ya Gonja yenye kata nne na Tarafa ya Mamba/Vunta yenye kata tano ili kuwapunguzia wananchi adha wanazozipata inapotokea uhalifu.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Sagini alisema serikali inatambua umuhimu wa kuwa na vituo vya polisi katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi.

"Tarafa za Gonja na Mamba/Vunta hazina vituo vya polisi wala maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya polisi na nyumba za makazi ya askari, wananchi wa Tarafa za Gonja na Mamba/Vunta hupata huduma za polisi kutoka vituo vya polisi vya Same mjini na Gonja, na vituo vidogo vya polisi vya Kihurio na Ndungu," alisema.



HABARI KANDA KASKAZINI

## Miaka 20 gerezani kwa kukutwa na nyama swala

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKAZI wa Kijiji cha Gedamara, Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Dayu Hassan (30), amehukumiwa kutumikia kifungo miaka 20 gerezani, baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kukutwa na nyama ya swala.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Babati, Victor Kimario, alisema mahakama hiyo baada ya kupitia ushahidi wa upande wa mashtaka na ule wa utetezi, amejiridhisha pasipo shaka kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo kwa makusudi.

Hakimu huyo alisema, mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 86 (1) na (2) (C) (iii) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283 iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2022, ikisomwa pamoja na Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2022.

Alisema mshtakiwa, alikutwa na nyamapori Agosti 24, mwaka huu, katika Kitongoji cha Manyara kilichoko Kijiji cha Gedamara.

"Katika maelezo yake, mshtakiwa alikiri kukutwa na nyamapori yenye uzito wa kilogramu 3.5, sawa na mnyama mzima mwenye thamani ya shilingi milioni 1.032," alisema Hakimu Kimario.

Kwa mujibu wa Kimario, upande wa mashtaka ulikuwa na vielelezo saba, mashahidi watano na upande wa utetezi, mshtakiwa alijitetea mwenyewe.

Awali kabla ya kusomwa kwa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali, Peter Utafu, aliieleza mahakama hiyo kuwa, kwa vile mshtakiwa ana rekodi ya makosa ya uhalifu, anaomba mahakama itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Alipopewa nafasi ya kujitetea, mshtakiwa Dayu, alidai kuwa ana familia inayomtegemea na mama yake amezeeka hivyo anaomba mahakama impunguzie adhabu.

# RC awatangazia vita wenyeviti wanaowapora wananchi mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ametangaza vita dhidi ya wenyeviti wa serikali za vijiji na mitaa, wanaoendesha 'ubambuzi' wa kuku au kunyang'anya mali za wananchi walioshindwa kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo.

Amesema jambo hilo halikubaliki kwa sasa, kwa kuwa tayari Rais Samia Suluhu Hassan, ameshatoa fedha za kugharamia miradi hiyo.

Akizungumza jana na kamati za shule, madiwani, watendaji wa halmashauri na ofisi ya mkuu wa wilaya hiyo, Babu alisema suala hilo halikubaliki na watakaobainika kuhusika watachukuliwa hatua.

"Tumepokea Sh. bilioni 2.5 kwa maana ya kujenga madarasa 125 kwa mkoa mzima. Fedha hizi tumeletewa na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye anahangaika kuhakikisha Watanzania na watoto wao wanapata elimu bora na wanakaa kwenye madarasa mazuri ambayo yametimia.

"Ndiyo maana kwenye ziara yangu hii ya Wilaya ya Hai, nimetembelea na kukagua madarasa sita, kati ya madarasa 10 waliyopewa; nimejiridhisha kwamba manne yako kwenye hatua mbalimbali.

"Fedha hizi si za kufanyia mchezo na si fedha za kupanga matumizi mengine. Ni kwa ajili ya madarasa yaliyokamilika kama yalivyokuwa yameelekezwa na TAMISEMI (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)," alisema.

Kwa mujibu wa Babu, kitaifa serikali imepanga kila mkoa, kukamilisha jukumu hilo la kumaliza ujenzi wa madarasa yote ifikapo Desemba 15, mwaka huu, lakini kwa mkoa wake, amepanga mwisho ni Desemba 5 yawe yamekamilika yakiwa pamoja na madawati.

"Sitaki wakija wakae chini lakini kwa hatua niliyoiona, nimeridhishwa sana na kasi ya ujenzi wa madarasa katika Wilaya ya Hai," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dionis Myinga, akizungumzia miradi hiyo, alisema kwa mwaka huu, wamepewa Sh. milioni 200 za miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 10.

"Mojawapo ya vyumba vinavyojengwa kwa fedha hizo ni miradi inayoendelea kwa kasi katika Shule za Sekondari za Mukwasa, Hai Day na Longoi.

Mwaka jana, tuliletewa shilingi milioni 860, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 43, ambavyo tulivijenga kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19).Tunafanya kazi na tuko katika kasi inayoridhisha na inayoendana na malengo ya mkoa na ngazi ya taifa," alisema Myinga.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (aliyeshika karatasi), akitangaza kuwa Desemba 5 mwaka huu, ndio siku ya ukomo wa umaliziaji wa miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa mkoani humo, baada ya kukagua miradi sita kati ya 10 katika Wilaya ya Hai jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wapewa muda kuondoka Hifadhi Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

JAMII ya wafugaji wa Kimasai, ambayo bado imesalia ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ikiendelea kufanya shughuli za kiuchumi hasa ufugaji, imepewa muda zaidi wa kujiandikisha kuomba kuhama kwa hiari.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala, alisema serikali imeongeza muda kwa wafugaji hao kuendelea kujiandikisha, kabla ya kufikiria kufunga utaratibu huo.

Alikuwa akizungumza jana, wakati wa hafla ya kuwaaga wafugaji 317 wanaohamia katika Kijiji cha Msomera kilichoko Kata ya Misima, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga.


"Wale wanaobaki, ambao bado hawajachukua hatua ni wakati muafaka. Jiandikisheni lakini muwe na subira. Sio uandikishwe leo, utake kuondoka leo, inategemea kwa sababu tumeanza kazi hii tangu mwezi Juni 2022," alisema.

Awali, Naibu Kamishna wa Uhifadhi, Huduma za Mamlaka za NCAA, Needpeace Wambura, alisema wananchi hao wa Ngorongoro waliohama kwa hiari ni kundi la 15.

"Tunazihamisha kaya 50 zenye jumla ya watu 317 na mifugo 1,304. Huko mnakokwenda sasa ni neema zaidi, hamtakiwi kulala.

"Idadi ya wananchi wanaojitokeza kujiandikisha na kuhama kwa hiari, imeendelea kuongezeka kutokana na hamasa na elimu iliyotolewa kwa wananchi, hasa baada ya serikali kujenga kule Handeni miundombinu ya huduma za kijamii kama shule, hospitali, huduma ya maji, majosho, malambo, barabara, nyumba za kuishi, mashamba, nishati ya umeme pamoja na mawasiliano.

"Muende mkafanye shughuli nyingi za kiuchumi ili muweze kujiongezea kipato lakini muweze kutengeneza maisha kwa ajili ya familia zenu."





## Mpango kuwahamisha wananchi waiva rasmi

**Na Mary Mosha,** HAI

MPANGO wa serikali wa kuwahamisha wananchi wa vijiji vitano vya ukanda wa tambarare katika Wilaya ya Hai, wanaodaiwa kujenga makazi ya kudumu na kufanya shughuli za kiuchumi katika eneo linalomilikiwa na Kampuni ya Usimamizi na Uendeshaji ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), umeiva.

Wananchi hao wako katika mgogoro na KADCO na wanadaiwa kuvamia eneo la uwanja huo kinyume cha sheria.

Akitangaza mpango huo jana, wakati wa uzinduzi wa uwekaji alama za mipaka kwenye maeneo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliwasihi wananchi wa vijiji vitano kuwa na utulivu wakati shughuli za tathmini na upimaji ardhi zikiendelea kwenye eneo lenye  kilomita za mraba 110.

"Shughuli ya upimaji ardhi na tathmini itakapokamilika, wananchi ambao watabainika kuingia eneo la uwanja wa ndege wa kimataifa wa KIA, watalipwa fidia zao za ardhi na mali na kutakiwa kuondoka kwenye eneo hilo.

"Wito wangu kwa wananchi wa KIA  na Menejimenti ya wa KADCO tutekeleze agizo hili la serikali ili tujue, ni nani ameingia na ni nani hajaingia eneo la uwanja. Na wale watakaobainika wameingia hawataondoka hivi hivi, wote watalipwa lakini walipwa kwa huruma ya Rais Samia Suluhu Hassan, maana eneo hili lina hati ya miaka 99," alisema.

Kutokana na mpango huo wa serikali, Mkuu huyo wa Mkoa, amewasihi wananchi hao kutowachukia viongozi wao waliowachagua, kwa kuwa kinachofanyika ni uamuzi wa serikali, kwa kuwa suala hilo lina maslahi kwa taifa.

Kabla ya uzinduzi huo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, akizungumza katika eneo hilo alisema: "Kila mmoja tunaomba atoe ushirikiano, hakuna mtu anayemchukia Mtanzania."

Diwani wa KIA, Tehera Mollel, alimwomba mkuu huyo wa mkoa kuhakikisha wananchi watakaoondolewa kwenye maeneo hayo, wanatendewa haki kama serikali ilivyoagiza na kwamba hawawezi kupingana na serikali katika uamuzi uliochukuliwa.

# Askofu ataka ruzuku bei vyakula

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la TAG Kilimanjaro, Glorious Shoo, amesema serikali inapaswa kuandaa mpango maalum wa kupunguza makali ya bei ya vyakula nchini kwa kuweka ruzuku hasa kwenye mahindi ili kuwanusuru watu wake na baa la njaa.

Shoo alikuwa akitambulisha jana kongamano la kimataifa la kuombea ukame, mvua na mabadiliko ya tabianchi linaloendelea katika Uwanja wa Kumbukumbu ya King George maarufu Memorial, ulioko Manispaa ya Moshi.

Kongamano hilo linawahusisha wahubiri wa kimataifa kutoka mataifa ya Norway, Finland, Ujerumani na Tanzania.

"Ni vizuri tukaendelea kuhimiza watu kutumia kwa uangalifu chakula kilichoko ili tuweze kuhifadhi chakula kwa wakati huu, na wakati huo huo ni vizuri serikali yetu ikafikiria namna bora ya kukabili mfumuko wa bei ya vyakula unaoendelea.

"Kwa miezi mitatu sasa, vyakula vimekuwa vikipanda bei bila kushuka na tulitarajia kwamba labda mavuno yanayofanywa kwenye eneo fulani yangefanya bei kushuka, lakini haijatokea na imeendelea kubakia juu," alisema.

Kutokana na athari za kiuchumi zinazotokana na mfumuko huo, Askofu Shoo alisema kwenye suala la mfumuko wa bei, viongozi wa dini wanatamani serikali isaidie wananchi kwenye maeneo mawili. Alilitaja eneo la kwanza ni kusogeza chakula katika maeneo yote ambayo yameathirika na hali ni mbaya.

"Kama serikali ilivyoweka ruzuku kwenye mafuta yanayopakuliwa katika bandari za Tanzania, tunaamini linaweza likafanyika jambo hilo kwenye chakula, kabla hali haijawa mbaya zaidi.

"Ni vizuri tukaendelea kuweka restriction (zuio) kwenye uuzaji holela wa chakula na kwenye matumizi holela ya chakula. Ombi langu jingine ni kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, tunamwomba apige marufuku pombe za kienyeji zinazotumia mazao ya chakula.

"Ziko pombe nyingi sana za kienyeji hazimsaidii mtu yeyote, lakini ukweli bado zinapunguza kiwango kikubwa cha chakula, hasa zile zinazotozotengenezwa kwa kutumia mahindi, mbege na ndizi," alisema.

Aidha, Mwenyekiti wa Baraza la Makanisa ya Kipentekoste ya Mkoa wa Kilimanjaro (CPCT), Askofu Cleopa Kweka, alisema kongamano hilo la Novemba 9 hadi 13 ni mahususi kwa ajili ya kumuomba Mwenyezi Mungu alete mvua na kuzuia mabadiliko ya tabianchi yasiendelee kuwa kikwazo kwa maisha ya binadamu.

"Ni ukweli usiopingika na sasa hivi picha ya Tanzania tunaona jinsi ambavyo watu wana njaa, lakini mifugo ina kufa. Hali ni mbaya na ukiangalia maeneo mengi ya nchi hii, kuna njaa kali. Kwa hiyo janga hili sio linaathiri tu wanyama na viumbe vingine, bali pia binadamu.

"Watu hawana vyakula, serikali ingeangalia namna itakavyowasaidia watu wake, watu wengi wana wakati mgumu sana,"alisisitiza Askofu Kweka.

Katika kongamano hilo, kiongozi wa jopo la wahubiri hao wa kimataifa, Mwinjilisti Daniel Smenes wa Huduma ya Jesus to All Nations, alisema wahubiri waliopata wito wa kuiombea Tanzania dhidi ya ukame ni Lukas Abildsten, Waldemark Berschmeminiski na Patrizia Camnasio.

Mhubiri Smenes alisema: "Tunafahamu mabadiliko ya tabianchi na juu ya janga la ukame na ninaamini ya kwamba kwenye hilo si suala la maombi tu, tunatamani kuwahimiza watu waweze kuyatunza mazingira kwa sababu hilo halihitaji, maombi, hilo linatakiwa wawe ni watu wanaojali maeneo yao au wawajibike."



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Moshi, Faraji Swai (kushoto), akishiriki kujenga maabara katika shule mpya ya sekondari ya Mandaka, alipofanya ziara ya kichama, kukagua miradi ya maendeleo, Kata ya Msaranga, wilayani humo juzi. Shule hiyo, inatarajiwa kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023. **PICHA: MARY MOSHA**

# Madiwani washtushwa bei kubwa mahindi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

KUPANDA kwa bei ya mahindi katika masoko mbalimbali mkoani Kilimanjaro, kumewaibua madiwani wa wilaya ya Siha, kupaza sauti zao wakiomba serikali kuchukua hatua za haraka kuwanusuru wananchi na makali hayo ya bei.

Kutokana na hali hiyo, wamemwomba Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kuelekeza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kufikiria namna inavyoweza kupunguza     makali ya tatizo hilo kwa kupeleka na kuwauzia wananchi mahindi  kwa bei nafuu.

Siri ya kuwapo kwa tishio hilo ilifichuka jana, wakati madiwani hao walipokuwa wakiwasilisha taarifa za kata zao katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani.

Diwani wa Garagua, Zakaria Lukumay, alisema katika eneo lake hali si nzuri kwa kuwa wananchi wanashindwa hata kuchangia gharama ya chakula shuleni na kuna familia haziwezi kupata hata mlo mmoja kwa siku.

"Wazazi walikuwa wanachangia chakula shuleni lakini kwa sasa imekuwa ngumu. Utapelekaje chakula shuleni wakati nyumbani hakuna? Hata mifugo iliyoandaliwa kwa ajili ya kuuza ili kupata chakula, imekuwa tatizo kwa sababu mingi inakufa kwa ukame," alisema.

Aidha, Diwani wa Nasai, Humphrey Kifumu, akichangia mjadala huo, alisema hivi sasa wananchi wake wanapata mlo mmoja kwa siku, kwa kuwa hawana chakula na waathirika wengi zaidi ni watoto, wazee na kinamama.

Naye Simon Shija, ambaye ni Diwani wa Miti Mirefu, aliwaomba viongozi wa madhehebu ya dini kufanya maombi maalum ya kuombea mvua ili wananchi wapande mazao ya muda mfupi na muda mrefu kukabiliana na baa la njaa.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Noel Mollel, alisisitiza ni lazima Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Upendo     Mangali, afanye mawasiliano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kueleza juu ya jambo hilo.

Baada ya maelekezo hayo, Mkuu wa Divisheni ya Kilimo wa Wilaya hiyo, Habibu Abdallah, alisema tayari kumeshaanza kufanyika mchakato wa kushughulikia jambo hilo, ikiwamo kukutana na Kamati ya Maafa ya Wilaya na barua rasmi imeshawasilishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Willy Machumu.

Septemba 22, mwaka huu, timu maalumu inayoshughulikia suala hilo kutoka Wizara ya Kilimo, ilizuru wilaya ya Siha na kufanya tathmini ya kina katika vijiji vitano na kuondoka bila kutoa majibu ya kazi hiyo.

Kwa sasa, bei ya mahindi sokoni  kwa gunia moja katika Wilaya ya Siha  ni Sh. 150,000 na sadolini moja inauzwa kwa Sh. 5,000.

NFRA imekuwa ikipeleka mahindi hayo katika maeneo yenye upungufu wa chakula na kuyauza kwa gharama ya Sh. 63,000 badala ya ile inayouzwa na walanguzi sokoni.




Ukurasa 17

Tutawakumbuka sana Sokoine, Mrema na Rais Dk. Magufuli




**WIKI YA MWANA - KATAVI**
**...Mkoa wawekeza kwenye Royal Tour, waanza kushuhudia matokeo chanya**

Ukurasa 15

BUFE
IJUMAA NOVEMBA 11, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## JICHO LA MKUTANONI COP 27

# Hoja yaibuliwa kupinga miradi gesi inayoendelea Bara Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI wanapokutana kujadili jinsi ya kupunguza uzalishaji wa gesi chafu, vizazi vya wakazi wa kwanza wa Kusini mwa Afrika wanaibua wasiwasi kuhusu mradi wa utafiti wa mafuta na gesi.

Viongozi wa kidini pia wanauita kwamba 'ni dhambi; na kutoa wito kwa wajumbe wa COP27 kudhibiti shughuli za kampuni za mafuta.

Katika nchi za Kusini mwa Afrika, Botswana ni mojawapo ya delta kubwa zaidi za bara duniani, mandhari ambayo Umoja wa Mataifa umeitaja 'wa kipekee'" na 'nadra' kwa uzuri wake.

Okavango Delta ni chemichem inayopatikana katikati ya Jangwa la Kalahari. Eneo hilo ni makazi ya baadhi ya wanyama walio hatarini kutoweka duniani kama vile faru weusi, ndege, samaki na wanyama wanaoishi hapa wanafanya mfumo asilia wa eneo hili kuwa dhaifu.

Aidha, ni eneo lenye thamani kubwa katika urithi wa dunia, tembo wengi huhamia Delta ya Okavango kufuata maji kila mwaka

Lakini kuna hofu kwamba eneo hili linakabiliwa na tishio la kuharibiwa, kwa sababu linakadiriwa kuwa nishati ya mafuta.

Kampuni ya Reconnaissance Energy Africa (ReconAfrica), kutoka Canada inaamini kunaweza kuwa na utajiri wa mafuta na gesi chini ya ardhi kaskazini mwa Botswana na nchi jirani ya Namibia.

Kunakadiriwa kuna eneo la kilomita za mraba 34,325 linalozunguka mpaka wa nchi hizo mbili. Visima vitatu vya majaribio tayari vimeshachimbwa nchini Namibia.



Sehemu ya mitambo ya gesi iliyoko nchini Botswana. **PICHA: MTANDAO.**

Mwanyengwa Shapwanale, Mkuu wa Mawasiliano wa kampuni tanzu ya ReconAfrica ya Namibia anasema kampuni hiyo inafanya kazi na serikali ya Namibia akiainisha "sio tu tunaendana na kile kinachotarajiwa kutoka kwetu kulinda mazingira, haswa maji, lakini kuhakikisha kuwa tunakwenda hatua ya ziada."

Serikali ya Namibia ilikataa ukosoaji uliopo kwamba, ina jukumu la kuendeleza maliasili ya nchi hiyo kwa manufaa ya watu wake.

"Kupuuza jukumu hilo itakuwa ni kutojali, kwa hiyo kama nchi huru ya kidemokrasia, Namibia itachunguza na kuendeleza maliasili yake kwa uendelevu," ilisema kwamba uzalishaji wa gesi chafuzi nchini Namibia ikifafanua "haukuwa na maana ikilinganishwa na ule wa mataifa yaliyoendelea".

Afrika kwa ujumla inawajibika kwa chini ya 4% ya uzalishaji wa hewa chafu duniani.

Suala la nishati ya mafuta linaibuka kama hatua ya mgawanyiko katika COP ya mwaka huu, idadi kubwa ya wajumbe wanasema wanapaswa kuwa huru kutumia amana za mafuta na gesi, ili kukuza uchumi wao na kumaliza umaskini wa nishati. Lakini Askofu Pato bado hajashawishika.

Nchini Botswana wasiwasi huo unaungwa mkono na vizazi vya wakazi wa kwanza wa Kusini mwa Afrika: Wasan.

Kwa maelfu ya miaka jimii ya Wasan iliishi eneo ambalo sasa ni Kusini mwa Afrika, wakiishi maisha ya uwindaji.

Sasa watu wa jamii hiyo waliosalia wanadhaniwa kuwa karibu 90,000 wanaopatikana Botswana, Namibia, Afrika Kusini na Zambia.

Msingi wa mifumo ya tamaduni na imani zao ni kuishi kwa amani na asili. Msimamo wa kiroho wa Wasan inahusishwa kwa kiasi kikubwa na uhusiano wao na ardhi, mimea na wanyama.

"Hatutaki mradi huu ufanyike," anasema Diphetogo Anita Lekgowa, mwanaharakati wa Jamii ya San kutoka Botswana ambaye anahudhuria COP27 nchini Misri kama mwanaharakati wa haki za watu wa kiasili.

"Tunajali mazingira na ulinzi wa maliasili zetu, kwa sababu mara [uchimbaji visima unapoanza] kutakuwa na mabadiliko mengi.

Wanyama watahama na tunahofia kupoteza mimea yetu ya kiasili." Serikali ya Botswana ilikataa maombi kadhaa ya mahojiano, lakini Waziri wa Rasilimali Madini, Lefoko Moagi, amewahi kusema kwamba "masharti ya leseni yanahitaji ReconAfrica kuhifadhi mazingira asilia kadiri inavyowezekana na kupunguza ... uharibifu wa asili na rasilimali za kibaiolojia."

Serikali pia inasisitiza kwamba hakuna uchimbaji unaopangwa kwa sasa nchini Botswana - uchunguzi utafanywa kwa njia zisizo za uvamizi.

Lakini Anita anahofia kwamba iwapo uwepo wa mafuta au gesi utathibitishwa, hatimaye uchimbaji wa visima utaongezeka sana.

Askofu Pato ana wasiwasi kuhusu nini kinaweza kutokea. Yeye ni kutoka kwa watu wa Mto San, ambao wanaamini walipewa mto Okavango na miungu, kwa sababu haukauki kamwe.

Alipokuwa akikulia katika kijiji cha Khwai kwenye ukingo wa delta, heshima waliyokuwa nayo wazee wake kwa mto huo ilifumwa katika maisha yao, anasema.

"Wazazi wetu wangeenda kwenye mto ili kucheza, wakiungana na miungu, wakishukuru miungu. Utamaduni wetu, namna yetu ya maisha, roho yetu inaunganishwa na mto huu." Ikiwa mto huu na mandhari yake yatadhuriwa, Anita anasema, "itawaangamiza watu kihisia".

"Kwa nini serikali yetu inavutiwa na mafuta wakati kuna mambo mengine yanaweza kufanywa ambayo yanaweza kuleta mapato?"

**Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.**

UCHUMI

SIKU YA MWANA - KATAVI

# Mkuu Mkoa abainisha walivyopania mazito safarini msimu ujao wa kilimo

**Na Neema Hussein,** KATAVI

KATAVI ni miongoni mwa mikoa inayosifika kwa uzalishaji mazao ya chakula na hasa nafaka, kama vile mpunga, mahindi na maharage.

Mkoa katika kutambua wasifu huo, umeandaa 'Wiki ya Mwana-Katavi' ukilenga kuhamasisha kilimo na utalii ndani ya mkoa, inayoambatana na kuzinduliwa msimu mpya wa kilimo, kazi iliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa, Mwanamvua Mrindoko.

Ilikuwa kwenye kilele cha tukio hilo, iliyoanza kwa Mkuu wa Mkoa Mrindoko, kutembelea na kukagua mabanda yote yaliyokuwapo katika viwanja vya shule ya msingi Kashato, mjini Mpanda. Hapo ikijumuisha kuzuru kwenye mabanda ya usambazaji wa pembejeo za kilimo ikiwamo mbolea za ruzuku.

Baada ya kukagua mabanda hayo, Mkuu wa Mkoa Mrindoko, akawaambia wakala na wakulima yafuatayo:

"Niwatake kuhakikisha wanazingatia utaratibu uliowekwa na wawe waaminifu kwa asilimia mia moja wasifanye mchezo wowote, ambao utaashiria udanganyifu kwenye utoaji wa mbolea za ruzuku.

"Kama kuna yeyote atakayejaribu kufanya hujuma, kuiba au kuuza kwa bei tofauti na ile ambayo Rais ameelekeza, hatutasita kumchukulia hatua kali za kisheria.

"Niwatake wakulima wote wajiandikishe kwa maofisa wao wa kilimo au ofisi za watendaji wa kata na mitaa, ili waweze kupata namba maalumu ambazo zitawatambulisha kuwa wao ni wakulima, waweze kupata mbolea kwa utaratibu ambao mheshimiwa ameuweka."

Hapo Mrondoko anaelekeza: "Niwatake pia, wakulima kuwa waaminifu kwa asilimia mia moja kama tutakuta mfuko wa mbolea upo kwa mtu ambaye ni tofauti, wote wawili tutawachukulia hatua kali sana za kisheria."

Anasema katika msimu wa kilimo ulipo wa mwaka 2022/23, malengo ya mkoa ni kulima jumla ya hekta 339,187, zikiwamo hekta 273,436 za mazao ya chakula na hekta 65,752 za mazao ya biashara.

Mrindoko anafafanua malengo ya kimkoa ni kuvuna jumla ya tani 159,754, 975 za mazao ya chakula na tani 85,568,000 ya mazao ya biashara.

Anasema, katika uzalishaji huo, kunahitajika kuwekeza mbolea takribani tani 14,811, ambayo kazi ya kuzifikisha kwa walengwa inaelezwa inahitaji juhudi za maofisa ugani na kampuni husika za mbolea, kuhakikisha malengo hayo yanatimia.



Mkulima akiwa amenunua mahitaji yake, kwenye viwanja vya maonyesho ya Mwana-Katavi,mjini Mpanda, kwa ajili ya msimu wa kilimo ulioanza. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

> **"Kama mnakumbuka kwenye Sensa ya Mwaka 2002, tulikuwa wananchi laki tano 564 na kitu hivi...kama 240, lakini kwa Sensa ya Mwaka 2022 wananchi wa mkoa wa Katavi tuko 1,152, 958.**



Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, akizindua msimu wa kilimo, mjini Mpanda.

"Niwatake maofisa ugani wote kasimamieni kupitia pikipiki mlizopewa, kuhakikisha mnawafikia wakulima na kuhakikisha migogoro midogo midogo ndani ya wilaya zenu, inamalizika kabla ya mvua hazijaanza kunyesha.

"Niwaombe pia, wakuu wa wilaya mkasimamie kikamilifu, kama kuna mgogoro unaufahamu huko kwenye eneo lako, hakikisha unautatua mvua zikinyesha kila mwananchi anaingia shambani analima, anapanda, anapalilia anaweka mbolea na kuelekea kwenye mavuno, ili kuleta tija iliokusudiwa," anaagiza Mrindoko.

Pia anagusia dhana hiyo na uhusiano wake na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika hivi karibuni, akiutaka umma huo kuhamasisha wana - Katavi, waendelee kufanya kazi na kuongeza bidii shambani, kufanane na ongezeko lao lililoko kwenye taarifa ya sensa kimkoa.

"Kama mnakumbuka kwenye Sensa ya Mwaka 2002, tulikuwa wananchi laki tano 564 na kitu hivi...kama 240, lakini kwa Sensa ya Mwaka 2022 wananchi wa mkoa wa Katavi tuko 1,152, 958.

"Kwa maana hiyo, sisi tumeongezeka kwa asilimia saba. Hiyo si ndogo na kwa mujibu wa taarifa nilizoziona huko kwenye 'mataarifa - taarifa' nakwamba sisi mkoa wa Katavi, tunaongoza Tanzania nzima, kwa kuwa na ukuaji mkubwa zaidi kuliko mikoa mingine yote.

"Maana yake nini? Kwamba kutaja tu hii idadi ndio tumemaliza kazi, hapana! Maana yake ni kwamba, tutumie nguvu kazi hii vizuri kuweza kuzalisha mazao ya kilimo, tutumie nguvu kazi hii, kuweza kuongeza ukubwa wa mashamba bila ya kuvamia misitu na maeneo yaliotengwa kwa mujibu wa sheria," anasema Mrindoko.

**WARATIBU SHAMBANI**

Faridu Abdalla, ni Ofisa Kilimo Mkoa wa Katavi, anayesema kazi ya kuuza mbolea za ruzuku, inaendelea na tayari wameishaingiza tani 1500 za mbolea.

"Msimu wa mwaka juzi, mfuko mmoja wa mbolea ulikuwa Sh.140 000. Kwa mwaka huu kupitia ruzuku mfuko mmoja, mkulima anaununua Sh. 70,000 kwa hiyo, mkulima amerahisishiwa sana cha msingi nikufate zile taratibu zilizowekwa, aweze kunufaika.

"Wakulima zaidi ya 45,000 tayari wameshajisajili kupata mbolea za ruzuku na lengo letu ni kusajili wakulima 400,000. Kama ulivyosikia, kwenye sensa hii, tuko wengi sana tuko watu milioni moja na kitu," anasisitiza Faridu.

Exaud Mbwilu, ni wakala wa mbolea za ruzuku ambaye anasema changamoto kubwa wanayokutana nayo wao kwa nafasi yao ya uwakala, ni mkulima kutokuwa na uelewa pindi wanapomweleza cha kufanya.

"Tunawaomba maofisa ugani wawaelimishe wakulima, ili waingie kwenye kilimo cha kisasa. Unamwambia mkulima mbolea hii ni ya kupandia tu, inatakiwa uchukue tena na ya kukuzia.

"Anakwambia 'hii inatosha'. Unamwambia 'tumia mbegu hii ya kisasa' anakwambia 'hapana nina mbegu yangu niliitunza.' Pia, changamoto nyingine ni bei ya mbolea tuseme tu ukweli, bado iko juu sana!

"Hebu fikiria mfuko mmoja Sh.70, 000 hizi mkulima mdogo anaweza kununua mifuko kumi ya mbolea sawa na laki saba, itoke wapi hiyo kwa mkulima? Wanaishia mfuko mmoja au miwili," anasema Mbwilu.

Wakulima nao wanatumia nafasi hiyo kuiomba serikali kuendelea kupunguza bei ya mbolea za ruzuku hata wale wakulima wadogo, waweze kumudu kununua mifuko mingi, ili kuleta tija katika uzalishaji shambani.

UCHUMI

SIKU YA MWANA - KATAVI

# ...Mkoa wawekeza kwenye Royal Tour, waanza kushuhudia matokeo chanya

• Hifadhi ya miaka 48, kinachofanyika & kitakachofanyika

**Na Neema Hussein,** KATAVI



Hali halisi ya vivutio vya wanyama, katika Hifadhi ya Taifa Katavi. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

NI wiki ya 'Mwana - Katavi' na kilele chake cha hivi karibuni. Ni mkoa ambao una vivutio vingi vya utalii, wakiwemo wanyama wa aina mbalimbali na wanaovutia watalii wengi.

Katika kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza vivutio vilivyo ndani ya nchi kupitia filamu ya 'The Royal Tour', mkoa wa Katavi ukaamua kuandaa wiki ya Mwana- Katavi, kwenye kilimo na Utalii.

Ni wiki iliyokuwa na lengo la kutangazwa vivutio vya utalii ndani ya mkoa na kuhamasisha wananchi kufanya kazi halali, katika mustakabali wa kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, akajibebesha jukumu la kuongoza makundi mbalimbali ya wananchi, kwenda kutembelea vivutio vilivyo ndani ya mkoa, ikiwemo Banda la Ndege aina ya Mbuni.

Baada ya kutoka hapo, msafara wa Mkuu wa Mkoa, ulielekea moja kwa moja katika Hifadhi ya Taifa Katavi (KANAPA) kujionea Wanyama wa aina mbalimbali kama vile viboko na twiga.

Baada ya kufika na kushuhudia hayo, ndipo Mkuu wa Mkoa akarejea hadhira kuwapa maneno:" Niendelee kumshukuru Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya mkoa wetu na nchi yetu kwa ujumla, kwa kufanya ile filamu ya 'The Royal Tour' ambayo imeongeza idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vyetu.

"Niendelee kuwahamasisha wananchi kuwa, kila mmoja ndani ya nchi na ndani ya Katavi, ni mtalii. Kwa hiyo kila mtu ahakikishe hakosi kufanya matembezi ndani ya 'Katavi National Park' (Hifadhi ya Taifa ya Katavi) kwa kujenga uchumi, pia kujiendeleza mwenyewe,"anasema.

Vivutio hivyo ni vipi? Hapo Mrindoko ana ufafanuzi: "Kujifunza na kufurahia mandhari na vivutio mbalimbali vilivyopo, uoto wa asili, wanyama wa aina mbalimbali, ndege wa aina mbalimbali, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumemheshimisha Rais wetu.

"Upekee wa 'Katavi National Park ni kama tunavyoona hapa nyuma (anaelekeza waliko wanyama) kuna kundi kubwa la viboko wakiwa wanaishi sehemu moja. Huku nyuma yangu sio kwamba hivyo ni vichuguu au ni mawe, hao ni viboko! Sasa tumekuja kuona wakiwa pamoja wanakaa namna gani.

"Na hapa tumeambiwa ni sehemu ambayo wanajihami kwa jua, kwa sababu ya 'nature' (asili) ya ngozi zao hawawezi kukaa kwenye jua kali, lazima wakae sehemu ambayo inaunyevunyevu. Niendelee kuwakaribisha watalii wa ndani ya mkoa na nje ya mkoa kuja kujionea tunu zilizopo.

"Nitumie nafasi hii kuiomba Wizara ya Maliasili na Utalii, iendelee kuboresha mazingira hasa miondombinu ya kupokea wageni tunaamini kabisa kwa tukio hili idadi ya wageni itaongezeka, kwa sababu majengo yale ni madogo madogo, yanaweza yasitosheleze sana kuwapokea watu wote watakao kwenda.

"Katavi National Park, kwa sasa imefunguka, imetangazwa. Suala lingine niwaombe, wananchi kuendelea kuwekeza walio ndani ya mkoa na nje ya mkoa, fursa kwenye utalii tunazo nyingi.

"Bado tunahitaji 'ma-hoteli' bado tunahitaji usafirishaji, bado tunahitaji watu maeneo ya kupokea wageni, kulala na chakula, maeneo ya kupumzika na vingine mbalimbali," anasema Mrindoko.

**WASIMAMIZI WAKUU**

Kaimu Kamishna Mhifadhi Katavi Manendo Maziku, anawataka wananchi wabadilike, kwamba mtalii ni lazima awe mgeni, bali hata yeye ana nafasi hiyo.

"Mkuu wa Mkoa, nachukua nafasi hii kuwakaribisha wewe na wote ulioambatana nao kuja kuenzi kazi nzuri ya Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kupitia filamu ya 'The Royal Tour'.

"Tayari matokeo ya filamu hiyo yameanza kuonekana, hata hapa Katavi tunapokea makundi makubwa ya wageni. Tuna imani, haya ni matokeo ya Mama ambayo ameyaanzisha na sisi tunayaendeleza.

"Hifadhi hii ni kongwe. Imeanza tangu mwaka 1974 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 2,253 wakati ule, lakini hifadhi iliweza kuongezewa ukubwa na kufikia kilomita za mraba 4,471.

"Tuna changamoto ambazo mojawapo, ni upungufu wa maji katika bwawa la viboko. Kama mmepita hapo kwenye daraja la viboko, mmeona na inaweza kuleta madhara, baadaye japo hatujaanza kupata madhara.

"Hifadhi ni nzuri na salama. Kutembelewa kuna viboko, mamba walioishi kwenye mapango. Makundi makubwa ya ndege, kuna ndege wahamao na ndege wazawa aina 250 na wanyama wakubwa na wadogo,"anasema Maziku.

Msafara huo kabla ya kufika hifadhini, ulisimama katika kijiji cha Stalike na kuzungumza na wananchi waliokuwa wamekusanyika katika eneo la barabara hiyo kuelekea katika hifadhi na hapa Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa Katavi , Nehemia James anatoa ufafanuzi:

"Siku ya leo mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ni siku ambayo umeichagua kutangaza vivutio vilivyo ndani ya mkoa. Lakini, ukasema penyewe ni lango kuu la utalii kuingia katika Hifadhi ya Taifa Katavi, ambako inatakiwa tuwaambie wananchi wawe tayari kuwapokea watalii. Lakini, wananchi hawa wana uwezo pia wa kwenda kutalii katika hifadhi yetu ya Katavi."

Wiki ya mwana - Katavi yenye kaulimbiu isemayo 'Katavi Yetu'. Pale ilitamkwa neno hilo kama kibwagizo, wananchi wakaitikia 'kazi, amani na mazingira kwa maendeleo yetu, kazi iendelee', hapo ikiwa na maana

kazi zilizo halali na rasmi kwa ajili ya uchumi na amani.

Hapo Nehemia akafafanua kwamba, panapokuwapo amani, pana utulivu na usalama wa wananchi, hivyo ni rahisi kufanya kazi na kujenga uchumi katika staili ya kuhamasisha wananchi watunze mazingira na kazi iendelee, kuenzi kazi kubwa ya Rais Samia kutangaza utalii

"The Royal Tour mama ameanza Katavi tunaendeleza," anahitimisha Nehemia, kwa salamu za majumuisho.



"

**Tayari matokeo ya filamu hiyo yameanza kuonekana, hata hapa Katavi tunapokea makundi makubwa ya wageni. Tuna imani, haya ni matokeo ya Mama ambayo ameyaanzisha na sisi tunayaendeleza.**

IJUMAA NOVEMBA 11, 2022 BUFE 17

UCHUMI

MTAALAMU DK. BULAMILE:

# Bodi ya Ujenzi tunapata tabu kuona majengo yanayokinzana na mipango ya maendeleo

- Alalamikia Dar... Sinza, Mwananyamala imepitwa na wakati
- Amdokeza Naibu Waziri shida barabarani, Sheria ya Ununuzi

**Na Romana Mallya**

"UTEKELEZAJI wa miradi katika viwango duni, ikiwamo ya serikali, unatokana na kutokushirikishwa wataalamu wa fani husika wakiwamo wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi,"

Ni Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Dk. Ludigija Bulamile, anavyobainisha katika mazungumzo yake.

Kutokana na changamoto hiyo, Dk. Bulamile anaishauri serikali kwamba kila mradi wa ujenzi uwe wa barabara, majengo, usambazaji maji, upanuzi wa bandari, unatakiwa ushirikishe wataalamu wa aina zote wa ndani, ili iweze kuishi muda mrefu.

Ukiwa ni mkutano wa tatu wa AQRB wa mwaka uliofanyika kwa siku mbili kuanzia Oktoba 19 mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Katika mkutano huo, mambo makubwa yaliyojitokeza ni namna ambavyo ushiriki wa wataalam wa fani zote katika miradi na kusababisha baadhi yake kutekelezwa kwa kiwango duni.

Dk. Bulamile, kwanza anabainisha lengo la mkutano huo ni kuwanoa wataalam, waendane na mabadiliko ya teknolojia ya ujenzi na mada kuu ikiwa ni 'Uhifadhi wa Majengo kwenye Miji ya Afrika kwa sasa'.

Anasema ni mada inayokumbusha umuhimu wa uhifadhi wa urithi wa majengo na maeneo ya kihistoria katika kazi zao za kila siku na kwamba, ubora wa majengo unahitajika, ili yaweze kuwa himilivu na endelevu.

"Tukumbuke majengo tunayojenga kwa sasa kwa vizazi vijavyo yatakuwa ya kale, tunapojenga lazima tukumbuke kufuata au kutumia wataalam wanaostahili ili yaishi.

"Kwa sasa tunajenga majengo mengi sana. Ukiangalia ubora wake haufikii ubora unaotegemea jengo kuishi muda mrefu. Kimsingi, mipango miji una kipindi cha mpito kilichogawanyika sehemu tatu, majengo yanayoishi miaka 33, 66 na 99."

Mtaalamu huyo anabainisha kuwa, wanapojenga jengo la miaka 30, linatakiwa kutumia gharama ndogo linaloweza kuishi muda huo, ili baada ya hapo serikali iweze kubadili matumizi ya ardhi na kutaka majengo mengine yenye umri zaidi.

"Kwa sasa miji inazidi kupanuka kwa kuwa hatufuati sheria ya muda maalum ya utoaji maeneo, unakuta maeneo kama Mwananyamala au Sinza, kipindi cha mpito kilikuwa miaka 33 na ilishaisha, hivyo kwa sasa ni wakati wa kuibadilisha Sinza, ili eneo liwe na majengo makubwa zaidi yanayochukua watu wengi, badala ya kuupanua mji kwenda nje.

"Matokeo yake, gharama za usafiri kuja kufanya kazi mjini inakuwa kubwa zaidi na ukarabati wa mji ukipanuka unakuwa mgumu zaidi, jengo la serikali lazima liishi zaidi ya miaka 66 au miaka 99."

Kuhusu jijini Dar es Salaam, anaigeukia barabara ya njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha, akitoa mfano kwamba lengo lilikuwa ni kuhakikisha magari yaende mwendo kasi kutokana na foleni.

Dk. Bulamile anaiambia serikali kwamba, kwa kuwa mradi huo haukushirikisha wataalam wote wanaotakiwa, kinachoshuhudiwa ni kwamba, kila baada ya umbali wa mita 500 au kilometa moja, kumewekwa eneo la wavukao kwa miguu.

"Ukitaka kwenda Hospitali ya Mlongazila, ilikuwa ni eneo ambalo ulikuwa unalitumia kwa urahisi kwenda, lakini kwa sababu ya kutoshirikisha wataalamu, mnakwenda kujenga daraja kwenye mlima, mnatumia gharama kubwa zaidi unaacha bonde ambalo mngelitumia kupita chini, watu wakaenda Mlongazila," anasema.

**JICHO LA NDANI**

Anautoa mfano mwingine, serikali kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma, imeruhusu taasisi za umma kutekeleza miradi ya ujenzi kwa kutumia wataalam wake wa ndani, lengo ni kupunguza gharama za kuendeleza miradi.

Anasema kutokana na changamoto za miradi zilizotolewa kwa utaratibu huo, ipo iliyotelekezwa bila ya kutumia wataalam wote wa ndani.

"Unakuta mkuu wa taasisi kama daktari anajenga hospitali, anaambiwa 'tunakupa fedha kiasi hiki jenga', matokeo yake mnampa adhabu wakati haimstahili, ushauri wetu wa bodi, taasisi zinazotekeleza miradi kwa mfumo wa manunuzi wawe na wataalam wote wanaotakiwa katika majenzi," anasisitiza.

Hata hivyo, anasema kuwapo miradi mikubwa nchini ni kiashiria cha maendeleo kwenye sekta ya ujenzi na uchukuzi.

"Ni kiashiria kwamba sekta ya ujenzi na uchukuzi inaendelea kufanya vizuri katika nchi yetu, matarajio yetu ni kwamba miradi mikubwa ya ujenzi na uchukuzi itaendelea kuongezeka na wadau wa sekta hii waangalie namna bora ya kunufaika kutokana na hatua hizi zilizofikiwa na zinazotarajiwa kuendelea," anasema.

Anasema, wanafahamu serikali kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma (PPRA), imeruhusu taasisi za umma kutekeleza miradi ya ujenzi kwa kutumia wataalamu wake wa ndani kwa lengo la kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi.

Dk. Bulamile, anasema kutokana na taarifa za changamoto za miradi inayotekelezwa kwa utaratibu uitwao ' Force Account', Bodi hiyo ya ujenzi, inashauri pale panapotekelezwa, basi watumiwe wataalamu wote wanaotakiwa katika ujenzi wa mradi.

Anataja changamoto nyingine, ni kutokuwapo sheria rasmi ya majengo, ilikwishawasilishwa kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tangu mwaka 2013, taratibu na kanuni za ujenzi pia kukosekana viwango na vipimo, kunasababisha taifa kukosa manufaa mengi kwenye tasnia ya majengo.

**NAIBU WAZIRI**

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Atupele Mwakibete, anayemuwakilisha Waziri, Prof. Makame Mbarawa, anasema serikali imeyapokea yaliyoelezwa mkutanoni, akikiri eneo moja kwamba kuna Mazingira Sheria ya Manunuzi ya Umma, imekuwa ikitumika kama kichaka.

"Nimefurahi kusikia bodi inafanya marekebisho ya sheria yake, ili wataalamu wake hasa wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi, washiriki kikamilifu kwenye miradi ya majengo katika hamashauri na majiji kwa kutumia nguvu za wananchi," anasema.

Mwakibete anasema, wizara imeunda timu ambayo inakagua kuhakikisha hakutakuwapo mradi utakaotekelezwa bila ya kushirikisha wataalamu wote wa ndani, kuanzia sasa.

Anasema, ameshiriki katika mradi wa kupunguza ajali za barabarani, ambazo zimekuwa nyingi kutokana na barabara husika wakati wa kuzibuni, hazikushirikisha wataalamu mbalimbali.

"Ajali zinatokea ndani ya nchi ni zaidi ya watu 16,000 kila mwaka wanapoteza uhai wao, kwa sababu hatukuhusisha wengine waenda kwa miguu, baiskeli, wenye ulemavu.

"Hii programu tuliyoizindua hivi karibuni, ni mtambo ambao unatembea barabara zote kuu nchini, tukianzia za Dar es Salaam. Kila baada ya mita moja utaainisha mapungufu ya barabara hiyo, ili tuzipangilie upya," anasema

Naibu Waziri Mwakibete, anasema suala la kutungwa sheria ya majengo, nambari za ujenzi na viwango na vipimo yote yanashughulikiwa na wizara hiyo, kupitia Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC).

"Ninamwelekeza Naibu Katibu Mkuu kwa niaba ya Katibu Mkuu Ujenzi, lisimamie hili haraka iwezekanavyo," anasema.

**MSAJILI WA BODI**

Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Edwin Nnunduma, anasema pia kuna masuala muhimu katika sekta hiyo ambayo wanafanyia mapitio.

Nnunduma anayataja kuwa ni; urithi wa usanifu majengo upangaji wa kisasa wa miji, kuhifadhi urithi wa majengo yaliyojengwa mfano ni Mji Mkongwe Zanzibar na Soko Kuu la Kariakoo na athari za majengo mapya katika maeneo ya kihistoria.

Nyinginezo anataja ni penye athari kiuchumi na kijamii kwenye uhifadhi wa majengo ya kihistoria, katika maeneo ya mijini na hali ya sasa, pia fursa za kuboresha uhifadhi wa maeneo ya urithi wa utamaduni, katika mtazamo wa Tanzania na wakaguzi wa nje.



Eneo la Sinza, Dar es Salaam, likionekana kutoka angani.




Moja ya mitaa maarufu ya eneo kongwe la Mama Zakaria, Mwananyamala, Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **"Ninamwelekeza Naibu Katibu Mkuu kwa niaba ya Katibu Mkuu Ujenzi, lisimamie hili haraka iwezekanavyo," anasema.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tutawakumbuka sana Sokoine, Mrema na Rais Dk. Magufuli






**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008
kulangwasos@gmail.com

TANZANIA ni nchi ya amani. Wengi tunasema hivyo na hata kuamini. Nami naamini hivyo na kwa kuwa naamani si kwamba hatuwezi kuhitilafiana la hasha, kuhitilafiana kupo tu.

Ndiyo sababu huambiwa kuwa vikombe kabatini licha ya kwamba hukaa na kulala pamoja, lakini haviachi kugongana. Ndivyo nasi Watanzania tulivyo pamoja, lakini hatuishi kukosana na kukosoana.

Kuwa na amani si kuwa mazezeta, kwamba mnakubali kila lolote litolewalo na yeyote hata kama ni maamuma. Hata kama ni mwenye shida ya afya ya akili, hapana. Amani ni kuzungumza mkaelewana na kushirikiana kwa mambo yenu yanayokuleteeni ustawi na faraja.

Kama tunakubaliana, basi kumbukeni, kwamba Taifa hili ni letu sote na tuna jukumu la kulijenga, chini ya viongozi wetu tunaochagua wenyewe na wakati mwingine kusingiziana kwamba tumeletewa na Mungu.

Mungu yupo kutuangalia tu tunavyofanya, tukikosea kupata viongozi, basi imekula kwetu, hivyo tunapaswa kuwa makini katika kupata viongozi makini, tunaojua kuwa wako tayari kutuongoza, ili kufikia tunachokitaka au kutarajia.

Tanzania tumepitia miongo mingi ya utawala, tumekuwa na viongozi wakapita na kuja wengine na sasa tunao wengine, na tunafanya hivyo kila muda ukifika kulingana na takwa la katiba yetu wenyewe.

Katika historia ya maisha yetu, tumekuwa na viongozi mbalimbali wafananao na watofautianao, lakini ni Watanzania walewale, wenye maono na mwelekeo ule ule na huja wakiondoka tukawa na wengine.

Tunakumbuka miaka ya themanini, tulipata kuwa na kiongozi anaitwa Edward Sokoine, miaka ya tisini akaja mwingine anaitwa Augustine Mrema na miaka ya elfu mbili tukawa na mwingine anaitwa John Magufuli.

Mtashangaa kwa nini hawa! Ni kwa sababu naona kama ni watu walikuwa wakifanana kwa baadhi ya mambo na kutofautiana pia, ndiyo sababu nikawataja hawa na nitawafafanua, kwa muktadha wa tabia na misimamo yao.

Sokoine alikuwa Waziri Mkuu katika serikali Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Julius Nyerere. Alikuwa mtu mwenye msimamo na hakika. Mwalimu alimpenda sana.

Hakika alikuwa mwenye msimamo na alipambana sana na wabadhirifu wa mali za umma. Hakuwa na maskhara hata kidogo na alifikia hatua ya kufanya ziara za kushitukiza ofisini na alipokuta kiongozi hayupo sehemu yake ya kazi, alikiona cha moto, ikiwa ni pamoja na kuondoka na kiti chake.

Huyu ni kiongozi ambaye kifo chake kilimliza Mwalimu hadharani, kuonyesha jinsi alivyokuwa akimwamini katika kusimamia serikali na masuala mengine ya wananchi.

Katika kipindi chake, wahujumu uchumi walionja joto ya jiwe, mpaka wengine kutupa mali zao kwa hofu. Alifariki dunia mwaka 1984 kwa ajali ya barabarani.

Mrema ni kiongozi mwingine aliyekuwa mchapakazi akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini pia Naibu Waziri Mkuu katika serikali ya Awamu ya Pili ya Alhaji Ali Hassan Mwinyi. Licha ya kupenda maskhara, lakini alichapa kazi kupindukia, akikabiliana na waonevu.

Mrema alikimbiza, akipambana na uhalifu hata akidiriki kutoa siku saba kwa waovu kujirekebisha, akifuatilia mpaka kuwataka baadhi ya viongozi kumfuata kijijini kwake Kiraracha kujieleza.

Katika kuimarisha usalama, alianzisha vikundi vya ulinzi wa sungusungu, sambamba na ujenzi wa vituo vidogo vya Polisi. Wanawake walioonewa na waume zao hawatamsahau. Alifariki dunia mwaka huu.

Magufuli alikuwa Rais wa Awamu ya Tano, alipenda maskhara wakati mwingine yakipindukia, lakini alikuwa mfuatiliaji, akitaka kujua kila kinachofanyika nchini. Hakuogopa kitu wala mtu. Watu hawakulala wakihofia kutumbuliwa, kwa sababu hakutaka kuchelewesha mambo ya maendeleo kwa wananchi. Naye alifuatilia kwa ziara za kushitukiza.

Akiwa Waziri kabla ya urais, aliaminiwa sana na Rais wa Awamu ya Tatu, marehemu Benjamin Mkapa. Yeye alifariki dunia mwaka jana, akarithiwa na Rais wa sasa, Samia Suluhu Hassan.

Viongozi hawa watatu bila ya kuonyesha udhaifu wao, ni watu wanaoacha historia ya kuchangamsha nchi kiutendaji na kufanya wenye dhamana za umma wasilale, wachape kazi.

Ni kwa sababu Watanzania ukiwaacha bila ya kuwafuatilia na kuchukua hatua, hakika utavuna mabua. Ajali ya karibuni ya ndege ya Precision Air, imezua mjadala mkubwa wa umma kuhusu uwajibikaji wa wahusika, pale ufanisi kwa namna moja ukitajwa umetoka kwa wavuvi. Poleni ndugu zetu mliopoteza ndugu Bukoba. Poleni mliojeruhiwa Bukoba. Alamsiki!

BIASHARA

# Kutana na maduka ya ughaibuni yanayounganisha watu na kwao

- Mhindi ang'ara nalo Uingereza
- Wa diaspora na tovuti ughaibuni

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA duka la familia la vyakula liitwalo 'Popat Mithai & Farsan' linalomilikiwa na Vijaya Popat na wafanyakazi wake wote ni wanawake.

Mara nyingi huwa na shughuli nyingi sana kushughulikia wateja wa lugha nyingi, kiasi cha kukosa muda wa kukaa chini.

Popat, mwenye asili ya Kihindi, alianzisha biashara hiyo, huko Leicester mwaka 2011 ili kuuza bidhaa kama pipi na vyakula vya kihindi, ikianza na wafanyakazi wawili hadi wafanyakazi 15 wa sasa. Huduma kupitia mtandao ilizinduliwa mnamo 2018.

Ikihudumia watu wa Asia Kusini katika jiji la Midlands Mashariki na maeneo ya mbali zaidi, mauzo yaliongezeka wakati wa janga la corona.

Wateja walitafuta vyakula vya faraja zaidi - ladha ambazo wao au mababu zao walileta Uingereza kutoka nchini mwao zikiwemo India, Pakistan, Bangladesh na Sri Lanka.

Mtoto wa Popat, Shyam, ana ufafanuzi:"Mama yangu anajulikana sana katika jamii kama mtu anayeendesha biashara." Anaendelea:" Wote wanataka kuongea naye haswa ili kuona kama anaweza kutoa vitu fulani."

Biashara ya Popat Mithai & Farsan ya mtandaoni imesaidia kuhudumia wateja wake katika maeneo mbalimbali ya Uingereza.

Anaongeza kuwa wahamiaji wakongwe na wale ambao wa baadaye nchini Uingereza, wanaounda msingi wa wateja wake, akieleza:"Mauzo ya mtandaoni sasa yanachukua takriban robo moja hadi theluthi moja ya mauzo yote ya biashara."

Dukani pia wananunua bidhaa kutoka Kenya, nchi hiyo ikiwa mwezi Septemba kuwa, ikiahidi itaunda wizara mpya kwa ajili ya Wakenya wanaoishi nje ya nchi.

Rais wa Marekani, Joe Biden, naye ametangaza kwamba atauambia Mkutano wa Viongozi wa Marekani na Afrika utakaofanyika mwezi ujao mjini Washington, kwamba anataka "kukuza uhusiano wa wageni wanaoishi nchini humo".



Duka la familia la vyakula la Popat Mithai & Farsan, linalomilikiwa na Vijaya Popat, nchini Uingereza, wafanyakazi wake wote wanawake na wanahudumia wateja kwa lugha nyingi. Picha nyingine, baadhi ya bidhaa zinazopatikana dukani humo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



**WAHAMIAJI NA BIASHARA**

Jambo la hakika, ni kwamba msukumo wa ujasiriamali kwa wageni wakiwemo wahamiaji umekuwa ukitambuliwa kwa muda mrefu.

Ripoti ya mwaka 2010 ya Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo, inasema kuwa wajasiriamali wahamiaji wamekuwa na elimu bora kuliko wenzao asilia na kuna uwezekano mkubwa wa kuunda biashara mpya.

Mara nyingi makampuni au biashara nyingi za wageni zinahusika katika uingizaji vyakula, nguo au bidhaa nyingine kutoka nchi zao za asili, kama anavyofanya Vijaya Popat mzaliwa wa India na duka lake linalostawi huko Leicester.

Duka hilo na mengine kama hayo, yalichangia mauzo ya nje ya India kwenda Uingereza jumla ya dola za Marekani bilioni 10.4 mwaka jana.

Akiwa jijini Paris, Ufaransa, Olivier Habiyambere, anayesaidia kukuza mauzo ya Kenya hadi Ulaya, ndiye mwanzilishi wa tovuti ya Kenyan Diaspora Market, ambayo huagiza chakula na nguo kwa wingi kutoka nchi hiyo ya Kiafrika, na kisha kuziuza kwa wateja katika bara la Ulaya.

Habiyambere, aliyelelewa nchini Kenya, alipata wazo la biashara alipohamia Paris kusoma na kukutana na watu wengine kutoka Kenya na Afrika Mashariki.

"Kila mtu alitaka bidhaa za Kenya, lakini suala lilikuwa kuleta bidhaa hizo kutoka Kenya hadi hapa," anasema na kuendelea: "Watu wangeweza kuchukua bidhaa walipoenda Kenya, lakini wasingeweza kufanya hivyo kila mwaka."

Kwa hiyo, anazindua biashara hiyo mnamo Aprili mwaka huu, ili kuwapa Wakenya wanaoishi barani Ulaya urahisi wa kununua bidhaa kutoka nyumbani.

Habiyambere anaongeza kuwa, biashara hiyo inakuwa polepole, ikisaidiwa na jamii za Wakenya kueneza habari kupitia vikundi vya WhatsApp.

Soko la Wakenya waliopo ughaibuni, huuza Ulaya mamia ya bidhaa kutoka Kenya na nchi zingine za Afrika Mashariki.

Pia, kuna tovuti yenye makao yake Glasgow, Uingereza sasa ina wateja wengi wasio na asili waliko.

Ilianzishwa muongo mmoja uliopita na mume na mke Christina Lyropoulou na Michael Sofianos, ambao walienda kusoma nchini Uingereza.

Sasa wameajiri watu 14 na kusambaza vyakula na vinywaji vya Kigiriki vinavyoagizwa kutoka nje kwenda kwenye migahawa, watu binafsi, na biashara nyinginezo.



"Tulianza kuipanua biashara kwa watu wa Uingereza - wale wanaosafiri kwenda Ugiriki au walikuwa na marafiki wa Ugiriki," anasema na anendelea: "Duka letu la mtandaoni lilishuhudia ongezeko la mauzo ya karibu asilimia 1000 katika miezi ya kwanza ya zuio la kutotoka nje kwa sababu ya corona."

**MAONI YA WASOMI**

Prof Pragya Agarwal, mwanasayansi katika Chuo Kikuu cha Loughborough, mara kwa mara hununua bidhaa zinazotoka India alikozaliwa kwa ajili yake na familia yake nchini Uingereza.

"Kwangu mimi binafsi, ni juu ya kudumisha uhusiano na nchi ya mama, nchi ya baba - vyovyote unavyoweza kuita," anasema.

Anagusia mapenzi yake ya embe za Kihindi na anakiri kila mara alikuwa akiagiza kutoka kwenye duka la mtandaoni, haswa wakati wa janga Uviko 19.

"Hicho ndicho nilichokuwa nakula wakati nakua nchini India kila msimu wa joto - na kila siku baada ya mlo," anasema.

Pia, Maria Elo, Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Kusini mwa Denmark, ambaye ana idadi ya vitabu na makala kuhusu watu wanaoishi ng'ambo na biashara.

Anasema, ni muhimu kufahamu muundo unaotokea wakati wowote jamii hiyo inapojadiliwa, huku wahamiaji mara nyingi wakielezewa katika mojawapo ya njia mbili.

Simulizi moja ni kwamba, uhamiaji na ughaibuni ni tatizo. Prof Elo anaelezea hilo kama "mtazamo wenye mapungufu" na wenye maana hasi. Lakini anaongeza pia kuna simulizi chanya ambayo inahusisha biashara na uchumi.

Anaongeza kuwa utafiti unaonyesha kuwa wafanyabiashara wanaoishi nje ni muhimu kwa biashara zinazovuka mipaka.

"Sote tunakula pizza leo, ingawa sisi sio wote waitaliano na hilo ni jambo ambalo limeanza muda mrefu uliopita."

**Kwa mujibu wa BBC.**

BIASHARA

# ‘Hohehahe’ Chalinze, Bagamoyo wasimulia TASAF inavyowageuza magwiji uzalishaji

**Na Thobias Mwanakatwe**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umekuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi walengwa wa kaya masikini katika Halmashauri za Wilaya ya Chalinze na Bagamoyo mkoani Pwani.

TASAF iliyoanza kutekeleza shughuli zake mwaka 2014 katika halmashauri hizo, hadi sasa kuna zaidi ya walengwa 3,837 wamenufaika kupewa ruzuku ya uzalishaji.

Wakizungumza na jopo la wanahabari waliotembelea miradi inayotekelezwa na wanufaika wa TASAF, wamesaidiwa kuinuka kiuchumi, kwani tangu wawezeshwe fedha wameanzisha miradi inayowaingizia pesa na kujenga nyumba bora za kuishi.

Wanataja miradi waliyoanzisha kutokana na ruzuku ya TASAF ni pamoja na ufugaji wa kuku, mbuzi, ng’ombe na kilimo cha mboga, pia magenge ya kuuza mboga.

Mnufaika, Prisca Felix (62), mfugaji kuku katika Kijiji cha Msoga, anajinasibu kwamba mtu akitaka kumpata kirahisi ni lazima aseme “anamtafuta mjasiriamali wa kuku na si kumuita jina lake.”

Anasema jina hilo maarufu, amelipata baada ya kuwezeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) waliompa Sh.500,000 kwa ajili ya ufugaji kuku, pale alipokidhi vigezo na akapatiwa mafunzo.

“TASAF wao waliniongezea nguvu baada ya kunipa fedha hizo, kwani ufugaji nilikuwa nikiufanya tangu zamani,” anasema Prisca.

Prisca anasema ufugaji kuku, umebadilisha maisha, kwani sasa anamudu mahitaji mbalimbali ya kifamilia, kama kusomesha watoto na chakula, akiwa na matarajio ya kuwa mfugaji mkubwa kijijini Msoga na maeneo mengine ya Chalinze, anakotafuta masoko makubwa ya kuku wake.

Mbali na Prisca Felix, wengine waliotembelewa na miradi yao kukaguliwa ni Mwajuma Rajabu, Veronica Kumpite na Maria Msigala, waliojikita katika ufugaji mbuzi, katika kijiji cha Mindutulieni.

Wanufaika wengine waliotembelewa ni kikundi cha Painfor Succes, kinachoendesha miradi ya kilimo, ufugaji bata na sasa wanafyatua matofali, kwa ajili ya kujenga banda la kufuga kuku.

**OFISA TASAF**

Ofisa Ufuatiliaji wa Miradi TASAF, Janeth Mtelelah, anasema walengwa 2517 wa TASAF katika Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze wamekidhi vigezo vya kupata ruzuku ya uzalishaji, ambayo mpango uliopo sasa ni kuwatoa kwenye mpango TASAF, wajitegemee.



Mnufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Zulfa Emmanuel (20), mkazi wa kijiji cha Magomeni Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo akiuza samaki ambapo mtaji wa kufanyia biashara hiyo aliwezeshwa na TASAF.

Anasema, awali 6011 ambao walikidhi vigezo vya kusoma na kupata shughuli zao, ikiwamo kilimo. Waliomba fedha kuanzia Sh.100,000 hadi 500,000.

“Fedha hizi tuliwapa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza tunawapa asilimia 50 kwa wafanyabiashara, asilimia 70 kwa wale wa mifugo na asilimia 60 kwa wale wa kilimo,” anasema na kuendelea:

“Jambo la kushukuru kwa awamu ya kwanza, walengwa 1960 miradi yao imefanya vizuri kutokana na timu yao ya ufuatiliaji kuwatembelea mara kwa mara.”

Anasema utaratibu uliotumika kutoa ruzuku ni kila mnufaika aliandika andiko lake la mradi na kisha kuomba fedha, akapatiwa kulingana na vigezo vilivyopo.

Mtelelah anasema, kuna uwezeshaji mkubwa unaofanywa na serikali, kwa kuwajali wananchi wa chini, kwani kabla ya kuwawezesha, baadhi yao walishindwa kumudu hata milo mitatu wanayoipata hivi sasa.

Mratibu wa TASAF katika halmashauri hiyo, Michael Mwakanjuki, anasema kazi kubwa wanayoifanya ni kwa walengwa kupata fedha hizo kuhakikisha wanashirikiana na wataalamu, ili miradi yao iende vizuri na kuinua uchumi wa kaya zao.

Anasema wataalam au wawezeshaji waliopewa mafunzo wamekuwa wakipita kwenye maeneo yao kutoa ushauri ili kukuza miradi yao.

Mwezeshaji wa Shughuli za TASAF katika halmashauri hiyo, Flora Balakana, anasema wamekuwa wakishirikiana na maofisa ugani katika vijiji 84, kuhakikisha walengwa wanafikiwa na kupewa huduma stahiki ili waweze kutekeleza miradi yao.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Shauri Selenda, anasema kwa mwaka wa fedha 2022/ 2023 imepokea zaidi ya Sh.bilioni 1 76 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Anasema katika fedha hizo Sh. Bilioni 1.76 walizipokea kwa ajili ya ruzuku ya uzalishaji na Sh milioni 512 walipokea kwa ajili ya ruzuku za kawaida na kuwa ruzuku za uzalishaji zinakwenda kusaidia kwenye shughuli za kilimo, ufugaji na biashara ndogondogo.

Anasema kuwa fedha za ruzuku ya kawaida zinakwenda kusaidia kwenye maeneo mengine kama ya uvuvi na ufugaji lakini hizo milioni 620 ni kwa ajili ya ruzuku za uzalishaji zinakwenda kuwanufaisha walengwa 1320 ambapo kati yao waliopata ruzuku za uzalishaji ni walengwa 1158 sawa na asilimia 88.



Mnufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Prisca Felix (65), mkazi wa kijiji cha Msoga ,kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze. ambaye ni mfugaji kuku akiwatoa nje kuku wake.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Bagamoyo, Rose Mndeme anasema wilaya hiyo ina jumla ya kata 11 na kuwa vijiji 26 vipo kwenye mradi wa TASAF vyenye walengwa 3056 ambao wanalipwa ruzuku za aina tatu, ruzuku ya kawaida, kufanya kazi kwa miradi (ajira ya muda mfupi) na ruzuku ya uzalishaji.

Anaongeza kuwa, katika ruzuku ya uzalishaji walengwa 1320 wamepewa ruzuku ya Sh.milioni 620 kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi ya ufugaji wa mbuzi , kuku, ngombe, kilimo cha mbogamboga, ukaangaji wa samaki na kuziuza, biashara ndogondogo kama za kuuza madera, usukaji wa mikeka na nyinginezo.

Ili kusimamia walengwa hao waweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa kuna timu ya wawezeshaji 26 kutoka katika kata hizo 11 kutoka katika idara za mifugo, maendeleo ya jamii,kilimo na afya ambao wanawatembelea walengwa hao 1320 ili kujua maendeleo yao na changamoto ambazo wanazitafutia ufumbuzi.

“Kufuatia timu hiyo ambayo inakwenda kutoa ushauri wa kitaalamu katika wilaya yetu miradi yote inayofanywa na walengwa inakwenda vizuri tunashukuru Mungu hivyo tunategemea kuwatoa kwenye mpango ili waweze kuwapisha watu wengine kwa kuwa sasa wameweza kusimama wenyewe,” anasema Mndeme.

Ofisa Ufuatiliaji wa Miradi TASAF, Janeth Mtelelah, anasema fedha zote zinazotolewa kwa walengwa hutumwa kwa mitandao ya simu na benki, wahusika walisaidiwa kufungua akaunti zao na kupata fedha pasipokuwa na changamoto zozote.

Baadhi ya walengwa waliotembelewa na miradi yao kukaguliwa ni Hidaya Mnyamisi mkazi wa Magomeni Bagamoyo ambaye ni mfugaji wa kuku, Zulfa Emmanuel, muuza samaki wa kukaanga.

Pia, Sikuzani Bwana, anayefanya biashara ndogondogo ya genge, Halima Juma, ambaye ni mkulima na anauza samaki, Hawa Diwani ambaye anasaidiwa na mume wake Abdallah Lukange ambao wanafanya kilimo cha mbogamboga na mpunga.

Wengine ni Mwanaheri Dalu ambaye ni mshonaji wa nguo na Elizabeth Stephano ambaye anajishughulisha na biashara ya duka.

UCHUMI

# Haja ya mjadala na maoni kwenye ongezeko la watu, kushuka kipato



Shughuli za Sensa ya Watu na Makazi, zilipokuwa zinaendelea mwaka huu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

INAWEZEKANA kukawepo uhalisia kwamba kuongezeka idadi ya watu, isiwe faraja ya moja kwa moja kwa taifa na badala yake kubaki changamoto, pale inapotokea uwezo wa kiuchumi kitaifa inapokea kushindwa kumudu.

Pia, si ajabu siku zinavyoenda uwezo wetu wa kuzitatua ukapungua zaidi. Taswira hiyo si jumuisho halisi la mantiki ya takwimu za ongezeko la watu nchini, kutoka watu milioni 44 na ushee katika sensa ya mwaka 2012 hadi watu milioni 61 sensa ya mwezi Agosti.

Ni hali inayoanza kuangaliwa kwa karibu na wapanga sera, pamoja na wachangiaji muhimu, yaani bunge kusaidia kupata majawabu ya changamoto na kuoanisha uhalisia huo na mipango yetu ya uchumi endelevu.

Mojawapo ya yanayoweza kujiri kutokana na takwimu za ongezeko la watu ni kushuka kipato cha wastani cha Watanzania ambacho sasa kinakaridiwa kufikia dola 990 za Marekani, chini ya wastani wa dola 1,000 kwa kila raia ili kupiga hatua kiuchumi.

Ni hali iliyovuruga mwonekano wa nchi, baada ya faraja iliyopatikana mwaka 2019 na 2020 kuwa sasa tumeingia katika uchumi wa kati. Magumu ya ukuaji uchumi na ongezeko la watu, vinapaswa kushikana kimkakati, ili jamii ibaki katika uchumi wa kati.

> **“ Majadiliano bungeni hayakuonekana kuzama kwa kina katika suala la ongezeko la watu na jinsi linavyotofautiana na kukua uchumi kwa jumla.**

Kinachoangaliwa sasa, ni vianzio vya uchumi vinavyoweza kuongeza kwa kiwango kinachoridhisha ukubwa wa uchumi wa nchi kwa jumla, uendane na ukubwa utakaokuwepo wa idadi ya watu.

Hiyo ndio inatetewa kiuchumi kwa namna ndio hali itakayowezesha Tanzania kurudi katika uchumi wa kati kwani idadi isiyo ndogo ya watu, inakuwa na hali bora zaidi ya uchumi pale inapopatikana njia ya kukuza uchumi kwa haraka, kwa maana kuongeza kipato kwa jumla.

Licha ya uhalisia kulingana na mazingira ya ukuaji huo au ongezeko la haraka la pato la taifa kwa jumla, muhimu ni pale viwango vya umaskini vitapungua na vichaka vya umaskini sugu kuondoka.

Njia mojawapo inayoweza kuleta mabadiliko katika eneo hilo, ni mradi wa kuchakata gesi asilia iwekwe katika mitungi, ambao hesabu zake kwanza kwa uwekezaji halafu kwa kuongeza pato la taifa.

Moja ya miradi iliyotakiwa iwe imetekelezwa miaka mitano au hata tangu 10 ulipobuniwa. Mwelekeo uliopo ni kutoa uhuru mpana kwa taasisi za usimamizi, kupanga mazingira ya uwekezaji, hatua hiyo bado haina kasi ikiangaliwa kwa karibu.

Utashi na mwelekeo wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ni kwamba sasa kuna mwanga kuwa mradi huo utatekelezwa na masharti yanayokubalika kwa mwekezaji kupita.

Wataalamu wanasema, mradi huo unahitaji zaidi ya dola bilioni 30 (wastani wa Sh. trilioni saba) kuanzishwa na hizo ni takwimu za miaka 10 iliyopita. Ni wazi gharama zitakuwa zimepanda.

Hivyo, ni jukumu la wabunge kuisaidia serikali kupata majawabu kwa matatizo magumu, licha ya kuwa kimsingi kinachofanyika katika maeneo tofauti, kinatokana kwanza na sera ya kisiasa (hasa kwa hatua za kimaendeleo, huduma za jamii) kila eneo. Vilevile kuna maoni ya rais aliyepo madarakani.

Majadiliano bungeni hayakuonekana kuzama kwa kina katika suala la ongezeko la watu na jinsi linavyotofautiana na kukua uchumi kwa jumla.

Imezama zaidi katika kuongeza juhudi katika maudhui ya uchumi, yaweze kukua haraka inavyotakiwa, kupunguza umasikini na kuongeza namna ya kugawana kilichopo.

Michango inaelekezwa katika umuhimu wa serikali kuongeza fedha za bajeti kwa sekta tangulizi, kuongeza ajira, mfano katika sekta kilimo ambako tayari kuna mkakati muhimu wa umwagiliaji; kuna vipingamizi pale miradi ya umwagiliaji inapoingiliana na upatikanaji maji.

Yako maeneo ya ubunifu wa kitaasisi yanayotokana na uzoefu serikalini wa baadhi ya wabunge wanaofurahia mifumo inayotumika kuendesha uchumi hadi sasa, licha ya mikwamo ya kushindwa kutumika hazina ya chuma na makaa ya mawe, au mradi wa kuchakata gesi kwa zaidi ya muongo mmoja sasa.

**MAWAZO MAPYA**

Wazo mojawapo la kitaalamu, ni kurejeshwa Tume ya Mipango iliyojumuishwa katika Wizara ya Fedha na Mipango, hata yakabanwa matumizi kiasi. Mipango kamili ni wawekezaji wanaridhia nini, halafu benki ndani ya nchi ziko tayari kukopesha kwa maeneo gani yenye tija, kurudisha fedha wanazokopa.

Ongezeko la watu, bado linaleta magumu hasa kibajeti, pale haja kama ya kuhakikisha nchi nzima inakuwa na bima ya afya kuweka hali za wananchi kiafya kuwa sawa.



## Wahamasishana matumizi mbolea asili kukabiliana mabadiliko tabianchi

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

KATIKA kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, wakulima wa zao la mpunga Wilaya ya Kyela, wamehamasishana kutumia mbolea za asili ikiwamo mboji ili kuhimili ukame na kutunza unyevu utakaosaidia kustawisha mazao.

Wakulima hao walitoa kauli hiyo juzi walipozungumza na Nipashe kuwa wamejiandaa kutumia mbolea za asili ambazo zitasaidia kuhimili hali ya ukame na kustawisha mazao shambani.

Furaha Mwasongela alisema licha ya kutambua faida za matumizi ya mbolea kwenye kilimo kwa ajili ya kutunza ikolojia, ni muhimu wakapatiwa elimu ya namna bora wanaweza kutumia mbolea hiyo ili kutunza mazingira.

Alisema kilimo cha Ikolojia kwenye zao la mpunga kina tija kubwa kwa wakulima kwani kwa kuzingatia maelekezo ya matumizi ya mbolea za asili zitasaidia kutibu afya ya udongo ambao kwa sasa umeathiriwa na matumizi ya mbolea za viwandani.

"Kwa sasa mambo yamebadilika, tumesikia na kuona kwenye vyombo vya habari kuhusu ukame, hali ya hewa na ukosefu wa maji hatujui mvua zitaanza lini ili tuanze msimu wa kilimo, lakini tunadhani tunapaswa kuachana na matumizi ya hizi mbolea za viwandani ambazo zina kemikali nyingi, tutumie hizi mbolea za asili kwa ajili utunzaji wa mazingira wakiwamo na viumbe hai na kupata mavuno mengi," alisema Mwasongela.

Akizungumzia faida za kilimo Ikolojia, Salome Mahusi alisema kimewasaidia wakulima hao, kutumia gharama ndogo za uzalishaji ambao kazi yao kubwa ni kuandaa mbolea za asili ambazo ni mboji zinazopatikana kwa urahisi ukilinganisha na zile za viwandani ambapo kwa msimu huu ziliuzwa hadi Sh. 130,000 kwa mfuko mmoja wa mbolea ya Dap.

Kwa upande wake, William Mmari, ambaye ni mtafiti wa udongo kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Uyole, alisema kutokana na matumizi ya mbolea ya viwandani kumechangia kwa kiasi kikubwa kuharibu afya ya udongo.

Alisema kilimo cha Ikolojia kimekuja kutibu afya ya udongo na kuwawezesha wakulima wa mpunga kupata mavuno mengi na yenye ubora ikilinganishwa na ilivyokuwa awali.

# Ukosefu daktari wa mifugo Rungwe wakwamisha ufugaji

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

LICHA ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuongoza kwa uzalishaji wa maziwa mkoani Mbeya, haina daktari wa mifugo hali inayokwamisha maendeleo ya ufugaji wa ng'ombe.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, ameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuajiri Ofisa Mifugo wilayani humo ili kutatua tatizo la uzalishaji bora wa maziwa.

Dk. Anney alitoa kauli hiyo jana kwenye uzinduzi wa kikundi cha Umoja wa Wanawake Wafugaji Rungwe, (UWAWARU) na alisema kukosekana kwa mtaalam wa mifugo wilayani humo kunaathiri ubora wa maziwa kutoka kwa wazalishaji kwa sababu ya kukosa elimu ya kuzalisha maziwa yenye kukidhi ubora.

"Wilaya hii ni ya kimkakati kwenye sekta ya maziwa ili kufanikisha azma ya ujenzi wa viwanda na wafugaji kupata faida kutokana na uzalishaji wa bidhaa hii tunaomba tupatiwe maofisa ugani wa kutosha pamoja na Ofisa Mifugo wa wilaya ambaye atakuwa daktari atakayesaidia kufanya operesheni hapa ili mifugo ikiwa na tatizo iwe rahisi kuitibu," alisema Dk. Anney.

Alisema uongozi wa wilaya utampatia ushirikiano wa kutosha Ofisa Mifugo atayaletwa wilayani humo kwa kuhakikisha anapatiwa vitendea kazi na masuala mengine ambayo yatamsaidia kutimiza majukumu yake ipasavyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, aliwaomba madiwani kuhamasisha kinamama kujiunga kwenye vikundi vya uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa.

Alisema vikundi vya uzalishaji maziwa kwa kinamama wa Wilaya ya Rungwe vina tija kubwa kwa kuwa vimewasaidia kujikwamu kiuchumi na kwa sasa wameanza kukopeshana fedha zinazotokana na mauzo na faida ya uuzaji wa maziwa.

Mwakilishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ambaye pia ni Mkurugenzi Msaidizi wa Utafiti wa Mifugo nchini, Hassan Mrutu, alisema Wilaya ya Rungwe imebarikiwa kuwa na mazingira mazuri ya hali ya hewa ambayo yanaruhusu ufugaji mzuri wa ng'ombe wa nyama na maziwa.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo wamejitahidi kufuga kisasa na wanazingatia ufugaji bora na wa kisasa wa mifugo yao ya kuchunga ndani ya zizi ikilinganishwa na baadhi ya maeneo nchini ambayo ufugaji wao ni wa kuhamahama.

Kutokana na mazingira hayo alisema ipo haja kwa serikali kuwasaidia wafugaji mbinu bora za uzalishaji ili kuongeza maradufu ya ilivyo sasa kwa kuhakikisha wanapatiwa wataalam wa mifugo. Mwenyekiti wa UWAWARU, Emmy Masetta, alisema umoja wao ulianzishwa mwaka 2021 ukiwa na lengo la ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na wanyama wengine kama nguruwe.

Alisema umoja huo umefanikiwa kuzalisha Sh. milioni kumi zinazotokana na michango ya hisa kwa wanachama pamoja na amana.

Umoja huo wenye wanachama 30 umeweka malengo hadi kufikia Desemba 2025, watakuwa wamekusanya Sh. milioni 50 kutokana na shughuli ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

"Tumefanikiwa kumiliki ng'ombe 100 wenye thamani ya Sh. milioni 200, lakini jitihada zetu zimeungwa mkono na kampuni ya ununuzi wa maziwa ya Asas Diaries Limited ambayo ilitupatia Sh. milioni 10 kwenye mtaji wetu, mafunzo kwa viongozi wa vikundi pamoja na wataalam wakati wa mchakato wa kuandaa katiba," alisema Masetta.

Alisema licha ya mafanikio yao, wanakabiliwa na vikwazo mbalimbali vya bei kubwa ya ununuzi wa ng'ombe bora na tija kidogo inayopatikana kwenye uzalishaji wa maziwa.




Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere (wa tatu kushoto), akitoa mada kwenye kongamano la kumbukizi ya kifo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Mzumbe Ndaki ya Mbeya jana. (Wa tatu kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Dereva aliyegonga gari, kuua wanafunzi akamatwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya, limemkamata dereva wa basi mali ya kampuni ya Mangare linalofanya safari zake kati ya Mbeya na Sumbawanga baada ya kugonga gari lenye namba za usajili T.452 DHD aina ya Toyota Raum na kusababisha vifo vya wanafunzi wawili na majeruhi watatu.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamini Kuzaga, dereva huyo ni Zefania Marijani (42), mkazi wa Iwambi jijini Mbeya.

"Baada ya dereva huyo kusababisha ajali kwenye mteremko wa Iwambi alikimbia kusikojulikana, polisi tulianza msako mara moja wa kumtafuta mahali alipo tulifanikiwa kumkamata tayari yuko kwenye mikono ya sheria," alisema Kuzaga.

Kamanda Kuzaga aliwataja watoto waliopoteza maisha kuwa ni Maria Alute (15) na Halima Mwaijumba (14) wanafunzi wa kidato cha pili.

Majeruhi wa ajali hiyo ni Seleman Ndosi (35), dereva wa Toyota Raum, Mwanaidi Kapalata (36) Mtumishi katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya pamoja na Sharifa Shushu (59), mkazi wa Iwambi.

Alisema majeruhi wote wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya na hali zao zinaendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazofanywa na madaktari.

Uongozi wa Shule ya Sekondari ya St. Francis, ulieleza majonzi yake ya kumpoteza mwanafunzi wao, Maria Alute wa kidato cha pili.

Mwalimu wa nidhamu wa shule hiyo, Neema Kimani, alisema marehemu Maria alimaliza mitihani yake vizuri na wiki iliyopita aliondoka shuleni hapo na kwenda kwa mlezi wake aishiye jijini Mbeya kwa ajili ya likizo.

Alisema taarifa za kifo cha mwanafunzi wao walizipata Novemba 9, mwaka huu majira ya saa tatu asubuhi ambapo waliarifiwa kuwa marehemu na ndugu zake walikuwa safarini kuelekea uwanja wa Ndege wa Songwe kwa ajili ya kwenda jijini Dar es Saalam.

"Tulipigiwa simu kwamba mwanafunzi wetu Maria amefariki dunia kwa ajali, habari hii ilitupa mshtuko kwa sababu wiki iliyopita alikuwepo hapa shuleni, tulitoa taarifa kwa wanafunzi wote na mara moja ratiba ya vipindi vya masomo ikavunjwa wanafunzi wakaanza kufanya sala huku tukisubiri taratibu nyingine za msiba ili tushiriki kikamilifu," alisema Kimani.

Alisema mwanafunzi Maria atakumbukwa kwa ukimya, upole na utulivu wake nyakati zote alizokuwepo shuleni hapo ambapo alikuwa ni mtu asiyependa ugomvi, hakuna kesi yeyote aliyofikishiwa mwalimu huyo ikimhusu Maria kuhusika na utovu wa nidhamu.

HABARI DODOMA



# Wafunga barabara kwa saa tatu wakishinikiza kujengwa matuta

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Kibaigwa, Kongwa mkoani Dodoma, wameifunga barabara kuu ya Dodoma - Morogoro kwa zaidi ya saa tatu wakishinikiza serikali kuweka matuta kutokana na vifo vinavyotokana na ajali za mara kwa mara katika eneo hilo.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake katika eneo la tukio, John Peter, mwanafunzi wa darasa la sita, alisema wamelazimika kuchukua hatua hiyo kwa lengo kuiomba serikali kuweka matuta kwa kuwa wamechoka kuona ndugu zao wakigongwa kama wanyama na maderevea wa magari.

"Tumelazimika kuifunga barabara hii ili serikali iweke matuta hapa. Tunaumia kuona wenzetu wakipoteza maisha kutokana na uzembe wa madereva wanaoendesha bila kuchukua tahadhari kuwa eneo hili kuna wanafunzi, wazee na wenye ulemavu," alisema Peter.

Naye Aisha Ramadhani, mmoja wa wazazi waliopoteza watoto kwa kugongwa na gari katika eneo hilo, alisema hakuna jitihadi zilizofanyika pamoja na uongozi wa eneo hilo kupatiwa taarifa. Alisema, serikali inatambua kilio cha wananchi juu ya eneo hilo kuomba kuwekewa matuta ili kupunguza ajali za mara kwa mara ambazo zinazosababisha vifo.

Ally Athumani (65) alisema serikali ya wilaya hiyo imekuwa na utekelezaji wa kusuasua hali ambayo imesababisha wanafunzi kuamua kuweka matuta na kuisimamisha barabara na kuleta usumbufu kwa watumiaji wengine.

Kutokana na tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, akizungumza na wananchi katika eneo hilo, alisema serikali tayari imeshaanza kuchukua hatua ya kuweka matuta kwenye eneo hilo.

Aliwataka wananchi kutokuwa na hasira na kujichukulia hatua za haraka kama tukio hili la kufunga barabara kwa kuwa wanaweza kusababisha hasara nyingi kwa serikali na hata wao binafsi.

"Kumbukeni mkifunga barabara watumiaji wako wengi. Kuna wagonjwa wanaowahishwa hospitali mizigo inayotakiwa kufikishwa kwa haraka kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu pia hata mapato yanaweza kupungua," alisema.

Mkuu huyo alisema jitihada za awali za uwekaji wa mchanga kwa ajili ya ujenzi wa matuta kwenye eneo hilo zimeanza hivyo kero ya kugongwa inaenda kumalizika. Pia aliwataka waendesha vifaa vya moto kuzingatia sheria za barabarani ikiwamo kujiepusha na mwendo kasi unaoweza kusababisha ajali na vifo.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo kuhusu kimondo chenye tani 12 na cha nane duniani kutoka kwa Mhifadhi Msimamizi Mwandamizi wa Wanyamapori wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Lowaeli Damalu (kulia), alipotembelea maonyesho ya utalii karibu kusini 2022, wilayani Kilolo, mkoani Iringa jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wanufaika mikopo wapatiwa mafunzo

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

WANUFAIKA wa mikopo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa wamepatiwa mafunzo ya namna ya kufanya biashara ili mikopo waliyopatiwa iwe na tija na kuwainua kiuchumi.

Mafunzo hayo yamefanyika katika ukumbi wa mikutano wa halmashauri na kuhudhuriwa na wanavikundi waliopata mkopo kwa robo ya kwanza.

Akitoa mada katika mafunzo hayo, Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Kondoa Mjini, Paschal Materu, aliwataka wanufaika hao kuwa wabunifu katika biashara wanazofanya ili kujiongezea soko na kuacha kufanya kazi kimazoea.

"Lazima unapofanya kazi zako ujiwekee malengo na ujiamini na huwezi kujiamini kama unatoa bidhaa mbovu ndiyo maana nimekwambia wale washindani wako unatakiwa uangalie wapi wanapofeli wewe ndiyo unaboresha. Wote tunashona nguo lakini ushonaji wangu na wako unatakiwa utofautiane hata kama mnauza bei moja, wa kwako ukiwa bora. Lazima watu watakuja kwako hata kama utaongeza bei," alisema.

Pia aliwataka kuwa na uhitaji wa mafanikio kutokana na wanachofanya na kile wanachotamani kufikia siku zijazo kutokana na faida anayoipata ikiwa ni pamoja na kuwa tayari kuibeba hasara. Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Latipha Koshuma, aliwataka wanavikundi hao kuwa makini wakati wa ununuzi wa mashine walizoomba kwa kuepuka kununua vitu mtandaoni kwa kuwa kufanya hivyo wanaweza kupoteza fedha kwa kuwalipa watu wasiowajua na kukosa mashine.

"Mnatakiwa kuchagua watu wawili kwa ajili ya kwenda Dodoma au Dar es Salaam kulingana na mashine mnazotaka. Nendeni moja kwa moja dukani mkaombe 'profoma invoice' halafu mrudi kuwaonyesha wanakikundi wengine na awape akaunti namba ya benki mfanye malipo halafu awatumie mashine. Msifanye vitu 'online' (kwa njia ya mtandao), hiyo itawapotezea muda na mnatakiwa kuwa makini," alisema.

# Kairuki atia mkono ujenzi madarasa 8,000

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia ujenzi wa madarasa 8,000 ya shule za sekondari nchini ili yakamilike kabla ya Desemba 15, mwaka huu.

Kairuki alisema hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa nne wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA).

Alisema wakuu wa mikoa na wilaya wanatakiwa kusimamia ujenzi huo wa madarasa 8,000 ya shule za sekondari ambayo yanaendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali.

Kwa mujibu wa waziri, madarasa hayo yanapaswa kukamilika kabla ya muda huo ili kutoa fursa kwa wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

"Nitumie mkutano huu kutoa maagizo kwa wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya wote kuhakikisha ujenzi wa madarasa 8,000 ya shule za sokondari yanakamilika kama ilivyopangwa ili wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, wajiunge bila kikwazo chochote.

"Pia nawaagiza kuhakikisha ujenzi wa shule 232 ambazo tulipeleka Sh. milioni 470 kwa kila shule unakamilika. Ujenzi huu ulipaswa kukamilika Oktoba 31 lakini bado kuna shule ambazo hazijakamilika hadi sasa," alisema. Kairuki alisema serikali imetoa Sh. bilioni 160 ili kujenga madarasa 8,000 ikiwa ni maandalizi ya kuwapokea waliohitimu darasa la saba mwaka huu ambao wanatarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza Januari, mwakani.

"Serikali imeshatuma fedha hizi zote katika mamlaka za serikali za mitaa na shule za sekondari zinazohusika nchini ili zikamilishe ujenzi wa madarasa haya ifikapo Desemba 15, mwaka huu," alisema.

Kairuki pia aliwaagiza wakuu wa shule za awali na msingi pamoja na sekondari nchini kusimamia vizuri utekelezaji wa mtaala wa elimu msingi na sekondari ili kuwawesha wanafunzi kupata maarifa, ujuzi na stadi zilizokusudiwa kwao kuwasaidia kukabiliana na mazingira wanayoishi.

"Kwa kuwa msingi wa elimu bora unajengwa kwenye elimu ya awali na msingi, walimu wakuu na walimu wote wa shule za awali na msingi nchini wahakikishe wanafunzi wanapata umahiri na ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) wamalizapo darasa ya kwanza," alisema.

Aidha, walimu wa somo la Kiingereza wa shule za msingi wahakikishe wanafunzi wanapata umahiri wa lugha hiyo wanapomaliza darasa la saba, ili kuwapa umahiri kumudu masomo ya sekondari ipasavyo ambako lugha ya kujifunzia ni Kiingereza.





# JK ataja mipango udhibiti vifo uzazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MJUMBE wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Rais mstaafu wa Tanzania, Jakaya Kikwete, amesema wanashirikiana na viongozi wa nchi za mataifa duniani kuhakikisha vifo vinavyotokana uzazi vinadhibitiwa ifikapo mwaka 2030.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kutembelea na kupata taarifa ya kituo cha kutoa huduma kwa wajawazito na watoto, Sebleni mjini Unguja, alisema wakati umefika kuona viongozi wa nchi kujikita katika kuhakikisha bajeti za wizara za afya zinakidhi mahitaji yote muhimu.

Kikwete pia alisema wakati umefika kuona huduma hizo zinafikishwa vijijini ambako zitawapunguzia mzigo kinamama wa kutembea masafa marefu kutafuta huduma hizo ikiwamo kuhudhuria kliniki kwa wakati.

"Miongoni mwa majukumu yetu na mikakati ambayo tumeiweka ni kuhakikisha viongozi wa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa wanahakikisha huduma za kinamama na watoto zinawafikia walengwa ikiwamo kuwapo kwa bajeti nzuri katika Wizara ya Afya ambayo itawezesha kufikisha huduma hizo kwa walengwa," alisema.

Naye Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema Zanzibar iko katika mikakati na juhudi za kutekeleza malengo endelevu ya Umoja wa Mataifa ikiwamo kupunguza vifo vinavyotokana na wajawazito na watoto kwa kufikisha huduma hadi vijijini.

Katika kutekeleza mpango huo, alisema serikali ya Zanzibar imetenga Sh. bilioni 36 kwa ajili ya kujenga hospitali 11 za wilaya Unguja na Pemba ambazo baada ya kukamilika zitakuwa na uwezo wa kutoa huduma za wajawazito na watoto kwa kiwango cha hali ya juu.

Alisema mikakati ya Wizara ya Afya ni kuona kwamba hakuna wajawazito na watoto wanaojifungua majumbani kwa sababu hospitali hizo za ziada zitakuwa na huduma kamili.

# Umaskini bado kikwazo kwa watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, amesema licha ya hali ya umaskini kwa watoto Zanzibar kupungua, bado wanaendelea kuathirika na tatizo hilo na kushindwa kufikia malengo yao.

Hayo aliyasema jana kwenye mkutano wa uzinduzi wa matokeo ya Utafiti wa Hali ya Umaskini Zanzibar, uliofanyika Hoteli ya Madinat Al Bahr, Mbweni mjini Unguja.

Alisema kutokana na uchambuzi wa taarifa za utafiti wa mapato na matumizi ya kaya kwa miaka 10, Zanzibar inatakiwa kuimarisha mipango yake na kuweka mazingira mazuri ili kukabiliana nayo.

Utafiti huo unaonesha kwamba watoto chini ya umri wa miaka 17 wanaathiriwa na matatizo mbalimbali yakiwamo ya elimu, afya, makazi bora na lishe, hali ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa watoto kuendelea kuwa maskini na kudumaza maendeleo yao.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Zanzibar, Rahma Mahfoudh, alisema kuzinduliwa kwa ripoti hiyo kutasaidia kujua ukubwa wa hali ya umaskini nchini ukiwamo wa watoto na kuelekea uchumi shirikishi.

"Kama inavyofahamika umaskini ni tatizo linalotokana na kukosekana kwa upatikanaji wa mahitaji ya msingi ya binadamu yakiwamo chakula, maji safi na salama, huduma za afya, malezi, elimu na huduma za malazi," alisema.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF), Shalini Buhuguna, alisema licha ya kuwa watoto wengi wanaishi na umaskini, Zanzibar imepiga hatua kubwa katika mipango yake ya kupunguza umaskini hasa kwa watoto.

Alisema Serikali ya Zanzibar imekuwa na sera ya kumjali mtoto ikiwamo kumrudisha shuleni ili kupata elimu kwa ajili ya maendeleo yake na taifa.

Pia alisema mipango ya UNICEF ni kuendelea kushirikiana na Serikali ya Zanzibar katika mpango wa kuwajali watoto katika nyanja mbalimbali yakiwamo makuzi yao.

Mchumi Mwandamizi kutoka Benki ya Dunia, Rob Swinkels, alisema nchi nyingi za Afrika bado zimekuwa na tatizo la umaskini wa kipato, waathirika wakuu wakiwa watoto.

Hata hivyo, alisema Zanzibar imepiga hatua kwa kuwajali kinamama na watoto katika kuwajengea mazingira mazuri ya kumudu maisha yao.

"Benki ya Dunia kwa kushirikiana na serikali ya Zanzibar bado ina mipango mizuri ya maendeleo ikiwamo ya kuwasaidia kinamama na watoto," alisema.

Akiwasilisha matokeo ya ripoti za utafiti kwa kipindi cha mwaka 2009 hadi 2019 kwa watoto Zanzibar, Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Pato la Taifa, Khalid Chum, alisema kiwango cha kupunguza umaskini kimepungua kwa takriban asilimia moja kwa mwaka katika kipindi hicho.

Alisema hali hiyo ilipungua kutoka asilimia 34.9 mwaka 2009 hadi asilimia 30.4 mwaka 2015 na asilimia 25.7 mwaka 2019, hali ambayo inaonesha kuwa umaskini umepungua kwa asilimia 9.2 ndani ya kipindi cha miaka 10.



Mwenyekiti Mwenza wa Kamisheni ya kufuatilia maazimio yaliyofikiwa katika mkutano wa Nairobi wa mwaka 2019, Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, akizungumza na wajawazito waliofika katika Kituo cha Afya cha Sebleni, mjini Zanzibar jana kwa ajili ya kupima afya zao. Kulia ni Mrithi wa Mfalme wa Denmark, Mary ambaye ni miongoni mwa wajumbe 29 wanaounda kamisheni hiyo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# BoT yaridhishwa ujenzi uwanja wa ndege

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imeridhishwa na hatua za ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume katika jengo lake la tatu la abiria (Terminal Three) ambalo kwa sasa liko katika hatua za mwisho kukamilika.


Hayo yalisemwa jana visiwani humo na Gavana wa BoT, Prof. Florence Luoga, alipofanya ziara katika jengo hilo.

Alisema visiwa vya Zanzibar vinategemea utalii katika harakati zake za kiuchumi ili kuongeza pato na kwa maendeleo kwa ujumla, hivyo kukamilika kwa jengo hilo kutafanya idadi ya watalii kuongezeka.

Prof. Luoga alisema benki inasifu jitihada za serikali ya Zanzibar kwa kuendeleza na kusimamia vyema miradi yake ya maendeleo ukiwamo uwanja huo ambao kwa sasa uko hatua za mwisho kukamilika. Gavana huyo alisema nchi yoyote ya kisiwa ina wigo wa kutengeneza viwanja vya ndege ili kuona namna gani watalii wanaoingia wanakuwa salama katika safari zao za utalii. Alisema katika kipindi kifupi kijacho baada ya uwanja huo kukamilika, Zanzibar itarajie kuwa na wageni wengi kwa vile usafiri wa anga ni mzuri na miundombinu yake ni bora. Pia alisema majengo ya uwanja huo yanawashawishi wageni kufika Zanzibar kutalii na kuwafanya wawekezaji kuwa na hamasa ya kuwekeza kwa vile usafiri wa anga unavutia.

Katika kukuza uchumi, alisema BoT inahusika kutoa ushauri katika mambo mbalimbali yanayohusu fedha ili uchumi ukue na maendeleo kupatikana kwa haraka. "Benki Kuu imeridhishwa na namna gani uchumi utakavyokuwa kwa vile huduma za ubadilishaji wa fedha za kigeni zitapatikana katika uwanja huu," alisema Gavana huyo," alisema.

Pia alisema licha ya uwepo wa changamoto vita kati ya Ukraine na Urusi na kuifanya dunia kuwa katika hali ngumu ya kiuchumi lakini Tanzania bado ipo salama katika uchumi wake.



# Wenye ualbino waomba ulinzi uimarishwe

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya watu wenye ualbino mkoani Mwanza wameiomba serikali kuimarisha ulinzi wao ili kukabiliana na matukio ya kikatili na mauaji yaliyoanza kujitokeza hivi karibuni.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, walisema kwa sasa wameanza kuishi kwa hofu licha ya serikali kujitahidi kuweka nguvu kuwabaini wahusika wa tukio la mwenzao kukatwa mkono na kusababishiwa kifo.

Emanuel Jacob, mkazi wa Mwanza wilayani Ilemela, mwenye ualbino alisema jana kuwa, kutokana na tukio lililotokea usiku wa kuamkia Novemba 3, mwaka huu la kuuawa kwa mwenzao Joseph Mathias, mkazi wa kijiji cha Ngulla, wilayani Kwimba na baadhi ya watu kuanza kuwatenga na kuwaogopa.

Alisema hivi sasa inahitajika serikali kuimarisha ulinzi na kutoa elimu kwa jamii ili waache kuwatenga na kuwaogopa kwa kuwa wao ni watu kama wengi licha ya utofauti wa ngozi.

Angelina Chuma, Katibu wa Chama cha Watu wenye ualbino Mkoa wa Mwanza alikemea wahusika wa kitendo cha mauaji mwenzao huku akiiomba jamii kuendelea kuishi nao kama watu wengine na wasiwaogope kutokana na hofu ya kuhusishwa na hatari ya kuwa karibu nao.

Naye Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Mwanza, Stalon Makoye, aliipongeza serikali mkoani humo kupitia Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, aliyehakikisha wahusika wa tukio la mwenzao kukatwa mkono wanakamatwa wakiwa na kipande hicho cha mkono.

Makoye aliiomba serikali kupitia mihimili yake kuchukua hatua stahiki kwa watu hao ikiwa ni pamoja na kuharakisha kesi hiyo ili waathirika wapate haki yao mapema na kuifanya jamii iendelee kuwaheshimu na kuwathamini.

Novemba 3, mwaka huu, baada ya kutokea kwa tukio hilo Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alitoa siku saba kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha wanawapata wahusika wa tukio hilo na kuwachukulia hatua.

Ndani ya siku tatu Jeshi la Polisi mkoani hapa lilitoa taarifa ya kukamatwa kwa watu watano wanaohusika na tukio hilo ikiwa ni pamoja na mwanamume mmoja ambaye jina lake lilihifadhiwa kwa ajili ya upelelezi zaidi aliyekamatwa na kipande cha mkono kilichokatwa kutoka kwa mtu mwenye ualbino.

Mtu huyo mkazi wa kijiji cha Ngulla, alikamatwa katika Kata ya Kanyerere, wilayani Misungwi, akiwa amebeba begi lenye mkono huo baada ya kuhisiwa na wananchi kutokana na kutoa harufu kali.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akishiriki ujenzi wa vyumba vya madarasa vitano katika shule mpya ya Sekondari Salawe, alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa shule hiyo juzi, ili mwakani ianze kufundisha wanafunzi wa kidato cha kwanza. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Familia yaomba eneo lao wanalodai kuchukuliwa na CCM

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

FAMILIA ya marehemu Musa Kasuka, mkazi wa kijiji cha Mpera, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamelazimika kushinda kwenye kaburi la babu yao wakimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwasaidia kupata eneo lao linalodaiwa kuchukuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Gazeti hili lilikuta familia hiyo juzi katika eneo la kaburi la babu yao na walipohojiwa walibainisha kuwapo kwa vitu mbalimbali vya familia hiyo likiwamo kaburi hilo.

Mussa Makoye, mmoja wa wanafamilia hao alisema katika eneo hilo ambalo kwa sasa linamilikiwa na CCM kuna miti ya miembe, misonobari pamoja na nyumba moja chakavu aliyokuwa anaishi marehemu babu yao na kaburi lake.

Alisema marehemu babu yao alilipata mwaka 1974 kwenye operesheni kijiji na alifariki mwaka 1982 na kudai chama hicho kilimuomba mke wa marehemu kutumia nyumba hiyo kama ofisi ya chama.

Edward Makoye, mwanafamilia alisema wamefuatilia eneo hilo bila mafanikio licha ya kufuata utaratibu na mpaka sasa yapata miaka 20 tangu mama yao alipofariki hali inayowafanya kushinda kaburini kwa babu yao wakimwomba Rais Samia kuwasaidia kulipata eneo lao.

Aidha, alisema familia yao walikubaliana kuwakatia eneo lingine Serikali ya Kijiji cha Mpera ili wajenge Ofisi ya Kijiji chini ya diwani aliyekuwa madarakani, Andrew Gerado, mwaka 2015-2020, lakini ilishindikana na kuendelea kulitaka eneo hilo ambalo linakaburi na nyumba ya babu yao aliyefariki tangu mwaka 1982.

Naye mzee maarufu wa kijiji cha mpera, Omari Mayala (102) alisema, marehemu mzee Mussa walipakana mipaka ya viwanja vyao na mashamba hayo yalikuwa ni ya ujamaa waliyoyapata kwenye operesheni kijiji tangu mwaka 1974.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kahama, Thomas Muyonga, akijibu malalamiko hayo alisema, hajapata taarifa rasmi za suala hilo japo anazisikia fununu huku akiahidi kulifuatilia kujua uhalali wake.

Muyonga alisema, mali zote za chama zipo chini ya Baraza la wadhamini la chama na kuwataka wajukuu wa marehemu kufuata taratibu za kisheria ili haki iweze kutendeka kwa kila mmoja kuliko kuendelea kushinda kaburini na kulalamika.

# Mwanafunzi aliyetoroshwa kuozwa aokolewa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amemwokoa mwanafunzi wa kidato cha pili aliyekuwa akisoma katika Shule ya Sekondari Solwa wilayani Shinyanga, ambaye alitoroshwa na wazazi wake kwa ajili ya kwenda kuozwa Mpanda, mkoani Katavi.

Mboneko alibainisha hayo Novemba 9, 2022 alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa, pamoja na kumtembelea mwanafunzi huyo katika Shule ya Sekondari Solwa, ambaye kwa sasa yupo chini ya uangalizi wa serikali na anaishi na mwalimu shuleni hapo.

Alisema, Oktoba 28, mwaka huu, alipokea taarifa kuwa kuna mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Solwa ametoroshwa na baba yake na kupelekwa Mpanda mkoani Katavi kwa ajili ya kuozwa, ndipo akafanya mawasiliano na Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika- Katavi na kufanikiwa kumkamata mzazi wake na mtoto huyo huku muoaji akitokomea kusikojulikana.

"Nilipopewa taarifa tu juu ya mtoto huyu, siku hiyo hiyo nilifanya mawasiliano ya haraka na Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika tukawakamata na kufanikiwa kumrudisha mtoto shuleni na akafanya mtihani wake wa kidato cha pili," alisema Mboneko.

"Mwanafunzi huyu kwa sasa anaishi na mwalimu shuleni hapa chini ya uangalizi wa serikali na hatoruhusiwa kwenda likizo kwa wazazi wake, wao watakuwa wakija hapa shuleni kumsalimia na nitamsimamia hadi afike chuo kikuu na kutimiza ndoto zake," aliongeza Mboneko.

Katika hatua nyingine Mkuu huyo wa Wilaya aliwaonya wazazi kuacha tabia ya kuozesha wanafunzi wa kike wawaache wasome na kutimiza ndoto zao na kubainisha kuwa wataendelea kufuatilia watoto wote watoro shuleni ili kubaini wanakabiliwa na matatizo gani na kuzuia ndoa za utotoni.

Naye mwalimu anayeishi na mtoto huyo kwa uangalizi zaidi, Oliva Kalinga, alisema baada ya kumaliza mtihani wake wa kidato cha pili wanaendelea kumpatia masomo ya ziada ili aendelee kuwa vizuri darasani.

Mwanafunzi huyo (jina lake limehifadhiwa) alisema anapenda kusoma na ndoto zake ni kuja kuwa mwalimu, huku akimshukuru Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, kwa kuokoa ndoto zake.

## Mipango ufadhili yatangazwa mkutano wa COP27

**SHARM EL-SHEIKH,** MISRI

SUALA la ufadhili limechukua hatamu katika mkutano wa COP27 nchini Misri, huku wataalamu wakichapisha orodha ya miradi yenye thamani ya dola bilioni 120 za Kimarekani kuzisaidia nchi maskini.

Mradi wa dola bilioni tatu za Kimarekani wa kuhamisha maji baina ya Lesotho na Botswana pamoja na mpango wa kuboresha mfumo wa maji ya umma nchini Mauritius ulio na thamani ya dola milioni 10, ni miongoni mwa miradi iliyotangazwa jana ikijumuisha miradi 19 barani Afrika.

Mjumbe wa Marekani kuhusu mazingira John Kerry alitangaza kuundwa kwa mfuko wa kukabiliana na gesi ya kaboni unaolenga kuyasaidia mataifa yanayoendelea kuharakisha kuondokana na matumizi ya nishati ya mafuta ya kuchimbwa.

Kerry alizindua mfuko huo kwa jina la (ETA) kwa lengo la kufadhili miradi ya nishati mbadala na kuharakisha matumizi ya nishati safi katika nchi zinazoendelea, ambapo Chile na Nigeria ni miongoni mwa nchi ambazo zimeonyesha nia ya mapema katika mfuko huo.

"Kama hatutakuja na njia za ubunifu za kukusanya pesa tunazohitaji ili kuharakisha kipindi cha mpito katika sekta ya nishati, tutashuka chini ya nyuzi joto 1.5 katika kipimo cha Celsius na niko tayari kukubali kwamba tumekwama mahali ambapo hatuwezi kufikiria tofauti na kujaribu kitu tofauti ili kukamilisha kazi hii," alisema.

Wakati huo huo, Afrika Kusini itapokea kitita cha euro milioni 600 kutoka Ufaransa na Ujerumani kama sehemu ya mpango wa uwekezaji wa kuisaidia katika kipindi cha mpito wa nishati.

Taarifa ya pamoja imeeleza kwamba nchi hizo tatu zimesaini makubaliano ya mkopo kwa nchi mbili za Ulaya kutoa euro 300 kila mmoja ili kuzisaidia nchi hizo katika juhudi zake za kupunguza utegemezi kwenye nishati ya makaa ya mawe.

Afrika Kusini ambayo ni miongoni mwa mataifa 12 yenye uchafuzi duniani, inazalisha karibu asilimia 80 ya umeme wake kupitia makaa ya mawe.

Katika hatua nyingine, wanaharakati wa mazingira waliandamana nje ya mkutano wa COP27 katika mji wa Sharm al-Sheikh wakipinga mabadiliko ya serikali nyingi duniani katika matumizi ya nishati ya mafuta yanayoharibu mazingira katika jitihada za kukabiliana na mzozo wa nishati.

Mkutano wa COP27 unafanyika wakati ulimwengu ukikabiliwa na majanga ya asili, ikiwa ni pamoja na mafuriko, joto kali na ukame uliosababisha madhara makubwa katika maeneo kadhaa duniani. **DW**

# Urusi yaondoa vikosi Kherson Ukraine

**MOSCOW,** URUSI

URUSI imeviamuru vikosi vyake kujiondoa kutoka mji wa Kherson nchini Ukraine, mji mkuu pekee wa mkoa uliotekwa na majeshi ya Rais wa nchi hiyo Vladmir Putin tangu kuanza kwa vita hivyo vilivyodumu kwa miezi minane sasa.

Kherson ni moja ya mikoa minne ya Ukraine ambayo Rais Putin alitangaza mwezi Septemba kuiunganisha milele na Urusi, baada ya kura ya maoni iliyokoselewa kuwa haramu na Ukraine na washirika wake.

Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa jana na DW, tangazo hilo linakuja baada ya vikosi vya Ukraine kuzidi kusonga mbele na kuukaribia mji wa Kherson.

Katika maelezo yaliyotangazwa kupitia televisheni, kamanda wa jeshi la Urusi nchini Ukraine, Jenerali Sergei Surovikin, alisema haiwezekani tena kufikisha mahitaji mjini Kherson, na kupendekeza badala yake waimarishe safu yao kwenye kingo ya kushoto ya mto Dnieper.

"Nafahamu kuwa huu ni uamuzi mgumu sana, lakini wakati huo huo, tutahifadhi jambo muhimu zaidi maisha ya wanajeshi wetu, na kwa ujumla, ufanisi wa kimapambano wa askari, jambo ambalo halina faida kuimarisha eneo dogo la ukingo wa kulia," alisema Surovikin.

Waziri wa ulinzi wa Urusi Sergei Shoigu pia aliunga mkono maelezo hayo na kusema, "nakubaliana na mahitimisho yako na mapendekezo. Endelea na uondoaji wa vikosi na kuchukua hatua zote kuvusha wanajeshi mto."

Tangazo hilo pia lilikuja saa kadhaa baada ya naibu kiongozi wa Kherson aliyewekwa na Urusi, kuripotiwa kuuawa katika ajali ya gari, wiki kadhaa baada ya kuwasihi wakazi kuondoka katika eneo hilo.

Nao maofisa mjini Kyiv walijibu kwa tahadhari, wakisema jeshi la Urusi halina uwezekano wa kuondoka kutoka mji huo wa kimkakati bila mapigano, huku rais wa Marekani Joe Biden, akisema kujiondoa kwa Urusi ni ushahidi kwamba Moscow inakabiliwa na matatizo ya kweli kwenye uwanja wa mapambano.

Mchambuzi wa kijeshi na ulinzi wa Urusi mwenye makao yake mjini Moscow, Pavel Felgenhauer, alisema tangazo hilo lilikuwa pigo kubwa kwa Moscow, hatua iliyomsababishia ukosoaji mkubwa kwenye chaneli za Telegram zenye mafungamano na mrengo mkali wa kulia.

Waungaji mkono mashuhuri wa Kremlin akiwamo mwanzilishi wa kundi la mamluki wa kijeshi la Wagner Yevgeny Prigozhin, na mhariri mkuu wa shirika la habari la serikali la RT, Margarita Simonyan, walijaribu kulipaka mafuta tangazo la Surovikin, wakibainisha haja ya kunusuru maisha.

Katikati ya wiki hii daraja kuu lililoko kwenye barabara ya kutoka mji wa Kherson lililipuliwa, huku uvumi ukienea miongoni mwa wa Ukraine kwamba limelipuliwa na majeshi ya Urusi katika maandalizi ya kujiondoa.

Wakati huo huo ikulu ya Kremlin imetangaza kuwa Rais Putin hatohudhuria mkutano wa kilele wa mataifa ya G20 mjini Bali Indonesia, na badala yake atawakilishwa na waziri wake wa mambo ya nje Sergei Lavrov.

Mkuu wa itifaki wa ubalozi wa Urusi nchini Indonesia Yulia Tomskaya alisema "Naweza kuthibitisha waziri wa mambo ya nje Sergei Lavrov ataongoza ujumbe wa Urusi kwenye mkutano wa G20. Programu ya Rais Putin bado inafanyiwa kazi, huenda akashiriki kwa njia ya mtandao."

Rais wa Indonesia Joko Widogo alimualika Putin kuhudhuria mkutano huo unaotarajiwa kufanyika Novemba 15 -16 mwaka huu, huku ikielezwa kuwa Kremlin haijathibitisha mipango ya kiongozi huyo mpaka sasa. **DW**




Wanaharakati wa mazingira wakiandamana. **PICHA: MTANDAO**

## Kesi ufisadi inayomkabili Gachagua yafutwa

**NAIROBI,** KENYA

MAHAKAMA ya Kenya imeruhusu ombi la upande wa mashtaka kuondoa kesi ya ufisadi ya Sh. bilioni 7.4 dhidi ya Naibu Rais Rigathi Gachagua na wengine tisa.

Katika uamuzi huo, hakimu Victor Wakumile alikubali ombi la Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) huku akiwaonya washtakiwa kwamba wanaweza kukamatwa tena iwapo wapelelezi watapata ushahidi wa kuwashutumu.

Ofisi ya DPP ilituma maombi ya kufuta kesi hiyo kwa sababu ya ukosefu wa ushahidi, na kuwalaumu wapelelezi wa polisi kwa kutokamilisha uchunguzi.

Mwendesha mashtaka wa umma hivi karibuni alikosolewa kwa kuondoa kesi za ufisadi dhidi ya watu mashuhuri, wakiwamo mawaziri.

Awali Naibu Rais alikuwa amekanusha mashtaka yaliyotolewa dhidi yake alipokuwa mbunge, akisema kuwa yalichochewa kisiasa. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**BRAYAN EPIMACKI VITALIS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S2380.0048.2018.** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **OKAONI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/MPW/RB/437079/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMMED ENTREPRISES (T) LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BAJAJ BOXER BM 150X** yenye usajili namba **MC325 CGQ** , CHASSIS NAMBA: **MD2A21BY5KWC91664** na ENGINE NAMBA: **PFZWKB36711.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/419260/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HENRY GEORGE MKOMA,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya **TOYOTA ALTEZZA** yenye usajili namba **T292DNE**, CHASSIS **NO SXE100019930,** ENGINE NO **3S9389589** yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo Chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD /RB /183416/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**Aneth Koku Bairu** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya TVS KING yenye usajili namba **MC961BRJ,** CHASIS NAMBA; **MD6M14PK8H4A55485** na ENGINE NAMBA: **OK4AH4874613.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **GER/TR/RB/123/2022**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SINGIDA LILILOPO SINGIDA**

**MAOMBI MADOGO NA. 74 ya 2022**

**JUMA ABUSHIRI ................................MWOMBAJI NA. 1**
**SALEHE KABAMA ........................... MWOMBAJI NA. 2**

**DHIDI YA**

**OMAR SAKILU SOMBI ........................ MJIBU MAOMBI**

**KWA: OMARI SAKILU SOMBI**
**POPOTE ULIPO TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji tajwa hapo juu ameleta maombi yake hapa Barazani ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo yanapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria hapa Barazani tarehe 08/12/2022 saa 2:00 asubuhi siku ya kutajwa shauri hilo.
Unatakiwa uhudhurie mwenyewe au mwakilishi wako anaetambuliwa kisheria siku na saa tajwa hapo juu.
**ANGALIA:** kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itapangwa na kusikilizwa upande mmoja tu na uamuzi kutolewa bila ya wewe au mwakilishi wako kuwepo.
**HATI** hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Baraza hii leo tarehe 07 mwezi wa Novemba, 2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SINGIDA.

**TEGEMEZA AUCTION MART LIMITED**
**P.O.BOX 77593, MBEZI BEACH, DSM**

**TANGAZO LA MNADA NA NOTISI**

**Kesi namba 208/2021**
**Mdai: ABDALLAH MUSHINI SHARIF**
**MDAIWA: ANGEL MWANGA**

Kwa mamlaka tuliyopewa na mahakama ya mwanzo KIMARA /SINZA MANZESE kutakuwa na mnada wa hadhara.

| TAREHE -MUDA | MAHALI PA MNADA | AINA YA MALI |
|---|---|---|
| 15/11/2022 SAA 4:00 asubuhi | Mbezi Beach Tangi bovu | Gari Alphard Namba T 324 DXX |
| 15/11/2022 Saa 4:00 asubuhi | Mbezi beach Tangi bovu | Suzuki Grand Namba T 936 BCQ |

**Masharti ya mnada**
- Unalipa asilimia 25 siku ya mnada na baada ya siku 14 unamalizia 75% kama utashindwa kumaliza pesa ya awali haitarudishwa.
- Mali inauzwa kama ilivyo .
- Kubadili kadi ni gharama za mteja .

**Kwa mawasiliano zaidi 0719-187677.**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# YOUNG LUNYA: MIMI NDIO MANGWEA

WAKATI leo Novemba 11 rapa Young Lunya akitarajia kuachia wimbo wake mpya, amesema watu sasa watamuelewa kwanini atajiita Albert Mangwea wa sasa.

Young Lunya ataachia ngoma hiyo leo baada ya kuwa kimya kwa muda mrefu na amebainisha kuwa itakuwa moto balaa.

"Kesho(leo) nitaachia ngoma yangu mpya niliyoipa jina la Simu na watu wataelewa kwanini najiita jina la marehemu Albert Mangwea wa kisasa," aliandika kupitia ukurasa wake wa Instagram.

"Mimi ndio Mangwea wa kisasa," alitamba Young..

# Rapa TakeOff kuzikwa leo

**GEORGIA,** Marekani

WAKATI rapa Kirshnik Khari Ball maarufu kama 'TakeOff' anatarajiwa kuzikwa leo Novemba 11, mamlaka ya Uwanja wa State Farm Arena uliopo jijini Atlanta Georgia, Marekani umetangaza kuwa tiketi maalum kwa ajili ya kuhudhuria shughuli ya mazishi zimeisha, kwa mujibu wa MTZ.com.

Rapa huyo anatarajiwa kuzikwa leo Novemba 11 jijini humo baada ya kupigwa risasi wiki iliyopita.

Wananchi wa Atlanta walipata fursa ya kupata tiketi hizo za bure kwa ajili ya kutoa heshima zao za mwisho.

Aidha mamlaka ya uwanja huo imetangaza kwamba haitaruhusu zawadi au chochote kuwekwa nje ya uwanja au ndani. Pia simu na kamera vimepigwa marufuku.

Takeoff alipigwa risasi Novemba 1 mwaka huu na kufariki dunia akiwa na wasanii wenzake.





# *Harmonize ajivunia Made For Us ilivyomnoa*

NYOTA wa muziki wa Bongofleva, Rajab Abdul Kahali maarufu kama Harmonize amesema anajivunia mafanikio ya albam yake mpya ya Made For Us.

Albam hiyo ya tatu ya bosi huyo wa Lebo ya Konde Music Worldwide yenye nyimbo 14 imefanikiwa kupata streams zaidi ya milioni tatu kwenye mtandao wa BoomPlay katika kipindi cha wiki mbili pekee.

Harmonize au Konde Boy amesherehekea mafanikio hayo makubwa na kubainisha kuwa yamemfanya apate hisia za ushindi.

"Hata nikifa leo, najua ninavyohisi kuwa namba moja kwenye mchezo," aliandika Harmonize kwenye mtadano wa kijamii.

Aliongeza kuwa hakuhitaji promosheni ya vyombo vya habari, matangazo mengine yoyote wala machawa kufanikisha ushindi huo.

"Ni Mungu pekee na watu wazuri waliofanikisha," alisema.

Albamu ya nyota huyo pia inaongoza nchini Tanzania kwenye mtandao wa Audio Mack.

Harmonize aliachia albam ya Made For Us mwishoni mwa Oktoba, ikiwa ni ya tatu hadi sasa.

Ngoma zinazopatikana ndani ya albam hiyo ni pamoja na Mwenyewe, My Way, Leave Me Alone, Wote, Nitaubeba, Utanikumbuka, I Miss You, Die, The Way You Are, Miss Bantu, Best Friend, Deka, Too Much na Amelowa.

Harmonize anatoa shukran zake za dhati kwa mchumba wake, Kajala Masanja kwa kumsaidia katika utayarishaji wa albam hiyo.

"Umeifanya akili yangu iwe na utulivu, naweza kutunga mistari inayostahili."

# TINO: NABI SASA AACHWE AFANYE KAZI YAKE

**Na Hadija Mngwai**

BAADA ya Yanga kufanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, kumemuibua nyota wa zamani wa timu hiyo na Taifa Stars, Peter Tino kwa kusema ni vyema sasa kocha Nasreddine Nabi aachwe afanye kazi yake asiingiliwe.

Yanga ilifanikiwa kutinga hatua ya makundi ya mashindano hayo Jumatano baada ya kuifunga Club African ya Tunisia 1-0 nyumbani kwao bao lililofungwa na Stephanie Aziz Ki. Katika mchezo wa kwanza uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zilitoka suluhu.

Akizungumza na Nipashe, Tino alisema kwa sasa kocha Nabi ameanza kukaa sawa na kikosi chake hivyo katika hatua ya makundi waliyoingia hatakiwi kusumbuliwa ili afanye kazi kwa utulivu.

"Watu waliiona Yanga kama ni timu ya kawaida, lakini sio hivyo, ni timu kubwa na yenye ushindani, matokeo kama haya yalishawahi kutokea huko nyuma tulitoka sare hapa nyumbani kisha Mbuyu Twite akaenda kufunga ugenini na tukatinga hatua ya makundi.

"Kwa sasa, Nabi aachwe afanye kazi yake mwanzo alikuwa akisumbuliwa sana, naamini kocha akiachwa kwenye makundi atafanya vizuri sana kwa kuwa Yanga ikitoka kwenye misukosuko ndio inakuwa nzuri zaidi.

"Nabi awali alikuwa hajakaa sawa na kikosi chake wachezaji wengi ni wapya, kwa sasa tayari ameshawajua hivyo kikosi kitakuwa na ushindani," alisema Tino.



Vijana wakionyesha mchezo wa kuzuia pikipiki, wakati wa mahafali ya wanafunzi wa shule za sekondari zinazomilikiwa na Jumuiya za Kiislam katika viwanja vya Garden Ilala, Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Ongala tishio Ligi Kuu, Azam yaiengua Simba*

**Na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa Azam FC Kalimangonga Ongala amefanikiwa kushinda mechi ya tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, huku akiwaambia wachezaji wake wapambane kwa kwa ajili ya nembo ya klabu na si kwa ajili yao binafsi.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Azam Complex, Azam ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji, Ongala mchezaji wa zamani wa Abajalo na Yanga alisema pamoja na ushindi huo lakini kuna vitu ambavyo hakufurahiwa navyo, ingawa walikataa kuvitaja.

"Kulikuwa na faulo nyingi, tulijua watakuja hivyo, baada ya kufunga bao tukarudi chini na hapo ndipo tukawapa nafasi ya kurudi mchezoni, cha muhimu ni kwamba tumeshinda lakini kuna vitu hatukufurahiwa navyo, tumewaambia wachezaji kila mmoja apambane kwa nafasi yake. Apambane kutafuta namba na siyo kwa ajili ya kutafuta sifa zake binafsi," alisema.

Tangu alipoichukua timu hiyo baada ya kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya KMC, Oktoba 21, Kally ameshinda mechi zote tatu alizoisimamia timu hiyo, ikishinda bao 1-0 dhidi ya Simba na Ihefu kabla ya juzi kuifunga Dodoma Jiji mabao 2-1, yaliyotiwa ndani ya nyavu na Ismail Aziz na Idriss Mbombo kwa mkwaju wa penalti, goli la kufutia machozi la Dodoma Jiji likifungwa na Collins Opare.

Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope amesema imewauma kupoteza mechi ambayo walikuwa na uwezo wa kushinda.

Alisema waliwakamata Azam baadhi ya maeneo, lakini kwa bahati mbaya wenzao walipata penalti dakika za mwisho wakapata bao la pili.

"Tuliwasoma tukajua mapungufu yao, wanatumia mipira mirefu kwa sababu wana mastraika wenye uwezo wa kwenda juu, lakini tulikuwa tunagombea mipira inayodondoka, hapo kwenye kugombea mipira iliyodondoka ndipo tuliwaweza, lakini kwa bahati mbaya wenzetu wakapata penalti ikatumaliza," alisema Liogope.

Matokeo hayo yameifanya Azam kuiengua Simba kwenye nafasi ya pili hadi ya tatu. Azam sasa imejikita kwenye nafasi ya pili ikiwa na pointi 20 kama kinara Yanga lakini imezidi michezo miwili mbele, Simba ikiwa nafasi ya tatu na pointi zake 18..

## Odhiambo: Tatizo la Prisons ni muunganiko

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Prisons, Patrick Odhiambo amesema kutokuwa na muunganiko wa kikosi chake ni sababu kubwa ya kutopata matokeo mazuri ya michezo waliyocheza ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Prisons imecheza michezo 10, ikishinda tatu, sare tano na wakipoteza mbili wakiwa nafasi ya nane katika msimamo wa ligi hiyo. Akizungumza na gazeti hili jana, Odhiambo alisema anakiri timu yake haikuanza vizuri msimu huu sababu ya kutokuwa na muunganiko mzuri.

Alisema anaimani na wachezaji waliopo katika kikosi chake kwa sababu ya kuendelea kufanyia kazi mapungufu ya timu yake na kujenga muunganiko katika mazoezi.

"Ni kweli timu yangu haina muunganiko mzuri kwa wachezaji wapya na wale wa msimu uliopita, ninaimani tunaenda kutengeneza timu kidogo kidogo," alisema Odhiambo.

Alisema wanaendelea kufanyia kazi mapungufu yao kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika michezo ijayo ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo.

Odhiambo alisema wanapambana kutafuta pointi kila mechi katika mechi za mzunguko wa kwanza ili hapo baadae wasije kucheza kwa presha kubwa ya kukinusuru kubaki katika ligi.

## Kocha Singida Big Stars alia na sare

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Singida Big Stars limesema kukosa Pointi tatu katika mchezo wao walioucheza juzi dhidi ya Simba kumewaathiri kwa kiasi kikubwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha mkuu wa timu ya Singida, Hans Pluijm alisema wachezaji wake kipindi cha kwanza walicheza vizuri, lakini kipindi cha pili walifanya makosa na wapinzani wao wakaweza kupata goli la kusawazisha.

"Kukosa pointi tatu katika mchezo wetu wa jana (juzi) kumetuathiri kwa kiasi kikubwa, kwani wachezaji wangu walishindwa kufuata vema maelekezo niliyowapa," alisema Pluijm.

Alisema hajaridhishwa na sare waliyoipata kwani alitarajia kupata pointi tatu akiwa kwenye uwanja wa nyumbani.

Alisema mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani na kuahidi kuyafanyia kazi makosa yote aliyoyabaini katika mchezo huo.

Aliongeza kuwa kwa sasa anajipanga kwa ajili ya michezo mingine ijayo na kuomba wachezaji kuwa makini pindi anapowapa maelekezo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN AWINDWA MAN
MSHAMBULIAJI wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23, yuko kwenye rada za Manchester United wanaotafuta mshambuliaji kwa ajili ya msimu ujao. (*Manchester Everning*)

### OSIMHEN AGOMBEWA
MANCHESTER United inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Real Madrid kwa usajili wa Victor Osimhen, huku kocha Carlo Ancelotti akijaribu kumshawishi rais wa mabingwa hao wa Hispania, Florentino Perez kumsajili pamoja na mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23 Januari. (*Sport via Mail*)

### FERNANDEZ AWANIWA MAN
KLABU ya Manchester United pia ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 21 kutoka Benfica. (*Record*)

### MOUKOKO ATAKIWA LIVERPOOL
LIVERPOOL inavutiwa na mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Youssoufa Moukoko mwenye umri wa miaka 17, ambaye amefunga mabao sita katika mechi 13 msimu huu. (*Bild*)

### NEWCASTLE KUBORESHWA
WAMILIKI wa Newcastle United wako tayari kutumia pauni milioni 70 kwa ajili ya usajili msimu huu wa joto ili kuendelea kuimarisha kikosi chao. (Sun)

### BAYERN HAIJASHAWISHIKA
KLABU ya Bayern Munich haijashawishika kuhusu uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa England na Tottenham Hotspur, Harry Kane licha ya ripoti za mwezi uliopita kudokeza kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 ndiye anayepewa kipaumbele na klabu hiyo ya Ujerumani. (*Bild, via The Sun*)

### PERRONE ANYATIWA
KLABU ya Newcastle United inajiandaa kuwasilisha ofa kwa kiungo wa kati wa Velez Sarsfield raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 19, Maximo Perrone. (*Express*)

### PELLISTRI HATAKI KURUDI
KIUNGO wa kati wa Uruguay, Facundo Pellistri mwenye umri wa miaka 20 anataka kuondoka Manchester United moja kwa moja baada ya kukamilisha kipindi cha mkopo katika klabu ya Alaves ya Hispania. (Mail)

### CONTE KUBAKI
ANTONIO Conte anatarajia kubakia Tottenham Hotspur na atasaini mkataba mpya, amesema msaidizi wake Cristian Stellini. (*Evening Standard*)

### KONE ASAKWA
KIUNGO wa Ufaransa, Borussia Monchengladbach, Kouadio 'Manu' Kone anasakwa na West Ham katika dirisha la Januari. (*Bild*)

### ARSENAL WAKOMAA NA MUDRYK
ARSENAL iko tayari kutoa kitita kinachotakiwa na Shakhtar Donetsk cha pauni milioni 56 kwa winga wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21. (*Give me Sport*)

### DIAZ ATAKIWA WOLVES
KOCHA mpya wa Wolves, Julen Lopetegui ana nia ya kuwasajili beki wa Hispania, Nacho Fernandez mwenye umri wa miaka 32 na mshambuliaji raia wa Dominica, Mariano Diaz mwenye umri wa miaka 29 kutoka Real Madrid. (*Goal*)

## DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA



# SCALONI AMTAKA MESSI KOMBE LA DUNIA 2026

## ●●● Akitunzwa vizuri anaweza kucheza mashindano hayo katika umri wa miaka 39...

**BUENOS AIRES,** Argentina

LIONEL Messi alitangaza kwamba, kombe la Dunia la Qatar 2022 litakuwa la mwisho kwake, lakini kocha mkuu wa Argentina, Lionel Scaloni ana matumaini haitakuwa hivyo.

Mshambulizi huyo wa Paris Saint-Germain, Messi atashiriki katika mashindano hayo makubwa zaidi ngazi ya kimataifa kwa mara ya tano wakati michuano hiyo itakapoanza wiki ijayo.

Messi, ambaye atatimiza umri wa miaka 39 wakati wa kombe la Dunia la mwaka 2026, alisema katika mahojiano mwezi uliopita kwamba, hili litakuwa "Kombe langu la Dunia la mwisho, hakika, ndio".

Hata hivyo, Scaloni ana matumaini nyota huyo wa zamani wa Barcelona bado atakuwa na sehemu ya kuichezea Argentina iwapo watafuzu kwa fainali zijazo zitakazoandaliwa na nchi tatu, Canada, Mexico na Marekani.

"Linaweza kuwa Kombe lake la mwisho la Dunia, lakini natumaini sivyo," alisema Scaloni akiiambia CNN. "Ana furaha uwanjani na huwafurahisha watu wengi.

"Iwapo tutamtunza na kumbeba inavyotubidi, kuna uwezekano wa michezo mingi zaidi, kwa sababu ulimwengu wa soka unaomba."

Messi ana jumla ya mabao 26 na asisti za PSG msimu huu - Erling Haaland pekee na mchezaji mwenzake Neymar wanaweza kufikia kati ya wachezaji kutoka ligi tano bora za Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 anauguza jeraha la kifundo cha mguu ambalo lilimweka nje ya ushindi wa PSG wa 2-1 dhidi ya Lorient wikendi iliyopita, lakini Scaloni hana wasiwasi wowote kuhusu utimamu wake wa mwili.

"Hakuna mchezaji ambaye atafikia asilimia 100 kabla ya Kombe la Dunia," alisema. "Tutafanya kila tuwezalo katika wiki ya mwisho kabla ya mchuano kusaidia kila mchezaji.

"Kuna baadhi ambao hawatacheza mechi za mwisho (kwa klabu zao) kama tahadhari, lakini tunajua wako sawa."

Messi amefunga mabao sita kwenye Kombe la Dunia, lakini bado hajazifumania nyavu katika dakika 756 za mchezo katika hatua ya mtoano ya mashindano hayo.

Messi alikaribia zaidi kubeba taji hilo mwaka 2014 wakati Argentina ilipotinga fainali huko Brazil, ambapo walifungwa na Ujerumani.

Alifunga (manne) na kusaidia (moja) mabao matano kati ya nane ya timu yake katika michuano hiyo kuelekea kushinda tuzo ya mpira wa dhahabu kwa kuwa mchezaji bora wa fainali hizo.

Argentina haikufua dafu katika michuano ya Urusi 2018, ambapo walishindwa na Ufaransa katika hatua ya 16 bora, lakini wanaelekea Qatar kama moja ya timu zinazopewa nafasi kubwa ya kutwaa taji hilo.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,048,8
MECHI KALI
GEITA GOLD FC
VERSUS
KMC
1 | 2.28
X | 2.85
2 | 3.55
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LUKAKU HATARINI KUKOSA KOMBE LA DUNIA

**BRUSSELS,** Ubelgiji

ROMELU Lukaku yuko hatarini kukosa Kombe la Dunia kwa sababu ya jeraha la paja, huku kocha wa Ubelgiji, Roberto Martinez akionya kwamba hayuko tayari kutomchagua mshambuliaji huyo wa Inter Milan kama akiwa bado hajawa fiti.

Lukaku, ambaye amefunga mabao 57 katika mechi zake 60 zilizopita za kimataifa, tayari ameshuhudia msimu wake wa 2022/23 wa klabu ukitatizwa na matatizo ya misuli ya paja.

Jeraha hilo limesababisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kucheza mara nne pekee katika mashindano yote akiwa na Inter hadi sasa msimu huu.

Lukaku yupo kwa mkopo kwa Nerazzurri hao baada ya kushindwa kurejea Chelsea, alirudi uwanjani dhidi ya Sampdoria mwishoni mwa Oktoba, lakini ikabidi akose mechi dhidi ya Bayern Munich, Juventus na Bologna mwezi huu kutokana na majeruhi.

Mchezaji huyo wa zamani wa Everton na Manchester United alikuwa mbioni kushiriki Kombe lake la tatu la Dunia baada ya kucheza mwaka 2014 na 2018, lakini sasa uhusika wake uko shakani.

Martinez amethibitisha kwamba atamchagua Lukaku ikiwa yuko fiti kutosha kucheza angalau moja ya mechi tatu za makundi za Ubelgiji.

Hiyo ina maana kwamba yuko katika kinyang'anyiro dhidi ya wakati, huku Mashetani Wekundu hao wakimaliza raundi ya kwanza Desemba 1 watakapomenyana na Croatia.

"Ikiwa wafanyakazi wa matibabu wataamua kuwa Lukaku hatakuwa sawa hadi raundi ya mtoano, hataenda Qatar," alisema Martinez akinukuliwa na L'Equipe.

"Kwa sasa hapatikani na yuko mikononi mwa madaktari. Ikiwa yuko katika nafasi ya kushiriki katika moja ya mechi tatu za kwanza, Romelu ni mchezaji tunayemhitaji.

"Kama hawezi kucheza hatua ya makundi, hatakuwa nasi. Tunafanya kazi siku baada ya siku, lakini hivi sasa uamuzi ni wa kimatibabu kabisa, tunamfahamu vizuri na tunaona dalili mbalimbali za kuboresha."

# *Blatter: Qatar haikupaswa kuandaa Kombe la Dunia*

**GENEVA,** Uswisi

RAIS wa zamani wa Shirikisho la soka la Kimataifa, Fifa, Sepp Blatter amesema uamuzi wa kuipa nafasi nchi ya Qatar kuandaa michuano ya Kombe la Dunia la 2022 ulikuwa ni "kosa".

Blatter mwenye umri wa miaka 86, alikuwa rais wa Fifa wakati Qatar ilipotunukiwa nafasi ya kuandaa mashindano hayo mwaka 2010.

Nchi hiyo ya Ghuba imekosolewa kwa msimamo wake kuhusu, rekodi ya haki za binadamu na kuwatendea isivyo haki wafanyakazi wahamiaji.

"Nchi ni ndogo sana. Soka na Kombe la Dunia ni kubwa mno," alisema Blatter akiliambia gazeti la Uswisi la Tages Anzeiger.




Kombe la Dunia la Qatar, ambalo ni la kwanza kuandaliwa Mashariki ya Kati katika historia ya miaka 92 ya michuano hiyo na la kwanza wakati wa majira ya baridi kali ya Ukanda wa Kaskazini, litafanyika kuanzia Novemba 20 hadi Desemba 18 mwaka huu.

Blatter alisema Fifa ilirekebisha vigezo vilivyotumika kuchagua nchi zinazoandaa kombe la dunia mwaka 2012 baada ya kuibuliwa wasiwasi kuhusu jinsi wanavyotendewa wafanyakazi wahamiaji wanaojenga viwanja vya Kombe la Dunia nchini Qatar.

"Tangu wakati huo, masuala ya kijamii na haki za binadamu yanazingatiwa," aliongeza.

Sepp Blatter alijiunga na Fifa kama mkurugenzi wa ufundi kwa mara ya kwanza mwaka 1975 na alichaguliwa kuwa rais mwaka 1998.

Blatter alitumia miaka 17 akiwa rais wa Fifa, lakini alilazimika kuachia ngazi mwaka 2015 kwa madai kwamba alipanga kinyume cha sheria uhamisho wa faranga milioni mbili za Uswizi (sawa na dola milioni 2.19) kwa rais wa zamani wa Uefa, Michel Platini, ambaye pia alilazimika kujiuzulu nafasi yake kwenye Fifa.

Awali alifungiwa kwa miaka nane, baadaye ikapunguzwa hadi sita..

375,802/-

# SIMBA QUEENS HAIKUWA NA BAHATI - KOCHA

**NA SOMOE NG'ITU,** RABAT

WAKATI Idara ya Ufundi ya Mamelodi Sundowns Ladies ikikiri imekutana na mechi ngumu, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema kikosi chake kilishindwa kutumia vyema nafasi za kufunga walizotengeneza na kupelekea kushindwa kutinga fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake yanayoendelea nchini Morocco.

Simba Queens ambayo juzi ilifungwa bao 1-0 na mabingwa watetezi wa michuano hiyo sasa kesho itakutana na Bayelsa Queens kutoka Nigeria katika mechi ya kusaka mshindi wa tatu, lakini wote wataambulia zawadi ya Dola za Marekani 200,000.

Lukula aliliambia gazeti hili jana timu yake haikuwa na bahati kwa sababu nafasi mbalimbali walizotengeneza walishindwa kuzitumia lakini pia akiwalaumu waamuzi walikuwa upande wa wapinzani wao.

"Mwamuzi pia hakuwa upande wetu, aliwapa kadi nyingi wachezaji wangu ili kuwapunguza kasi na aliwaonya kwa mdomo wapinzani wao, hata Oppah alipofanyiwa faulo hakuchukua hatua yoyote na kupelekea wao kwenda kufunga bao," aliongeza Mganga huyo.

Alisema ameshayabaini mapungufu yake na anaamini akipata mshambuliaji mwingine atakayesaidiana na Oppah Clement katika safu hiyo watafunga mabao mengi na kuisaidia timu kufikia malengo yake.

"Hatukua na bahati, tulikuwa na tatizo katika umaliziaji, tumetengeneza nafasi nyingi hasa katika kipindi cha pili lakini tulishindwa kufunga, hatukua na bahati ya kufunga mabao mengi katika mashindano haya, " alisema Lukula.

Hata hivyo kocha huyo aliwapongeza wachezaji wake kwa namna walivyopambana kusaka ushindi katika mechi zote walizocheza na kinachofuata ni kuhakikisha wanashinda mechi ya kesho na kurejea nyumbani na medali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Akademi za Klabu ya Mamelodi Sundowns inayoshiriki Ligi Kuu ya Afrika Kusini, Shawn Bishop, aliwapongeza Simba Queens kwa ushindani waliouonyesha na kuitabiria makubwa siku zijazo.

Bishop alisema Mamelodi Sundowns Ladies haijawahi kucheza mechi ngumu kama waliyokutana nayo juzi na kupitia mchezo huo wamebaini mapungufu ya kikosi chao na watayafanyia kazi.

"Hatujawahi kucheza mechi ngumu kama hii, ni mara ya kwanza kukutana na changamoto hii, ninawapongeza sana, niko tayari kusema mbele ya benchi lenu la ufundi na kuwapa video ya tathmini ya mchezo tutakayofanya," Bishop alimweleza Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez.

Kiongozi huyo alisema pia atafurahi kuona Simba Queens na Mamelodi Sundowns Ladies zitakutana katika mechi za kirafiki na hii itawasaidia kujiimarisha katika kuanza kwa michuano ya msimu ujao. Aliongeza soka la wanawake Afrika limekua na hii imetokana na uwekezaji unaofanywa na wamiliki wa klabu kwa kushirikiana na vyama vya michezo vya nchi husika.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Asha Djafari (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Mamelodi Sundowns Ladies, Karabo Makhurubetshi katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan juzi usiku. Simba Queens ilifungwa bao 1-0. **PICHA: SOMOE NG'ITU.**

## Fetty Densa wa Simba Queens atakiwa Mamelodi

INATOKA UK 32

Simba Queens itashuka dimbani tena kesho kusaka nafasi ya mshindi wa tatu kwa kuwakabili Bayelsa Queens kutoka Nigeria wakati fainali za mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zitachezwa Jumapili kwa kuwakutanisha ASFAR FC dhidi ya Mamelodi Sundowns Ladies, ambao ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo.

Bingwa wa michuano hiyo inayodhaminiwa na UMBRO na Tiktok atapata zawadi ya Dola za Marekani 400,000 huku mshindi wa pili ataondoka na Dola za Marekani 250,000 na itakayomaliza ya tatu na ya nne zitapewa Dola za Marekani 200,000 kila moja.

## *Nabi: Tuliwakamata hapa Club Africain*

INATOKA UK 24

Alisema katika chakula hicho kitakuwa na mambo mengi ikiwemo suala la bonasi ambalo wachezaji waliahidiwa na kupatiwa fedha hizo.

"Ni kweli wachezaji waliahidiwa fedha kama bonasi baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya makundi, jambo hilo litafanyika baada ya kutua nchini," alisema kiongozi huyo.

Kikosi cha Yanga kiliondoka Tunisia jana saa 11 jioni kwa saa za Tanzania na kulala Dubai na asubuhi ya leo wataanza safari ya kurejea Tanzania kwa ajili ya maandalizi ya michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga wataondoka saa 3 usiku wa leo kuelekea Mwanza na tayari kwa ajili ya mechi yao ya ligi dhidi ya Kagera Sugar, mchezo utakaopigwa Jumapili hii, uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Crystal Palace | 3.04 | 3.19 | 2.37 |
| 02. 12/11/22 | 18:00 | Bristol City vs Watford | 2.89 | 3.39 | 2.36 |
| 03. 12/11/22 | 18:00 | Bournemouth vs Everton | 2.78 | 3.23 | 2.53 |
| 04. 12/11/22 | 18:00 | Huddersfield vs Swansea | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 05. 12/11/22 | 18:00 | Preston vs Millwall | 2.41 | 3.13 | 3.03 |
| 06. 12/11/22 | 18:00 | Coventry vs QPR | 2.36 | 3.22 | 3.02 |
| 07. 12/11/22 | 20:00 | Basaksehir vs Galatasaray | 2.42 | 3.40 | 2.80 |
| 08. 12/11/22 | 20:00 | Sampdoria vs Lecce | 2.54 | 3.08 | 2.89 |
| 09. 12/11/22 | 20:00 | FC Sion vs St. Gallen | 2.80 | 3.60 | 2.37 |
| 10. 12/11/22 | 20:30 | Newcastle vs Chelsea | 2.32 | 3.34 | 2.99 |
| 11. 12/11/22 | 22:45 | Bologna vs Sassuolo | 2.38 | 3.34 | 2.89 |
| 12. 13/11/22 | 14:30 | Atalanta vs Inter | 2.90 | 3.54 | 2.29 |
| 13. 13/11/22 | 16:15 | FC Zurich vs Servette Geneva | 2.37 | 3.30 | 2.95 |
| 14. 13/11/22 | 17:00 | Istanbulspor vs Hatayspor | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 15. 13/11/22 | 17:00 | Kayserispor vs Konyaspor | 2.58 | 3.28 | 2.68 |
| 16. 13/11/22 | 17:00 | Montpellier vs Reims | 2.45 | 3.38 | 2.73 |
| 17. 13/11/22 | 17:30 | Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.44 | 3.41 | 2.72 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 11/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5958 | Torpedo Kutaisi vs FC Gagra | 1.53 | 3.90 | 5.26 |
| 13:30 | 5586 | Keshla FK vs FK Sumgayit | 2.87 | 3.12 | 2.32 |
| 14:00 | 2703 | South Korea vs Iceland | 1.42 | 4.36 | 7.91 |
| 15:00 | 3843 | Prachuap FC vs Ratchaburi | 2.96 | 3.16 | 2.24 |
| 15:45 | 3562 | Shabab AL Ahli Dubai Club vs Al Nasr Dubai | 1.57 | 4.09 | 4.58 |
| 15:45 | 5363 | AL Khaleej Khor Fakkan vs Al Dhafra | 1.69 | 3.89 | 3.98 |
| 16:00 | 2286 | Kustosija vs Croatia Zmijavci | 2.07 | 3.17 | 3.31 |
| 16:00 | 2974 | Thagafi Tulkarem vs Hilal Al-Quds | 4.50 | 3.75 | 1.71 |
| 16:00 | 2985 | Shabab Alsamu vs Shabab AL Amari | 1.80 | 3.80 | 4.00 |
| 16:00 | 4057 | Ethiopian Medhin vs Ethiopia Electricity | 2.14 | 3.07 | 3.26 |
| 16:00 | 5073 | Geita Gold FC vs KMC | 2.28 | 2.85 | 3.55 |
| 17:00 | 2154 | Bengaluru FC vs East Bengal | 1.71 | 3.60 | 4.19 |
| 18:30 | 1340 | Jazira Abu Dhabi vs AL Wahda Scc (UAE) | 2.31 | 3.57 | 2.59 |
| 18:30 | 2103 | Pribram vs MFK Chrudim | 1.98 | 3.34 | 3.39 |
| 18:30 | 2813 | Bahrain vs Canada | 4.85 | 3.74 | 1.71 |
| 18:45 | 2196 | AL Arabi vs AL Qadsia | 2.26 | 3.17 | 2.92 |
| 19:00 | 3282 | Kiyovu Sports vs Rayon Sports FC | 1.81 | 3.08 | 4.50 |
| 19:00 | 5129 | Sidama Bunna SC vs Hawassa Kenema SC | 2.41 | 2.92 | 2.92 |
| 19:00 | 5562 | Nizhny Novgorod vs Akhmat Grozny | 2.88 | 3.23 | 2.36 |
| 19:30 | 4651 | Spartak Trnava vs MFK Skalica | 1.42 | 4.18 | 6.41 |
| 20:00 | 1467 | Alanyaspor vs Adana Demirspor | 2.58 | 3.42 | 2.53 |
| 20:00 | 2593 | Tallinna JK Legion vs Parnu JK Vaprus | 2.00 | 3.59 | 3.11 |
| 20:00 | 3428 | Ankaragucu vs Trabzonspor | 3.37 | 3.37 | 2.07 |
| 20:00 | 3904 | Omonia Nicosia vs Olympiakos Nicosia | 1.56 | 3.90 | 5.80 |
| 20:00 | 4603 | Warta Poznan vs Stal Mielec | 1.84 | 3.26 | 3.99 |
| 20:00 | 5031 | Nea Salamis vs Aris Limassol | 3.85 | 3.50 | 1.91 |
| 20:00 | 5897 | Javor Ivanjica vs FK Napredak | 2.42 | 3.20 | 2.67 |
| 21:30 | 1057 | Neuchatel Xamax vs FC Stade LS Ouchy | 2.77 | 3.50 | 2.21 |
| 21:30 | 1190 | Dunkerque vs Paris 13 Atletico | 1.86 | 3.34 | 4.03 |
| 21:30 | 1658 | FC Versailles 78 vs Saint Brieuc | 1.86 | 3.41 | 3.95 |
| 21:30 | 2993 | Orleans vs Avranches | 1.95 | 3.25 | 3.79 |
| 21:30 | 5611 | Yverdon-Sport FC vs FC Vaduz | 2.07 | 3.74 | 2.86 |
| 22:00 | 1034 | VVV Venlo vs Willem II Tilburg | 3.90 | 3.60 | 1.82 |
| 22:00 | 1123 | PEC Zwolle vs FC Eindhoven | 1.59 | 3.85 | 5.13 |
| 22:00 | 1339 | Heracles Almelo vs NAC Breda | 1.50 | 4.53 | 5.12 |
| 22:00 | 4071 | Sparta Rotterdam vs Twente | 3.16 | 3.46 | 2.11 |
| 22:00 | 4989 | De Graafschap vs Jong PSV | 1.78 | 3.75 | 3.90 |
| 22:00 | 5002 | Telstar vs ADO Den Haag | 2.31 | 3.45 | 2.76 |
| 22:00 | 5212 | FC Oss vs Jong AZ Alkmaar | 2.47 | 3.45 | 2.56 |
| 22:00 | 5695 | Sepsi Osk vs Petrolul Ploiesti | 1.50 | 3.96 | 6.14 |
| 22:30 | 3679 | Wisla Plock vs Cracovia | 2.39 | 3.20 | 2.72 |
| 22:30 | 4147 | Ascoli vs Frosinone | 3.11 | 3.11 | 2.28 |
| 22:30 | 5242 | Monchengladbach vs Borussia Dortmund | 3.02 | 3.71 | 2.09 |
| 22:30 | 5289 | Amstetten vs SKN St Polten | 2.72 | 3.41 | 2.28 |
| 22:45 | 1797 | Coleraine FC vs Glentoran Belfast | 3.36 | 3.46 | 1.95 |
| 22:45 | 3231 | Empoli vs Cremonese | 2.30 | 3.36 | 2.87 |
| 22:45 | 3598 | Hamilton vs Ayr United | 3.30 | 3.45 | 2.03 |
| 23:00 | 1987 | Lyon vs Nice | 1.73 | 3.78 | 4.28 |
| 23:00 | 4232 | Birmingham vs Sunderland | 2.33 | 3.17 | 2.98 |
| 23:15 | 3054 | SCU Torreense vs Vilafranquense | 2.71 | 3.06 | 2.57 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Ijumaa Novemba 11, 2022

Nipashe



Scaloni amtaka Messi Kombe la Dunia 2026 UKURASA 29



Wachezaji wa Simba wakishuka kwenye ndege katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere Dar es Salaam jana, wakitokea mkoani Singida ambako walicheza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania bara dhidi ya Singida Big Stars kwenye Uwanja wa Liti. Timu hizo zilitoka sare ya kufungana bao 1-1. **PICHA: SIMBA**

## Fetty Densa wa Simba Queens atakiwa Mamelodi

**Na Somoe Ng'itu,** RABAT

BEKI tegemeo wa Simba Queens, Fatuma Issa 'Fetty Densa' amewavutia makocha wa Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini na huenda klabu hiyo ikaanza mazungumzo na Wekundu wa Msimbazi, imefahamika.

Mkuu wa Idara ya Ufundi wa Klabu ya Mamelodi Sundowns, Shawn Bishop, alisema Fetty Densa ameonyesha uwezo mkubwa katika mechi zote alizocheza ameisaidia Simba Queens kufika hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake yanayoendelea hapa nchini Morocco.

" Mna wachezaji wazuri, mna timu nzuri sana, niwe mkweli hata kama mmepoteza mechi ya leo (juzi), yule anayevaa jezi namba tano (Fetty Densa) na jezi namba sita ( Philomena Abakah), ni wazuri sana," alisema mkufunzi huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Mamelodi Sundowns Ladies, Jerry Tshabalala, alisema wakati umefika wa Fetty Densa kwenda kucheza Soka la kulipwa nje ya Tanzania.

"Umecheza vizuri sana, umenivutia mnooo, ninaweza kuleta maombi kwa klabu yako kwa ajili ya kukusajili, hongera sana, mmetupa ushindani mkubwa, sijaamini matokeo ambayo tumepata, " Tshabalala alimweleza Fetty Densa maneno hayo baada ya mechi ya nusu fainali kumalizika ambapo Simba Queens ililala kwa bao 1-0.

INAENDELEA UK 31

# Nabi: Tuliwakamata hapa Club Africain

## ●●● Rais Samia atoa kongole, wachezaji walilazimika kubaki uwanjani kwa saa 3 kwa vurugu, kutua leo, kujazwa noti...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amewapongeza wachezaji baada ya kutumia vizuri maelekezo ambayo aliwapa muda mfupi kabla ya mchezo wa marudiano wa kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

Wakati huo huo, Rais Samia Suluhu Hassan ameipa kongole Klabu ya Yanga kwa ushindi huo na kuitakia kila la kheri kwa hatua inayofuata.

"Kongole Yanga kwa ushindi na kufanikiwa kusonga mbele katika michuano ya soka la wanaume kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, msimu wa 2022/2023. Nawatakia kila la kheri katika hatua inayofuata" aliandika Rais Samia kupitia ukurasa wake wa twitter.

Yanga juzi ilifanikiwa kutinga hatua ya makundi baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Watunisia hao katika mchezo uliopigwa uwanja wa Olimpiki wa Hammedi Agrebi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema wapinzani wao walikuwa bora, wao walihitaji kuwashangaza waliokuwa wanaibeza timu hiyo.

Alisema kushinda ugenini na kufuzu ni hatua kubwa ambayo waliamini watafanikiwa kama kila mchezaji atacheza kwa kujituma na kujua umuhimu wa ushindi wa mchezo huo.

"Tulizungumza na kila mchezaji na kumuomba auchukulie mchezo huo kama vita, walifuata na kushirikiana vyema ikiwemo kuwa na nidhamu ya mchezo, tunamshukuru Mungu kwa hilo.

"Shukrani kwa kila mtu aliyefanikisha hili ikiwa ni pamoja na wachezaji wa timu yetu, wafanyakazi wa makocha, na mashabiki wetu wapendwa kwa kutuunga mkono na kutuamini. Tunaendelea kwa hatua inayofuata," alisema Nabi.

Alisema baada ya mchezo huo, Watunisia waliwafanyia fujo kwa kuwarushia, makopo na mawe uwanjani hali ambayo iliwafanya waendelee kukaa uwanjani kwa zaidi ya saa tatu.

"Waarabu hawakuamini kama tumewatoa, walitufanyia fujo sana kabla hatujatoka uwanjani, tunachoshukuru ni kuwa hakuna aliyejeruhiwa," alisema kocha huyo.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi wa mashindano ya Yanga, Saad Kawemba alisema timu inatarajia kutua nchini saa 7 mchana wa leo ikitokea Dubai baada ya hapo itakwenda moja kwa moja kupata chakula cha mchana na viongozi akiwemo mdhamini wao Mkuu, Gharib Said Mohamed, maarufu kama GSM.

INAENDELEA UK 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >